

# Kufundisha Hoja

Taasisi ya Ruhi







Kitabu cha 6

# Kufundisha Hoja

Taasisi ya Ruhi

Vitabu vilivyopo katika Mfuatano:

Hapa chini kuna majina ya vitabu vya sasa vilivyopo katika mfuatano uliosanifiwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vimekusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika jitihada ya hatua kwa hatua ya kuongeza uwezo wa vijana na watu wazima kuhudumia jumuiya zao. Taasisi ya Ruhi pia inaendelea kukuza seti ya kozi ambazo zinachepuka kutoka kitabu cha tatu kilichopo katika mfuatano kwa ajili ya kuwafunza walimu wa madarasa ya Kibahá'í ya watoto, hali kadhalika seti nyingine kutoka Kitabu cha 5 kwa ajili ya kuwainua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Hivi pia vimeainishwa katika orodha hapo chini. Sharti izingatiwe kwamba orodha inaweza kubadilika kadiri tajiriba ugani inavyoendelea, na vitabu vya ziada vitaongezwa kadiri idadi ya vipengele vya mtaala vinavyoendelea kukuzwa vitakapofikia hatua ambapo vitaweza kupatikana wingi.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Tafakari juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Kuinuka Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Kozi ya kwanza ya mchepuo wa Kitabu cha 5* |
| | *Upanuaji Wigo: Kozi ya pili ya mchepuo wa Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Kufundisha Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja Kwenye Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Agano la Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Inayopuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mjadala wa Umma* |

Hakimiliki © 2002, 2024 na Ruhi Msingi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo la 2.1.1.PE kilizochapishwa Desemba 2024
ISBN 978-628-96721-0-7

Kilichapishwa awali kwa Kihispania kama *Enseñar la Causa*
Hakimiliki © 1990, 1998, 2023 na Ruhi Msingi, Colombia
ISBN 978-628-95545-2-6

Taasisi ya Ruhi
Cali, Colombia
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo

Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi ...................... v

Asili ya Kiroho ya Ufundishaji ........................................ 1

Sifa na Mielekeo Muhimu kwa ajili ya Ufundishaji ...... 35

Kitendo cha Ufundishaji ................................................ 77

# Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi

Ni muhimu kwa wale wote wanaohudumu kama wakufunzi wa kozi za Taasisi ya Ruhi kuelewa kwamba *Kufundisha Hoja*, kitabu cha sita katika mfuatano wake mkuu, kinashika nafasi ya msingi katika mchakato wa kielimu ambao washiriki hujihusisha nao. Kwa upande mmoja, pamoja na tajiriba yao iliyolimbikizwa katika uga wa huduma, watakuwa tayari kutafakari kwa mapana zaidi juu ya mada ambayo ilitambulishwa kwao kwa mara ya kwanza katika Kitabu cha 2. Kwa upande mwingine, mada wanazozichunguza hapa zitaweka katika muktadha mengi ya yale wanayoyafanya kuendelea, kwa kuwa maisha yaliyotolewa katika huduma ya Hoja hayana budi kuwa yamejazwa na shauku kubwa ya kupata heshima ya kushiriki mafundisho ya Bahá'u'lláh na wengine.

Tangu kuanza njia ya huduma iliyofunguliwa na kozi, washiriki wamepata kiwango kikubwa cha tajiriba katika kutekeleza, pamoja na marafiki zao, seti ya vitendo vinavyohusiana vya huduma katika vijiji na ujirani wao—wakikaribisha mikutano ya ibada, wakifanya ziara zenye mpangilio za nyumbani, wakifundisha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto, na wakivihusisha vikundi vya vijana chipukizi katika programu kwa ajili ya uwezeshwaji wao wa kiroho. Yakifumwa pamoja na vitendo vyote hivi yamekuwa mazungumzo ambayo yameisaidia idadi inayoendelea kuongezeka kuzijua kanuni za Imani na kuimarisha ufahamu wa mafundisho yake. Kila moja ya kozi zilizotangulia, hususan Kitabu cha 2, imechangia kwenye ukukuzaji wa ule uwezo unaohitajika ili washiriki waweze kuingia katika mazungumzo kama haya. Bila shaka, wengi wao hadi wakati huu pia wamepata baraka ya kuzisaidia roho zingine katika kumtambua Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa wakati huu na katika kuonesha utiifu kwa Imani Yake. Sasa wamejiandaa vyema kufikiria kwa kina zaidi kuhusu kitendo cha ufundishaji, ambacho ndiyo lengo la kitengo cha tatu cha kitabu hiki. Cha pili kitawapa fursa ya kutafakari juu ya sifa na mielekeo ya kiroho ambayo wale wanaofundisha Imani wanapaswa kuwa nayo, ambapo kile cha kwanza kitaongeza uelewa wao wa maana ya kiroho ya kitendo hiki kitakatifu.

Katika kuchunguza asili ya wajibu ulioamriwa na Bahá'u'lláh juu yetu kufundisha Hoja Yake, kitengo cha kwanza kinabeba dhana kadhaa za kimsingi. Miongoni mwa zile zilizotambulishwa awali katika kitengo ni dhana ya "uwakaji". Washiriki wanahamasishwa kutambua kwamba wajibu wetu wa kufundisha unahusu hasa hali yetu ya ndani sawa na vitendo tunavyovitekeleza. Kwamba "kuwa" na "kutenda" ni vipengele viwili vinavyokamilishana vya maisha yanayofuata mafundisho ya Kibahá'í ni mada iliyopo kwenye msingi wa mlolomgo mzima wa kozi. Hapa inawekwa wazi na kwa hakika, inaupa umbo muundo mzima wa kitabu. Sehemu za mwanzo za kitengo hiki zitawasaidia washiriki kupata umaizi wa kiroho kuhusu wazo hili kwa kuwa linahusiana na ufundishaji wa Imani. Sitiari kadhaa zilizomo katika Maandiko zinatumika kuwasaidia kuona uhusiano kati ya "kuwa" na "kutenda"—hasa, taswira ya mwale, ambao haidhuru mdogo kiasi gani, hutoa joto na mwangaza. Kitendo cha ufundishaji, inasemekana ni udhihirisho wa kiasili wa hali ya kuwa, ule ambao unaweza kuelezwa vizuri kabisa kama hali ya uwakaji, ambamo upendo wa Mungu huwaka kwa wangavu mno katika myoyo yetu ambao tunajitahidi bila kuchoka kueneza Neno Lake.

Uelewa ambao washiriki wanaufikia kupitia usomaji wao wa vifungu vilivyomo katika sehemu hii, basi unapaswa uwawezeshe kutambua jinsi ukamilishanaji wa "kuwa" na "kutenda" unavyodhihirishwa katika vitendo kwenye uga wa huduma. Katika hili, matokeo ya dhana fulani fulani za kawaida zinazoshikiliwa ambazo hutenganisha hivi viwili, hususan zile za kidini kitabia, zitahitaji kueleweka kwa washiriki, ikiwa wanataka kuepukana na fikra zenye uwili kutokana na kuathari namna wanavyoyaona maisha yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya kuendeleza Hoja. Mazoezi yaliyopo katika Sehemu ya 9 na 10 yatasaidia katika hali hii, na wakufunzi sharti wahakikishe wanakuwa makini vya kutosha. Bila shaka, washiriki wataona bila wasi wasi kwamba kusudi la kimaadili lenye pande mbili ambalo wamekuwa wakilifuatilia hufungamanisha pamoja kila kipengele cha maisha yao—utafutaji wao wa maarifa, utiifu wao kwa sheria Takatifu, jitihada zao kumtumikia Mungu na kumkaribia Yeye na kupata sifa za kiroho na kurekebisha tabia zao.

Asili takatifu ya wajibu wa kufundisha ni shabaha ya sehemu kadhaa zinazofuata za kitengo. Katika ulimwengu ambamo kutoka humo dhana hasa ya utakatifu inapotea, washiriki wanapaswa kuibuka kutoka kwenye usomaji wao wa kozi pamoja na utambuzi wa papo hapo wa "utakatifu"—kile ambacho ni mali ya Mungu—na pamoja na uelewa wa kina wa dhana kwamba, katika kufundisha Imani, wanaingiliana na na vitu viwili vitakatifu: moyo wa mwanadamu na Ufunuo Wake. Tafakari juu ya vifungu vilivyochaguliwa kutoka Maandiko zitaangazia juu ya kile ambacho ni kitendo cha kiroho hasa—yaani, ufunguzi wa mji wa moyo wa mwanadamu kwa Ufunuo Wake kwa kutumia ufunguo wa usemi. Suala la "usemi" litachunguzwa kwa undani katika kitengo cha tatu, ambapo washiriki watazingatia maudhui ya ujumbe wanaouwasilisha kwa roho nyingine pale wafundishapo. Katika sehemu hii, wanaombwa kufikiria juu ya jinsi ya kuinua ufahamu wa utakatifu wa kitendo hiki hakuongezi tu ufanisi wa jitihada ugani. Bali, na muhimu zaidi, huachilia nguvu za kiroho zinazohitajika kuinua jitihada kama hizo juu ya masuala ya kiulimwengu, hivyo, zikianzisha michakato inayoweza kuleta mabadiliko ya kimsingi ya mtu binafsi na ya pamoja. Katika Sehemu ya 17 washiriki watatumia kiasi fulani cha muda kuchunguza matokeo ya ufahamu huu uliokuzwa. Miongoni mwa mambo ambayo Mkufunzi atataka kuhakikisha yamewafikia, mawili yanajitokeza: Kwanza, watalazimika kuwa waangalifu, wasije wakachukua mielekeo fulani ambayo, ingawa imeenea katika jamii, ingeingiza katika jitihada zao za ufundishaji, mitazamo na desturi ambazo zingehatarisha asili yao takatifu. Kitendo cha ufundishaji hakipaswi kuendewa kana kwamba mtu anaandikisha wajumbe wa hoja endelevu ya kijamii, hata kidogo isifikiriwe katika muktadha wa uuzaji wa bidhaa, haidhuru kina manufaa kiasi gani kwa mtumiaji. Pili, wanapaswa kutambua kwamba, kwa kuwa shughuli zote kwenye njia ya huduma inahusisha kuikutanisha mioyo na Neno la Mungu, hizi, pia, ni takatifu kiasili na zinapaswa kuendewa kwa utambuzi huu.

Kitengo hiki basi hugeukia mada ambayo inafahamika vyema kwa washiriki: athari ibadilishayo ya Neno la Mungu. Katika kitendo cha ufundishaji, uhusiano huundwa kati ya moyo wa mwanadamu na Ufunuo wa Bahá'u'lláh—majaliwa Yake makuu kabisa kwa wanadamu—uhusiano ambao kupitia huo mchakato udumuo wa mabadiliko unaweza kuanza. Neno la Mungu, pekee, limejaliwa nguvu iwezayo kuleta mabadiliko kama hayo. Kwa kiwango chochote kile ambacho washiriki wametafakari juu ya mada hii katika kozi zilizopita, hapa ndipo watajizamisha wenyewe katika Matamshi ya Bahá'u'lláh mwenyewe kuhusu maana ya Neno la Mungu na umuhimu wa kuchota kutoka nguvu yake wakati wanapofundisha Hoja Yake. Mkazo unaotolewa na Taasisi ya Ruhi juu ya kukariri vifungu kutoka Maandiko utakuwa wa lazima zaidi katika akili za washiriki. Kuelezea mafundisho kwa usahihi, kuyatoa kwa wengine jinsi yalivyo, ni miongoni mwa uwezo ambao sote tunatafuta kuukuza kadiri tunavyotembea kwenye njia ya huduma, na hili linahitaji tufanye jitihada wakati wote

kufungamanisha mawazo na maneno yetu kwa ukaribu kabisa na maandiko kadiri iwezekanavyo.

Kitengo hiki huhitimisha, kwa hiyo, huweka wazi kwamba, wakati tunapozungumza na wengine kuhusu Imani, tunapaswa kuchota si tu kutoka kwenye ujuzi tulioupata kwa ajili ya kutoa maelezo ya wazi na yenye kueleweka, bali pia juu ya nguvu ya upendo. Katika muktadha wa ufundishaji, mazungumzoi yanapaswa, pamoja na kupambanuliwa kwa furaha, kuunda na kuimarisha mafundo ya upendo kati ya mioyo ambayo kwayo hisia bora na fikra zenye ufahari sana vinaweza kutiririka.

Kitengo cha pili, "Sifa na Mielekeo Muhimu ya Ufundishaji", huanza kwa kuwakumbusha washiriki kile walichojifunza katika kitengo cha kwanza kinachohusiana na ukamilishanaji wa "kuwa" na "kutenda". Tangu mwanzo husisitiza kwamba uboreshaji wa hali ya ndani ya mtu, kwa kawaida hujidhihirisha katika huduma kwa wengine, wakati wa kuhudumia wengine ndipo hali ya ndani ya mtu mwenyewe inaboreshwa zaidi. Washiriki wanakaribishwa kutafakari juu ya sifa hizo za kiroho kama vile usafi wa moyo, kutojipendelea, imani, wema, ujasiri, hekima, kujitenga, na unyenyekevu kama zinavyofungamana na jitihada zetu za kueneza manukato Matakatifu. Ukuzaji wa sifa za kiroho, pamoja na mielekeo inayolingana, ni mada inayozungumziwa mara kwa mara katika kozi za Taasisi ya Ruhi, lakini daima katika muktadha wa ujenzi wa uwezo maalum—uwezo unaohitajika, kwa mfano kuchangia kwenye tabia ya kiibada ya jumuiya, kushiriki pamoja na wengine lulu za hekima kutoka Ufunuo wa Bahá'u'lláh, kuendesha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto. Kwa namna hii, uelewa wa washiriki wa sifa hizi muhimu za roho ya mwanadamu huongezeka na hujitwalia kina kikubwa zaidi kadiri muda upitavyo, kadiri wachunguzavyo mienendo ya kila moja kwa mtazamo mpya na kushuhudia utendakazi wake katika eneo fulani jipya la utendaji.

Katika kuongoza kikundi kupitia kitengo hiki, mkufunzi atahitaji kukumbuka dhana kuu kwa ajili ya uchunguzi wa sifa za kiroho, ambazo zimo katika kozi zote za mlolongo mkuu, anasonga mbele katika hili—yaani, sifa kama hizo hutegemea moja juu ya nyingine kwa ajili ya udhihirisho wake unaostahili. Jambo lenye umuhimu maalum katika kitendo cha ufundishaji ni uelewa wa jinsi ujasiri unavyohitaji hekima; jinsi hekima inavyobaki bila kudhihirishwa kwa kutokuwepo kwa ujasiri; jinsi usafi unavyohitaji kujitenga na tamaa za kiulimwengu, vile vile kutokuwa na ubinafsi; jinsi wema, usiporekebishwa na imani katika uwezo wa watu, unaweza kufunikwa na ubaba au jinsi, bila uaminifu, kiuhalisia, si kingine bali unafiki.

Wakufunzi hadi sasa wanalijua wazo hili, lililoelezewa katika Kitabu cha 3, kwamba sifa za kiroho ni ile miundo ya kudumu inayotuainisha jinsi tulivyo kama wanadamu. Upataji wa sifa hizi hutuwezesha kuonesha mielekeo ifaayo katika miingiliano yetu na wengine na kuepukana na ile isiyofaa ambayo pengine tumeipata kupitia malezi na utamaduni wetu. Uwazi wetu kuelekea watu na huruma tuliyonayo juu ya mapambano yao ya kuelewa ukweli ni mifano ya mielekeo inayoathiri ufundishaji. Kile ambacho wakufunzi wote wanahitaji kukitambua ni kwamba mjadala juu ya mielekeo umejengwa ndani ya uchunguzi wa sifa za kiroho ambazo ndiyo shabaha ya sehemu kubwa ya kitengo hiki. Kwa mfano, wakati wa kufikiria kuhusu sifa ya wema na subira katika Sehemu ya 7, washiriki huchambua hali ambamo mielekeo ya ubaba na kutowajibika inaweza kujidhihirisha yenyewe katika jina lao. Vivyo hivyo, baada ya kutafakari juu ya ubora wa kujitenga katika Sehemu ya 8, wataombwa kufikiria jinsi inavyohusika na shauku yetu ya kufundisha, matamanio ya hali ya juu ambayo sote tunayatamani. Washiriki sharti waweze kubaini ari na shauku kama mielekeo wanayopaswa

kujitahidi kuonesha na kukubali kuwa kutokujali na utepetevu kama ile ambayo wataipinga. Hili ndilo kusudi la zoezi la Sehemu ya 9, ambalo linapaswa kuwa somo la fikra makini.

Wale wanaohudumu kama wakufunzi, bila shaka wanatambua pia kwamba ukuzaji wa sifa yoyote ya kiroho huhusisha uelewa wa idadi kadhaa ya dhana zinazohusiana. Tukichukua mfano mmoja, ufikiaji wa viwango vya juu zaidi na zaidi vya usafi, unahitaji uelewa fulani wa kile ambacho moyo wa mwanadamu umeumbwa kukiakisi, wa kile kinachofanyiza vumbi na uchafu ambavyo vinaweza kuficha wangavu wake, na wa kile kinachohitajika kuufanya uendelee kusafishwa kutoka takataka kama hizo. Lakini, mbali na uelewa unaoendelea kuongezeka wa dhana kama hizo, mtu lazima awe na nia na shauku ya kweli kuendelea kiroho. Nia na shauku haijengeki kwa majadiliano ya kitaaluma tu, kuna haja ya tafakari ya kina na ya undani zaidi kwa kila mtu kuhusu hali yake ya ndani. Ni kazi ya kila mkufunzi, kwa hiyo, kujenga mazingira rafiki ya tafakari kama hiyo—mazingira ambayo hayaibui hisia ya hatia, ambayo hayahitaji maungamo, ambayo hayahamasishi tuhuma, yale ambamo kikundi cha marafiki wanaweza kujadiliana bila jazba juu ya masuala yote mawili ya kinadharia na ya kivitendo, yakimwacha kila mmoja kutafakari kwa faragha juu ya kile kinachohitajika kutoka kwake.

Sifa moja ya kiroho ambayo huhitaji uangalifu maalum ni unyenyekevu. Kwa upande mmoja, unyenyekevu wa kweli una uhusiano wa karibu sana kwa hali ya uwakaji ambayo sisi sote tunajitahidi kuifikia. Ili kufikia vilele vyake huhitaji kwamba tuendelee kusahau kabisa nafsi zetu wenyewe. Ni sifa inayoyapa maneno na vitendo vyetu uwezo wa kiroho na hutulinda dhidi ya mashambulizi ya kiburi na majigambo. Kwa upande mwingine, husababisha mwelekeo wa ujifunzaji ambao ni wa lazima sana kwa ajili ya ufundishaji unaofaa. Mwelekeo wa ujifunzaji uliojengwa juu ya msingi wa unyenyekevu wa kweli hulinda dhidi ya ung’ang’anivu katika mbinu na njia tunazotumia tunapofundisha Imani, kwa yote mawili katika jitihada zetu wenyewe na katika mchango wetu kwa shughuli za pamoja; inatusaidia kuwa hodari zaidi na zaidi katika kuitikia ipasavyo hali ambamo tunajikuta wenyewe—iwe kuendelea mbele kwa ujasiri au uangalifu, iwe kutenda kwa haraka au pole pole, iwe kuongea moja kwa moja na kwa uhakika kuhusu utu wa Bahá’u’lláh au kwa kawaida zaidi kuhusu mafundisho na kanuni Zake Alizitangaza. Majadiliano ya mawazo haya yanaanza katika Sehemu ya 10 na kumalizika na mazoezi katika Sehemu ya 14. Kama kawaida, mfano wa ‘Abdu’l-Bahá, ambao kwao kitengo huishia, utawaongoza washiriki katika tafakari zao juu ya sifa na mielekeo ambayo sharti ipambanue jinsi wanavyotenda pamoja na roho pokevu na wanavyoyaendea mazungumzo yao kuhusu Imani.

Kitengo cha tatu, kinachoongelea kitendo chenyewe cha ufundishaji, hushughulikia mada hii katika miktadha miwili: katika juhudi zetu wenyewe kama watu binafsi na katika jitihada za pamoja mashinani. Sehemu kubwa imewekwa kwa ajili ya ule wa kwanza, lakini wakufunzi sharti wakumbuke kwamba mengi ya watayojadili na washiriki yanahusu pande zote mbili sawa sawa. Kwa hakika, wakati kitengo hiki kinazingatia kila mmoja kwa zamu, kiuhalisia haijatenganishwa mmoja na mwingine bali inaingiliana kwa namna nyingi.

Miongoni mwa uwezo ambao kitengo kinapendekeza washiriki kuukuza ili wawe na ufanisi katika muktadha mmojawapo ni ule wa kutambua na kulea upokevu kwa ujumbe wa Bahá’u’lláh. Katika hili, sifa za kiroho ambazo zilikuwa shabaha ya kitengo cha pili zitakuwa ufunguo, kama ilivyoonwa na Mlinzi katika kifungu kilichopo Sehemu ya 3, kama utakavyokuwa uwezo wa kutumia fursa zilizoletwa na ghasia zilizopo katika jamii wakati huu. Katika majadiliano yao, washiriki wanapaswa kufikiria vya kutosha juu ya hali zinaoibuka

katika moyo wa mwanadamu chini ya msongo wa mawazo na madhara ya utaratibu umomonyokao wa ulimwengu.

Bila shaka, hata fursa kama hizo ziwe nyingi kiasi gani, hazitatambuliwa ikiwa uwezo wa kuwasilisha mafundisho ya Kibahá'í katika njia thabiti, ifaayo kwa hali hizo, haitapata umakinifu wa kutosha. Kiini cha kitengo hiki, hivyo, kimetolewa kwa uchunguzi wa uwezo huu, na washiriki wanasaidiwa kufikiria kuhusu asili yake kwa msaada wa mfano—mazungumzo ambamo kijana mmoja, Anna, anawasilisha Imani kwa rafiki yake Emilia. Wakufunzi watapaswa kuhakikisha kwamba washiriki watakapomaliza majadiliano haya ya msingi, watakuwa na angalau mawazo mawili yaliyoeleweka akilini mwao.

Kwanza, ni lazima kwamba washiriki siyo tu watambue tofauti kati ya dhana na taarifa, zilizoibuliwa katika Sehemu ya 4 hadi ya 6, lakini pia kwa nini tofauti hiyo ni muhimu sana. Hata hivyo, ni uelewa wa dhana na kweli za ndani ambazo huziwezesha roho kumkaribia Bahá'u'lláh, siyo uchukuaji tu wa taarifa. Kwa kiwango ambacho kitendo cha ufundishaji kinavyohusiana na uinuaji wa dhamiri na kulea uelewa, kinaweza kuonekana kama njia ya kusaidia kuwawezesha watu binafsi, kiakili na kiroho. Hapa, uwezo ambao washiriki wamekuwa wakiukuza tangu walipoingia katika mchakato wa taasisi wa kukutana na Neno la Mungu na kupata uelewa utaanza kufanya kazi, kadiri sasa wanavyowaza juu ya jinsi ya kuwaongoza wengine kuelekea kwenye fuko za ujuzi wa kweli.

Pili, washiriki sharti watambue kwamba mazungumzo kati ya Anna na rafiki yake, yaliyoelezwa katika Sehemu ya 7 hadi ya 21, yamekusudiwa kuwapa mfano wa kinachoweza kuwemo katika uwasilishaji wa kimantiki wa Imani; yasichukuliwe kama fomyula ya kutumilka bila busara. Kwa hakika, mazoezi yanayofuata kila sehemu ya uwasilishaji yameandaliwa kwa ajili ya kutilia mkazo mantiki yake yote na kutoa mawazo ya mwanzoni juu ya jinsi yanavyoweza kutumika katika usuli na raghba tofauti tofauti. Walakini, ikiwa washiriki wanahitajika kukuza uwezo wa kufanya hivi, watahitaji, kwanza kabisa, kujifunza uwasilishaji vizuri kama ulivyo na kuweza kuelezea mfuatano wa mawazo kwa maneno yao wenyewe.

Majadiliano ya jitihada za mtu binafsi za ufundishaji yanahitimishwa katika Sehemu ya 26, ambapo washiriki wanaombwa kuangalia hali za maisha yao na kubaini vipengele vya mpango binafsi wa ufundishaji. Katika Sehemu ya 27 wanahamasishwa kubuni kwenye misingi hiyo, mpango wa awali wa utendaji kwa kipindi fulani, ama majuma kadhaa au miezi michache. Inatumainiwa kamba zoezi hili litainua utambuzi wao juu ya umuhimu wa kujishughulisha kila mara katika ufundishaji kama ari binafsi katika maisha yao yote.

Sehemu ya 28, kisha, inageukia kwenye suala la utendaji wa pamoja, ambalo ndiyo shabaha ya sehemu iliyobaki ya kitengo hiki. Inatarajiwa kwamba, hadi kufikia hapa, washiriki tayari watakuwa wamehusika katika aina tofauti za kampeni shadidi. Zaidi, kila mmoja wao atakuwa sehemu ya kiini kikuacho cha wasaidizi amilifu wa Imani wakifanya kazi kwa uthabiti kuendeleza mchakato wa ujenzi wa jumuiya katika klasta ambamo wao wanaishi. Sehemu hizi za mwisho zitawasaidia kutafakari juu ya tajiriba zao kama washiriki katika utendaji wa pamoja kama huo. Ingawa mazoezi siyo magumu, hii haimaanishi kwamba sehemu hizo zipitiwe kwa haraka, na ni muhimu kwa mkufunzi kuhakikisha kwamba muda wa kutosha umetengwa kwa washiriki kuhusianisha kile wanachojifunza na tajiriba yao wenyewe. Kwa kufanya hivyo, wanapaswa waone namna gani katika utendaji wa pamoja, kila mtu anapaswa kuchangia kwa mazingira yanayoainishwa kwa kiwango kinachoendelea kukua cha umoja, katika sura zake mbalimbali. Wanapaswa wapate muono wa jinsi utendaji wa pamoja mashinani, pamoja na

jitihada binafsi, zinavyosaidia kuendeleza shughuli za kiulimwengu ambazo jumuiya ya Kibahá'í inajihusisha nazo.

Kufikia hapa, sehemu hizi zinaibua maswali kadhaa ambayo washiriki watayazingatia: Nini asili ya utendaji wa pamoja? Imaanisha kusema utendaji wa pamoja lazima uwe umeunganika? Ni zipi sifa za njia za ukuaji wa Imani ulimwenguni kote, na ni upi wajibu wa kampeni shadidi? Ni zipi baadhi ya sifa bainifu za watu ambao miongoni mwao wao wanafanya kazi, wawe wakazi wa kijiji au umati mpokevu unaoishi katika ujirani au waliosambaa kila mahali katika klasta? Ni imara kiasi gani nguvu zinazozalishwa kupitia utendaji wao wa pamoja kusukuma mjongeo wa umma kuelekea muono wa Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh? Je, uwezo unaojengwa kupitia mchakato wa kielimu unaoendelezwa na taasisi kwa watoto, vijana chipukizi, vijana na watu wazima una uhusiano wa karibu kiasi gani na ukuaji wa Imani? Je, mazingira yanayohitajika kwa ajili ya utendaji wa pamoja wenye ufanisi yanaendelea kujengwa? Je, mafundo ya undugu yanaendelea kuimarishwa? Je, umoja wa kusudi unaendelea kupatikana miongoni mwa washiriki katika utendaji wa pamoja? Je, unadhihirishwa katika shughuli zenye furaha na shadidi? Ni kwa kiwango gani mwelekeo wao wa ujifunzaji kuhusu ukuaji unavyoweza kutafsiriwa kwa vitendo, tafakari juu ya utendaji na ushauriano? Umuhimu wa swali hili la mwisho hauwezi kutiwa chumvi kwa kuwa hicho ndicho kiwango kinachotakiwa kuwa mtindo wa utendaji miongoni mwa kiini kinachoendelea kupanuka cha marafiki ambacho kitaweza kujenga viwango vya juu zaidi na zaidi vya umoja wa fikra, ambao ni wa lazima sana ikiwa wanataka kugundua kile kinachohitajika kuendelea kutoka hatua moja ya ukuaji hadi nyingine.



# Asili ya Kiroho ya Ufundishaji

## Kusudi

Kupata uelewa wa ufundishaji kama kitendo chenye maana maalum ya kiroho na kutambua kwamba ufundishaji wenye ufanisi huhusisha vyote viwili “kuwa” na “kutenda”—umakinifu kwa hali ya ndani ya mtu hali kadhalika shughuli za wakati wote

## SEHEMU YA 1

Hadi sasa umekuwa ukiendelea kwenye njia ya huduma kwa muda fulani—njia ambayo kwayo ukuaji wa kiroho na kiakili wa mtu binafsi hautenganishwi na uchangiaji wake kwa mabadilikaji ya jamii. Katika kila hatua ya njia hii mchanganyiko wa mafunzo na vitendo umeongeza uwezo wako wa kutumikia katika njia mbalimbali—katika kuimarisha tabia ya kiibada ya jumuiya yako, katika kuanzisha na kudumisha mazungumzo yainuayo kiroho pamoja na marafiki na familia katika ujirani au kijiji chako, katika kushiriki programu ya ziara za nyumbani zenye mpangilio, katika kutenda kama mwalimu wa darasa la watoto au kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi, au yote mawili. Katika shughul zote hizi, umepata furaha ya kushiriki na wale wa usuli tofauti na rika mbalimbali lulu za hekima kutoka bahari kuu ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh.

Bila shaka, kwa kuwa wewe umefanya kazi kuimarisha misingi ya kiroho ya jumuiya yako, umepata fursa za kusema moja kwa moja na kwa undani na wale wanaovutiwa kuhusu utu wa Bahá'u'lláh na Ufunuo Wake—kwa mfano, wakati wa kuwatembelea wazazi wenye watoto katika programu za kielimu za taasisi, labda, kama sehemu ya kampeni shadidi, au wakati wa kuzungumza na vijana wanaoingia katika mchakato wa taasisi kutokana na shauku yao ya kuhudumu. Hata katika mwingiliano wako wa kila siku na ndugu, marafiki, wanafunzi wenzako, wafanyakazi wenzako na watu unawafahamu kidogo wewe utakuwa umepata fursa kama hizo. Zaidi, katika matukio haya na mengineyo, hukuacha kuikaribisha roho pokevu kuukubali ukweli wa Ujumbe Wake na kujiunga na jumuiya ya wafuasi Wake. Vitengo vitatu vya kitabu hiki vitakusaidia kutafakari juu ya kitendo cha ufundisha, kitendo cha kuziongoza roho kwenye fuko za bahari kuu ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Bila shaka, kuna njia nyingi ambazo kwazo watu hufika kwenye fuko hizi. Tunapaswa tutambue, basi, kwamba mengi ya yale tutakayojifunza kuhusu nguvu za kiroho za ufundishaji zinazotumika kwa mapana kwa jitihada zetu zote, katika kila mazingira na hali, kujadili maadili bora ya Kibahá'í, kushiriki Imani na misimamo yetu, kuchunguza masuala ya kiroho pamoja na wengine, na hata kuwalea vijana—kwani jitihada hizi, vile vile, huhusisha kuzikutanisha roho na Neno la Mungu.

## SEHEMU YA 2

"Fundisheni Hoja ya Mungu, enyi watu wa Bahá," ni nasaha za Bahá'u'lláh, "kwani Mungu amemwamuru kila mmoja wajibu wa kutangaza Ujumbe Wake, na kukichukulia kama kitendo kistahilicho sifa kabisa kati ya vyote." Je, imaanisha nini kwa ufundishaji kuwa wajibu wa wale wote waliomtambua Bahá'u'lláh?

Neno "wajibu" linatumika katika kauli ya wanadamu kwa namna nyingi. Wakati mwingine, hubeba dhana ya seti ya sheria zilizowekwa juu yetu bila sababu dhahiri. Tunafikiria juu ya wajibu fulani kama kazi ambazo lazima tuzifanye hata kama ingependeza zaidi kama tungeepuka kuzifanya. Wajibu mwingine, unaohusiana na usitawi wetu na usitawi wa wale tunaowajali, tunafanya kwa furaha. Katika kushauriana na kikundi chako, orodhesha baadhi ya wajibu unaoleta furaha.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Kwa jumla, tunaelekea kutekeleza kwa bidii ule wajibu ambao huonekana ni wa muhimu kwetu. Mkulima, kwa mfano, hulijali kwa kuwajibika shamba lake kwa sababu anajua kila kazi ni ya lazima kwa lengo la mwisho la kuvuna mavuno mengi, ambayo juu yake riziki ya familia yake hutegemea. Sasa, ni yapi baadhi ya matunda tunayotumaini kuyapata kutokana na jitihada zetu za kufundisha Imani?

Wajibu ulioamriwa juu yetu na Mdhihirishaji wa Mungu unafaa kwa maslahi bora kabisa. Walakini thamani yao haimo tu katika mema unaoyatoa. Amri za Mungu siyo sheria tu zinazotuambia nini cha kufanya au kutofanya; kiasili amri hizo ni matamko kuhusu uhalisia wa uwepo wa wanadamu. Mfano mdogo utafafanua kipengele hiki.

Tunajua kwamba ili tuweze kuishi maisha yenye afya tunahitaji kula chakula kwa wastani mara kwa mara. Kula mara kwa mara, hata hivyo siyo kanuni ya kiholela ambayo mtu fulani ameiweka juu yetu; ni tamko kuhusu uhalisia wa uwepo wetu wa kimwili. Miili yetu imejengwa kwa namna ambayo kwamba huhitaji lishe kila baada ya saa kadhaa na sisi tunalazimika kuitikia hitaji hili; kulipuuzia hatimaye matokeo yake yanaweza kuwa kifo.

Vivyo hivyo, Mdhihirishaji wa Mungu anapotupa nasaha au amri, kwa mfano, ile inayotutaka tusali kila siku, Yeye halazimishi juu yetu kanuni fulani ya kiholela ya mwenendo. Bali, tunakuwa tunambiwa kitu fulani kuhusu uhalisia wa uwepo wetu—katika hali hii roho ya mwanadamu iliumbwa kwa namna ambayo kwamba, ili iweze kunawishwa lazima tugeuzie mioyo na akili zetu mara kwa mara kumuelekea Mungu na "kuzungumza" na Chanzo cha uwepo wetu. Hali kadhalika, wajibu wetu wa kufundisha Hoja Yake, mbali na manufaa dhahiri ambayo hutuletea sisi na jamii ya wanadamu, huweka wazi kweli fulani kuhusu asili ya roho ya mwanadamu na mahitaji yake. Katika sehemu kadhaa zinazofuata tutachunguza baadhi ya kweli hizi. Kabla ya kufanya hivi, walakini, utaona inasaidia kuandika sentensi moja kuhusu asili ya kila kimoja kati ya vifuatavyo. Mfano umetolewa kukusaidia.

1. Mshumaa: Asili ya mshumaa ni kutoa mwanga.

2. Nondo: 

3. Mwale: ______________________________________________

______________________________________________

4. Chemchemi: ______________________________________________

______________________________________________

5. Mawingu ya mvua: ______________________________________________

______________________________________________

6. Manukato: ______________________________________________

______________________________________________

Je, ungeafiki kwamba asili ya mwanadamu ni kutoa bila kukoma—kutoa mali zake, muda, nguvu na elimu?

## SEHEMU YA 3

Hebu tuanze tafakari zetu juu ya baadhi ya maana za wajibu wetu wa kufundisha kwa kusoma nukuu chache kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá katika sehemu hii na mbili zinazofuata. Katika tukio moja, Yeye huandika:

> **"Ewe mwale hai wa upendo wa mbinguni! Moyo wako umewashwa kwa upendo wa Mungu kiasi kwamba kutoka umbali wa maili elfu thelathini joto na mwangaza wake vinaweza kuhisiwa na kuonekana. Moto uliowashwa kwa mkono wa umauti hutoa mwangaza na joto kwa nafasi ndogo tu, ambapo ule mwale mtakatifu ambao Mkono wa Mungu umeuwasha, hata ukiwaka mashariki, utaiwasha magharibi na kutoa joto kote kaskazini na kusini; la, utainuka kutoka ulimwengu huu na kuwaka kwa mwale wenye joto kabisa katika milki za juu, ukiufurika kwa mwangaza Ufalme wa utukufu wa milele."**[1]

Kwa mujibu wa kifungu hiki, mioyo yetu inapaswa ____________ kwa upendo wa Mungu kiasi kwamba kutoka umbali wa ________________________________ na ____________ wake viweze _________________ na ___________ . 'Abdu'l-Bahá hutuambia kwamba ___________ unaowashwa kwa _________________ hutoa _____________ na ____________ kwa ___________ ndogo tu, ambapo ule ______________________ ambao _____________________ umeuwasha, hata ukiwaka __________ , uta ____________ , na kutoa __________ kote ___________ na ____________ . Utainuka kutoka ulimwengu huu na _____________ kwa ___________ katika milki za juu , ___________________________ wa mwangaza Ufalme wa _________________________ .

## SEHEMU YA 4

Kwa mmoja wa marafiki ambaye, akiwa na shauku ya muda mrefu kuufikia uwepo Wake, hatimaye alifanikiwa kukutana Naye kwa muda mfupi, 'Abdu'l-Bahá alimwambia maneno yafuatayo:

> **". . . Natumaini kwamba mkutano huu ulikuwa kama utambi wa taa uliokutana na moto na mara tu ulipoguswa uliwaka. Kwa matarajio nasubiri matokeo ya mkutano huu, ili Niweze kukuona umewashwa kama mshumaa na kuteketezwa kama nondo kwa moto wa upendo wa Mungu, uweze kuguswa kwa nguvu ya upendo na furaha, ukilia kama wingu, ukicheka kama konde la kijani, na kutetema kwa furaha kama mche mchanga usiolinganishwa unaopulizwa na pepo nyanana za Paradiso ya Abhá."**[2]

Kulingana na kifungu hiki, 'Abdu'l-Bahá hutumaini kutuona tukiwaka kama ________________ tukijiteketeza wenyewe kama _______________ kwa _____________ wa ______________ wa Mungu. Tukiguswa kwa ________________ ya _____________ na _______________ , Tunapaswa tulie kama _______________ , tukicheka kama ___________ _____________ , na kutetema kwa furaha kama ______________________________________ unaopulizwa na ____________________ za Paradiso ya Abhá.

## SEHEMU YA 5

Na katika Waraka mmoja ulioandikwa katika kujibu maswali kutoka kwa mmoja wa wafuasi wa mwanzoni wa Imani, 'Abdu'l-Bahá hueleza:

> **"Wajakazi wa Mungu sharti wainuke kufikia lile daraja kiasi kwamba, wao wenyewe na bila msaada, watazifahamu maana hizi za ndani, na kuweza kuelezea kikamilifu kila neno; daraja ambapo, kutokana na ukweli wa mioyo yao ya ndani kabisa, chemchemi ya hekima itabubujika, na kuchirizika kama vile kisima ambacho hububujisha kutoka chanzo chake chenyewe cha asili."**[3]

'Abdu'l-Bahá anatamani kwamba tuinuke kulifikia lile daraja ambapo, sisi wenyewe na bila msaada, ________________________ maana za ndani za mafundisho na kuweza ___________________ kikamilifu ____________________________________ . Hili ni daraja ambapo, kutokana na ____________ wa mioyo yetu ya ndani kabisa, ________________ ____________________ itabubujika, na __________________ kama vile _______________ ambacho ______________ kutoka _________________________________ .

## SEHEMU YA 6

Nukuu hizo tatu ambazo tumejifunza hivi punde hudokeza kwamba wajibu wetu wa kufundisha Hoja kwa kiasi kikubwa unahusiana na hali ya kuwa ambayo sharti tuifikie kwa kuwa i sambamba na vitendo tunavyopaswa kuvitekeleza. Kuna mengi tunayoweza kujifunza kuhusiana na hali hii ya kuwa kutoka sura zilizomo katika nukuu hizi. Zinazungumzia juu ya vitu ambavyo uwepo wake wenyewe huvitaka kujidhihirisha vyenyewe. Je, mwale unaweza kuchagua usitoe mwangaza na bado ukaitwa mwale? Je, chemchemi inaweza kuchagua isitiririshe na bado ikawa chemchemi? Vivyo hivyo pia, tumeumbwa kutoa na kuwa wakarimu. Kutoa, kugawana na wengine tulichonacho ni mahitaji ya uwepo wetu wa kiroho. Kati ya vyote tulivyonavyo kile chenye thamani kabisa ni zawadi ya imani—utambuzi wa Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku ya leo. Ni kawaida tu kwamba tungegawana na wengine ujuzi tunaoupata kutoka Ufunuo Wake na upendo na shangwe ambavyo kwavyo Ufunuo huu huzijaza roho zetu.

Tunaweza kukutana na vipingamizi vingi njiani mwetu, bila shaka, kadiri tunavyojitahidi kufundisha Hoja. Tunaweza kuwa wenye aibu, tunaweza kuwa wenye woga kutenda au kuzungumza, tunaweza kuona vigumu wakati mwingine kuelezea fikra kwa uwazi, lakini vyote hivi tunaweza kuvishinda pole pole kama tukielewa kwamba kwa kufundisha Hoja ya Mungu, tunajifunza kutoa kwa uhuru kile ambacho ni kipenzi kabisa kwetu. Maneno yafuatayo kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi yanaweza kutumika kama ukumbusho endelevu kwetu juu ya wajibu wetu wa kushiriki na wengine hekima takatifu iliyomo katika Ufunuo wa Bahá'u'lláh:

> **"Ulimwengu umo katika msukosuko mkubwa, na matatizo yake yanaonekana kuwa makali zaidi kila siku. Kwa hiyo, sharti tusikae bure, vinginevyo tunakuwa tumeshindwa kutimiza wajibu wetu mtakatifu. Bahá'u'lláh hakutupa Mafundisho Yake kuyahifadhi na kuyaficha kwa ajili ya furaha binafsi na starehe yetu. Yeye alitupa ili tuyafikishe kutoka mdomo hadi mdomo, hadi ulimwengu wote uyafahamu, na kufurahia baraka na athari zake ziinuazo."[4]**

## SEHEMU YA 7

Njia moja ya kubaini hali ya kuwa ambayo tunajitahidi kuifikia ndiyo kusema kwamba ni hali ya kuwaka. Tunapoyaelekeza mawazo na nguvu yetu juu ya ufundishaji, basi, tunapaswa tukumbuke kwamba moto wa upendo kwa Bahá'u'lláh mioyoni mwetu sharti uwake kwa wangavu zaidi na zaidi kila siku. Pengine ungependa kukariri kifungu kifuatacho kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá, ili daima kiweze kukukumbusha juu ya hitaji la kuulisha mwale wa upendo wa Mungu katika moyo wako:

> **"Ewe ambaye ni kama taa iliyowashwa kwa moto wa Upendo wa Mungu! Nimesoma barua yako ya hivi karibuni, ambayo imeonesha upendo wako wa dhati na kuwashwa kwako kwa moto wa upendo wa Bwana wako, Mwenye nguvu, Asifiwaye, na umeashiria athari ipenyezayo ya Roho wa Ukweli ndani ya viungo na neva zako, vena na ateri zako, mifupa, damu na nyama zako, kwa namna ambayo imechukua hatamu za uwezo kutoka mikononi mwako, na ikikusukuma ipendavyo, hukusababisha kuzungumzia kama ipendavyo na kukuvuta kama ipendavyo. Hii, kwa hakika hustahili kila moyo uliojazwa na roho ya upendo wa**

**Mungu. Punde utaona dalili zake za ajabu na kugundua ishara za Bwana wako Mwenye Nguvu."[5]**

## SEHEMU YA 8

Kifungu cha hapo juu huelezea hali ambamo hatuna budi kutumikia na kufundisha Hoja. Roho ya Ukweli itakuwa imejazwa mno ndani ya nafsi zetu kiasi kwamba itajitwalia kutoka kwetu hatamu za uwezo na kutusukuma kadiri ipendavyo. Jaribu kufikiria juu ya matokeo ya kuuzuia msukumo wa asili kama huu kwa kutafakari juu ya kila moja ya yafuatayo:

a. Chemchemi inayopokea maji lakini inakataa kutiririsha: ____________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b. Mtu ambaye daima hupokea fadhili za Mungu lakini hukataa kushiriki fadhili hizo na wengine: ________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

c. Mtu anayepata ujuzi lakini hashiriki na wengine: ___________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

d. Mtu anayepokea zawadi ya imani lakini hatumikii wala kufundisha Hoja: ______

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 9

Kadiri unavyotafakari juu ya asili ya uwakaji, sharti ukumbuke kwamba "kuwa" na "kutenda" ni sura mbili zinazokamilishana za kuishi kulingana na mafundisho ya Kibahá'í. Kwa ukaribu mno zimefumwa kiasi kwamba ni kazi bure kujaribu kuzitenganisha. Hatuwezi kungojea maisha yetu yote mpaka tufikie hali ya kuwaka kabisa kabla ya kuanza kutenda. Hata mwale mdogo kabisa hutoa joto na mwanga. Kuna mambo mengi ambayo tunapaswa tujitoe kuyafanya kwa wakati mmoja. Lazima tusali na kutafakari juu ya maana ya ndani kabisa ya Maandiko tujifunzayo kila siku. Lazima tujitahidi kutakasa mioyo yetu na kuakisi sifa Zake. Lazima tufungue macho yetu ya ndani, tuutazame uzuri Wake na kuvutiwa nao. Na lazima tuwe waamilifu katika uga wa huduma na kushiriki na wengine ujuzi tunaoupata kutoka Ufunuo wa

Bahá'u'lláh. Tukiwa na utambuzi wa uhusiano kati ya "kuwa" na "kutenda", zipi kati ya kauli zifuatazo ungeweza kuzitamka bila kusita? Ziwekee alama.

_____ Kuwatembelea watu katika nyumba zao na kuwahusisha katika mazungumzo ya maana huhitaji ujasiri mkubwa. Kwanza, lazima niishinde aibu yangu ya ndani, halafu nitakuwa tayari kutoa huduma hii.

_____ Ingawa nina hofu kuhusu kuanzisha mazungumzo na watu nisiowafahamu vyema, nimeweka imani yangu kwa Mungu, nikitambua kwamba ni kwa kupitia kuchukua hatua tu kwamba nitaweza kuushinda woga wangu.

_____ Mimi sina ujuzi wa kutosha kujadili Imani pamoja na wengine. Napaswa kujua zaidi kabla ya kuwatafuta watu wenye upokevu na kujaribu kushiriki nao mafundisho.

_____ Hekima tunayoweza kuipata kutoka Ufunuo wa Bahá'u'lláh haina mwisho, walakini hata umaizi mdogo tunaoupata kutoka kwake una thamani kubwa sana ambao lazima tushiriki na wengine kwa ukarimu.

_____ Najua mimi si mkamilifu kwa vyovyote na bado nina safari ndefu mbele yangu kabla ya kuakisi sifa nyingi za kiroho zinazoelezwa katika Maandiko. Hata hivyo, Bahá'u'lláh huahidi kwamba Yeye atawasaidia wale wote watakaoinuka kumtumikia Yeye, hivyo napaswa nifanye kila ninachoweza.

_____ Ingawa mimi nina mapungufu, nitainuka na kuitumikia Hoja. Kushiriki mafundisho ya Bahá'u'lláh na wengine husaidia kuongeza upendo wangu Kwake na hunisaidia kukuza uwezo na sifa za kiroho zihitajikazo.

_____ Ningependa kufundisha darasa la watoto, lakini kwanza napaswa nikuze sifa zote zinazohitajika za mwalimu mzuri. Wanafunzi watajifunzaje ikiwa sioneshi mfano unaofaa?

_____ Katika kitendo cha kufundisha darasa, upendo wangu kwa watoto hukua, na napata fursa nyingi za kuonesha kwa vitendo ukarimu, subira na wema wenye upendo.

_____ Vijana chipukizi katika kikundi ninachokiongoza kama mhuishaji wanapaswa waweze kuongea na mimi. Kama wanafikiria mimi ni mtakatifu sana, hawatajisikia huru kuelezea mawazo yao kwa uwazi. Jambo muhimu kabisa ni kwamba mimi nipo kwa ajili yao, kila juma bila kukosa.

_____ Katika kuhudumu kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi, lazima nirekebishe tabia zangu, kama vile ninavyojaribu kuwasaidia katika ukuaji wao wa kiroho na kiakili.

_____ Kwa jumla, katika uwanja wowote wa huduma, nikisema mambo sahihi, haileti tofauti yoyote kama roho yangu imewashwa au la.

_____ Kile ninachopaswa kufanya ni kuzingatia juu ya kumpenda Bahá'u'lláh. Kisha sitahitaji kusema hata neno moja. Moyo wangu utakuwa umewashwa mno

kiasi kwamba watu watajiuliza kwa nini nipo jinsi nilivyo. Wakigungudua kwamba ni kwa sababu mimi ni Mbahá'í, wataichunguza na kuikubali Imani wao wenyewe.

_____ Ufundishaji ni hali ya kuwa. Itakuja kwa njia ya kawaida. Kwa nini nifanye jitihada!

_____ Ufundishaji ni hali ya asili ya kuwa. Hakuna haja ya kuweka mipango yenye mpangilio wa kuzitafuta roho pokevu na kuzihusisha katika mazungumzo kuhusu utu wa Bahá'u'lláh na mafundisho Yake. We yaache tu mambo yatokee!

## SEHEMU YA 10

Tumekubaliana kwamba tunaweza na tunapaswa tufundishe Imani tangu tunapomtambua Bahá'u'lláh. Mfano ambao tumeutumia ni ule wa mwale ambao, haidhuru ni mdogo jinsi gani, bado unatoa mwangaza na joto. Wakati huo huo tunaelewa kwamba daima lazima tujitahidi kutajirisha maisha yetu ya kiroho, bila kuruhusu jitihada zetu za ufundishaji katika uga wa huduma kamwe kupungua, tukichochea moto wa upendo wa Mungu katika mioyo yetu na kuongeza ukali wake. Hebu tusite na tutafakari, basi, juu ya kile kinachoongeza uwakaji wetu.

Hapa chini kuna seti mbili za kauli. Kauli ya kushoto inajumuisha kauli ambazo, wakati zina ukweli fulani, zinasababisha mkanganyiko juu ya suala hili. Oanisha kila kauli iliyopo kwenye seti ya kushoto na ile ya kulia ambayo unaona inafaa zaidi.

______ Ujuzi ni utando. Ujuzi mwingi mno husababisha kiburi. Mtu sharti awe mwangalifu kutokazana mno kusoma Maandiko. Inatosha kuzingatia juu ya kumpenda Mungu na jamii ya wanadamu.

______ Uwakaji ni muhimu mno kiasi kwamba mtu anapaswa kujiondoa kwenye shughuli zote kwa muda fulani na kuishughulikia hali yake ya ndani peke yake.

______ Mtu anapowashwa kwa moto wa upendo wa Mungu, yeye huishi bila jitihada yoyote katika hali ya shangwe ya milele.

______ Tunashindwa kutii amri za Mungu kwa sababu hatumpendi Bahá'u'lláh vya kutosha.

a. Ufundishaji na huduma kwa Hoja ni vya lazima kwa ajili wa ukuaji wa kiroho na huongeza uwakaji wa mtu.

b. Hatimaye, uwakaji hutegemea juu ya neema ya Mungu. Walakini, hii haimaanishi kwamba jitihada haihitajiki. Kusali kila siku, kusihi kwenye Kizingiti Chake, kusoma Maandiko, na kumtumikia Yeye ipasavyo—hivi huongeza wepesi wa roho kuathiriwa ili kupokea neema na Fadhili za Mungu.

c. Ujuzi huchochea mwale wa upendo kwa Bahá'u'lláh katika moyo wa mtu. Kadiri mtu anavyomjua zaidi Yeye kupitia ujifunzaji wa Ufunuo Wake na kupitia huduma kwa Hoja Yake ndivyo mtu anavyompenda Yeye

______ Uwakaji hutokea kupitia neema ya Mungu tu. Kwa hiyo, hatuhitaji kufanya jitihada yoyote kuongeza ukali wake.

______ Mara moto wa upendo wa Mungu unapowashwa katika moyo wa mtu, hauwezi kuzimwa kamwe. Wenyewe, utabakia ukiwaka, ukiutakasa moyo wa nafsi na shauku.

kwa kina zaidi. Kama mtu hujiweka huru na ubinafsi, ambao husababisha kiburi na kuugeuza ujuzi kuwa utando, upataji wa ujuzi unaweza kuwa jambo muhimu katika kuongeza uwakaji wa mtu.

d. Kama vile sala na huduma kwa Hoja husaidia kuongeza mwale wa upendo wa Mungu katika moyo wa mtu, pepo za nafsi na tamaa za ubinafsi huuzima. Kwa hiyo, sharti mtu awe macho na kuulinda mwale wa upendo wa Mungu katika moyo wake.

e. Kadiri mtu anavyoshughulika kwa bidii katika njia ya Mungu, tando za nafsi huungulia mbali kwa moto wa upendo Wake, na mtu huhisi furaha ya kumkaribia Yeye.

f. Hata pale tunapompenda Bahá'u'lláh tunaweza kufanya makosa mengi, kwani sisi ni wadhaifu na wakati wote tunahitaji rehema na msamaha Wake. Kufanya jitihada kutii sheria Zake huongeza uwakaji.

Sasa andika aya fupi ukielezea kwa maneno yako mwenyewe jinsi uwakaji unavyoongezeka.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 11

Baada ya kufikiria kuhusu hali ya uwakaji, hali ambamo, tukiendelea kuwaka kwa moto wa upendo wa Mungu, tunaendelea kujitahidi kueneza mwangaza wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh, hebu tusome na kutafakari juu ya vifungu vifuatavyo:

**"Sema: Kunisaidia Mimi ni kufundisha Hoja Yangu. Hii ni mada ambayo kwayo Nyaraka zote zimesheheni. Hii ni amri isiyobadilika ya Mungu, ya milele wakati uliopita, ya milele wakati ujao."[6]**

**"Msifadhaike, Enyi watu wa ulimwengu, wakati nyota ya mchana ya uzuri Wangu ikitua, na mbingu ya hema Langu takatifu ikifichwa kutoka machoni penu. Inukeni kuendeleza Hoja Yangu na kutukuza Neno Langu miongoni mwa watu. Sisi tupo nanyi katika nyakati zote, na tutawaimarisha kupitia nguvu ya ukweli."[7]**

**"Kalamu ya Aliye Juu Kabisa imeamuru na kulazimisha juu ya kila mmoja wajibu wa kufundisha Hoja hii….Mungu, bila shaka, atamvuvia yeyote ajitengaye mwenyewe na vitu vyote isipokuwa Yeye, na atasababisha maji safi kabisa ya hekima na matamshi kumwagika na kutiririka kwa nguvu na kwa wingi kutoka moyoni mwake."[8]**

**"Mungu ameamuru kwa kila mmoja wajibu wa kufundisha Hoja Yake. Yeyote ainukaye kutimiza wajibu huu, sharti, kabla hajatangaza Ujumbe Wake, ajipambe mwenyewe kwa pambo la tabia ya unyoofu na istahiliyo sifa, ili maneno yake yaweze kuvutia mioyo ya wale ambao ni wapokevu kwa mwito wake."[9]**

**"Enyi wapendwa wa Mungu! Msijipumzishe wenyewe kwenye vitanda vyenu, la, jiamsheni wenyewe mara mumtambuapo Bwana wenu, Muumba, na kusikia juu ya mambo ambayo yamempata Yeye, na harakieni kumsaidia. Legezeni ndimi zenu, na tangazeni bila kukoma Hoja Yake. Hii itakuwa bora zaidi kwenu kuliko hazina zote za wakati uliopita na za ule ujao, kama mkiwa miongoni mwa wale ambao huutambua ukweli huu."[10]**

Pengine ungependa kukariri vifungu vya hapo juu vingi kadiri uwezavyo.

## SEHEMU YA 12

Tunapofikiria sura mbali mbali za wajibu wetu wa kufundisha, sharti tusisahau kwamba amri za Mungu ni ishara ya baraka Yake kwetu. Tusidhani hata kwa kitambo kidogo kwamba tunamfanyia Mungu fadhila kwa kufuata maagizo na amri Zake. Yeye angeweza, kwa neno moja, kujipatia ushindi kamili wa Hoja Yake. Kwamba Yeye ametupa fursa ya kueneza Imani Yake ni baraka isiyokadirika ambayo kila mmoja wetu amejaliwa. Bahá'u'lláh anasema:

> **"Kama tungependa, tungeijalia Hoja ushindi kupitia nguvu ya neno moja kutoka uwepo Wetu. Yeye kwa ukweli ni Mwenye Nguvu—Kabisa, Mshurutisha vyote. Kama ingekuwa dhamira ya Mungu, kutoka misitu ya nguvu za mbinguni angetokea simba mwenye nguvu zisizoshindika ambaye muungurumo wake ni mithili ya radi inayorindima milimani. Hata hivyo, kwa kuwa mjalia Wetu mwenye upendo huvipita vitu vyote, Sisi tumeamuru kwamba ushindi kamili sharti upatikane kupitia mazungumzo na matamshi, ili watumishi Wetu kote duniani hivyo waweze kuwa wapokeaji wa wema mtakatifu. Hii ni dalili moja tu ya fadhili za Mungu zilizojaliwa juu yao."[11]**

Katika lugha ya kuongea na kuandika, sitiari aghalabu hutumiwa kuwasilisha wazo, yaani, neno au kifungu cha maneno ambacho huleta fikra ya taswira fulani hutumika kuelezea jambo lenye utata. Katika kifungu hiki, Bahá'u'lláh hutumia sitiari ya simba. Simba huyo hutokea katika misitu ya nguvu za mbinguni, na muungurumo wake ni kama radi inayorindima milimani. Taswira hii hutupa kianga kidogo juu ya nguvu za Mungu, Muumba. Kwa kupitia kitendo kimoja, Yeye angeweza kuufanya Uwezo Wake ujulikane, na watu wote wa dunia wangesujudu kwa unyenyekevu mbele Yake. Ni kutokana na wema Wake wa upendo tu kwamba Yeye huturuhusu sisi, watumishi Wake, kuwa vyombo vya uenezaji wa Imani Yake. Kamilisha sentensi zifuatazo ukitumia maneno na vifungu vya maneno kutoka nukuu hiyo:

1. Kama Mungu angependa, Yeye angeweza ____________________________________

   ____________________________________________________________________ .

2. Kama ingekuwa dhamira ya Mungu, ange ___________________________________

   ____________________________________________________________________ .

3. Muungurumo wa simba huyu ungekuwa kama ______________________________

   _____________________________________________________ .

4. Walakini, kwa kuwa majaliwa Yake ya upendo huvipita vitu vyote, Mungu ameamuru kwamba _____________________________________________________________

   _________________________________ .

5. Yeye amefanya hii ili ___________________________________________________

   ______________________________________________________________ .

6. Hii ni _______________________ tu ____________________________________ .

## SEHEMU YA 13

Ni jambo la kawaida kwa watu kushikilia itikadi fulani na, wakati huo huo, kusema mambo ambayo kimsingi hupingana nazo. Kwa jumla, si rahisi kuwa mwenye msimamo. Sote tuna tabia akilini, zilizojengeka katika maisha yetu yote, zinazotufanya tuongee mambo bila kuyafikiria. Kama tungeyafikiria kidogo, ingekuwa dhahiri kwetu kwamba kwa kweli hatuyaamini hata baadhi ya matamshi tunayoyatoa. Hivyo, kadiri uelewa wetu unavyoongezeka kwa vyote viwili kupitia mafundisho na tajiriba, inafaa tusite mara kwa mara na kuchunguza uhalali wa kauli kadhaa. Amua ni zipi kati ya zifuatazo zinaendana na uelewa wako wa dhana ya ufundishaji kama wajibu. Ziwekee alama.

_____ Mimi nashiriki ipasavyo katika ushauriano wa jumuiya yangu juu ya kazi ya ufundishaji na kutoa mapendekezo kuhusu jinsi unavyopaswa kufanyika. Hivyo ndivyo ninavyotimiza wajibu wangu wa kufundisha.

_____ Kila zinapokuwepo jitihada zenye malengo ya ufundishaji katika jumuiya yangu, mimi nasema sala maalum kwa ajili ya hizo. Hivyo ndivyo ninavyotimiza wajibu wangu wa kufundisha.

_____ Kila fursa inapojitokeza, mimi hutoa umaizi fulani kutoka katika mafundisho ya Bahá'u'lláh. Hiyo inatosha kwangu kutimiza wajibu wangu wa kufundisha.

_____ Nimemfundisha Imani mtu mmoja mwaka huu. Nimetimiza wajibu wangu kwa mwaka huu.

_____ Kila mtu ninayemjua anatambua kwamba mimi ni Mbahá'í, na nimewaambia wale wenye shauku kuhusu Bahá'u'lláh na Ufunuo Wake. Nimemaliza njia zote zilizo wazi kwangu za kufundisha Imani.

_____ Mimi natimiza wajibu wangu wa kufundisha kwa kumwambia kila mmoja ninayekutana naye kuwa mimi ni Mbahá'í.

_____ Njia bora kabisa ninavyoweza kutimiza wajibu wangu wa kufundisha ni kuishi maisha ya mfano. Hakuna haja ya maneno.

_____ Mimi najaribu kutii amri na maagizo yote ya Bahá'u'lláh, ikiwemo ile ya kufundisha Hoja Yake, kwa kuwa ni kwa njia hii tu nitaweza kuishi maisha ya mfano.

_____ Najua Bahá'u'lláh ameamuru wajibu wa kufundisha Hoja Yake kwa kila mmoja wa wafuasi Wake. Lakini hakumaanisha hasa "kila mmoja". Yeye alikuwa anawaongelea wale wenye ujuzi mkubwa katika Imani na wana tajiriba ya kutosha.

_____ Kila ninapofikiria kuhusu uzuri wa mafundisho ya Bahá'u'lláh, huwa najawa na furaha mno kiasi kwamba sioni jinsi gani ningeacha kushiriki Ujumbe Wake na wengine.

_____ Ni katika kutimiza wajibu wangu wa kufundisha Hoja kwamba nitapokea uthibitisho Mtakatifu.

_____ Mimi natimiza wajibu wangu wa kufundisha Hoja kwa sababu ya upendo wangu kwa Bahá'u'lláh na upendo ambao Yeye ameuingiza ndani mwangu kwa ajili ya jamii nzima ya wanadamu.

_____ Tuna shughuli nyingi sana za kujenga jumuiya zinazoendelea katika ujirani wetu, na ni suala la muda tu kabla watu na familia zaidi na zaidi watakapoingia katika Imani. Hakuna haja ya sisi kutafuta fursa ya kuongea kuhusu Bahá'u'lláh na Ufunuo Wake na kusaidia kuzithibitisha roho katika Hoja Yake.

Kariri kifungu kifuatacho kutoka Waraka uliofunuliwa na 'Abdu'l-Bahá:

> **"Ee ewe mtafutaji wa Ufalme wa Mungu! Ikiwa unataka matamshi na kauli yako vipenyeze katika mioyo sugu, jiondoe mwenyewe kutokana na mwambatano wowote na ulimwengu huu na geuzia uso wako kwenye Ufalme wa Mungu. Washa moto wa upendo Wake ndani ya moyo wako kwa namna ambayo kwamba utakufanya uwe mwale unaowaka na mshumaa mwangavu wa uongozi Ndipo matamshi yako, kupitia uthibitisho wa Roho Mtakatifu, yatakapouchochea kila moyo."**[12]

## SEHEMU YA 14

Sasa kwa kuwa tumefikiria kuhusu maana ya ufundishaji kama wajibu wetu, hebu tutafakari juu ya utakatifu wa kitendo hiki, ambacho Mlinzi anatukumbusha katika nukuu tuliyoisoma katika Sehemu ya 6. Je, kwa namna gani ufundishaji ni mtakatifu? Bila shaka, ukweli tu kwamba ni maagizo ambayo hutoka kwa Mungu huufanya wajibu huu kuwa Mtakatifu. Lakini je, kuna sura zingine za utakatifu ambazo sharti tuzichunguze kuhusiana na ufundishaji? Katika mojawapo ya Nyaraka Zake Bahá'u'lláh husema

> **"Kile ambacho amekihifadhi kwa ajili Yake Mwenyewe ni miji ya mioyo ya watu; na kati ya hii wapendwa wa Yule Ambaye ndiye Ukweli Mkuu, katika Siku hii, ni kama funguo. Mungu akipenda awawezeshe wote kufungua, kupitia uwezo wa Jina Kuu Kabisa, milango ya miji hii."**[13]

Katika kifungu kingine Yeye husema:

> **"Vitu alivyojihifadhia Yeye Mwenyewe ni miji ya mioyo ya watu, ili aweze kuitakasa kutokana na najisi zote za kidunia, na kuiwezesha kukaribia Mahali patakatifu ambapo mikono ya makafiri kamwe haiwezi kupachafua. Ufungueni, Enyi watu, mji wa moyo wa wanadamu kwa ufunguo wa matamshi yenu. Hivyo ndivyo, kulingana na kipimo kilichoamriwa hapo awali, Tulivyoamuru juu yenu wajibu wenu."**[14]

Kujibu maswali yafuatayo kutakusaidia kuona jinsi vifungu hivi vinavyohusiana na utakatifu na kitendo cha ufundishaji:

1. Je, Mungu amejihifadhia nini kwa ajili Yake Mwenyewe? ______________________

2. Je, moyo wa mwanadamu ni mali ya nani? ____________________________________

3. Ni neno gani tunalitumia kuelezea "kile ambacho kinamilikiwa na Mungu"? _______

4. Ni kina nani ambao ni funguo za miji ya mioyo ya watu? _______________________

5. Je, Mungu anataka kuisafisha miji hii kutokana na nini? ________________________
________________________________________________________________________

6. Je, ni kwenye nini Yeye anataka mioyo hii ikaribie? ____________________________
________________________________________________________________________

7. Je, ni kwa ufunguo gani tutafungulia mji wa moyo wa mwanadamu? _____________

8. Je, ni wajibu gani umeamriwa juu yetu katika vifungu hivi? ____________________
________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 15

Bado kuna sura nyingine ya utakatifu tunayohitaji kuizingatia katika jitihada yetu ya kuchunguza uhusiano wake na ufundishaji. Katika mojawapo ya Nyaraka Zake Bahá'u'lláh hurejelea kwenye Ufunuo Wake kwa maneno haya:

> **"Sema: Hili ni Gombo la fumbo lililotiwa muhuri, ghala la Amri isiyobadilika ya Mungu, likiyabeba maneno ambayo Kidole cha Utakatifu kimeyachora, ambayo yalikuwa yameviringishwa ndani ya utaji wa siri isiyopenyezeka, na sasa limeshushwa kama dalili ya neema ya Yule Ambaye ni Mwenyezi, Mkale wa Siku. Ndani yake Sisi tumeamuru hatma za wakazi wote wa duniani na wenyeji wa mbinguni, na tumeandika ujuzi wa vitu vyote tangu mwanzo hadi mwisho."**[15]

Katika kifungu cha hapo juu, Bahá'u'lláh huelezea Ufunuo Wake kama Gombo lililopigwa kwa muhuri na la fumbo. Gombo ni karatasi iliyoviringishwa ambayo juu yake umeandikwa ujumbe muhimu. Gombo hili lililopigwa muhuri na la fumbo ni ghala ya Amri ya Mungu—yaani, hubeba kile ambacho Mungu ameamuru na kisichobadilika. Zoezi lifuatalo litakusaidia kupata umaizi wa maana ya kifungu hiki. Jazeni nafasi zilizo wazi kwa kutumia maneno kutoka nukuu hiyo na kisha someni sentensi hizo pamoja.

1. Ufunuo wa Bahá'u'lláh umeshushwa kwetu kama dalili ya __________ .

2. Kile ambacho kimeshushwa ni Gombo lililo ______________ na ______________ ambalo hapo kabla lilikuwa limeviringishwa ndani ya __________ wa ___________________________ .

3. Ni ghala ya ________________________________ ya Mungu.

4. Ndani yake Mungu ameamuru hatma za ____________________ wote wa duniani na mbinguni.

5. Ufunuo wa Bahá'u'lláh unajumuisha ndani mwake ___________________ wa vitu vyote tangu _____________ hadi ____________ .

## SEHEMU YA 16

Sasa fikiria kile tulichojifunza katika sehemu mbili zilizopita. Ufundishaji ni wajibu mtakatifu wa kila Mbahá'í, kwa kuwa umeamriwa juu yetu na Mungu. Aidha, tunapofundisha tunajihusisha na mambo mawili matakatifu sana. Moja ni moyo wa mwanadamu ambao kimsingi ni mali ya Mungu. Ufundishaji, kwa kweli, unaweza kuelezewa kama kile kitendo kitakatifu ambacho matokeo yake ni ufunguaji wa mji wa moyo wa mwanadamu Kwake. Jambo lingine takatifu ambalo kwalo ufundishaji huhusika ni Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Tunafundisha ili kuunganisha moyo na Ufunuo Wake, majaliwa Yake makuu kabisa kwa wanadamu.

Jaribu kukumbuka matukio maishani mwako ambapo ulihisi uwepo wa utakatifu. Kama umewahi kuwa ndani ya Makaburi Matakatifu ya Bahá'u'lláh na Báb, utaendelea kuwa na kumbukumbu thabiti ya jinsi ulivyohisi kukaribia, na kusujudu kwenye Vizingiti Vitakatifu vyao. Lakini hata kama bado hujapata baraka hiyo, lazima kumekuwa na nyakati nyingi maishani mwako ambapo ulifurahishwa mno katika sala, huku akili na moyo wako vikiwa vimegeuziwa kwa Mungu, na ulijihisi dhahiri kuwa umesimama mbele Yake. Ni zipi baadhi ya hisia ambazo zinaujaza moyo wako katika nyakati kama hizo? Ziwekee alama katika orodha ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| ______ upendo mkubwa | ______ unyenyekevu | ______ shangwe |
| ______ kicho | ______ kutaradadi | ______ kutostahili |
| ______ kutojali | ______ furaha kubwa | ______ uchaji |
| ______ kujinyenyekeza | ______ shukrani | ______ utulivu |

## SEHEMU YA 17

Zoezi hili la mwisho limetukumbusha mwelekeo wa heshima ambao mtu anapaswa kuwa nao anapokaribia kile ambacho ni kitakatifu, na juu ya hisia bora zinazoamka ndani ya moyo wa mtu anaposimama mbele ya uwepo utakatifu. Katika muktadha huu, swali muhimu sharti liulizwe: Jinsi gani utambuzi wako mwenyewe wa asili takatifu ya ufundishaji huvijaza nguvu vitendo vyako? Ili kukusaidia kujibu swali hili, inapendekezwa kwamba ufanye zoezi hilo hapo chini ambapo njia tatu tofauti za kukiangalia kitendo cha ufundishaji zinaelezwa, na unahamasishwa kufikiria juu ya matokeo ya kila mojawapo. Usihofu kwamba hali yenyewe iliyotolewa ni ya kubuni. Hata hivyo, zoezi hilo litakupa baadhi ya umaizi unaohitajika.

Kama sehemu ya kiini kinachoendelea kukua cha wasaidizi amilifu wa Imani katika ujirani au kijiji chako, wewe ni mjumnbe wa timu inayoshughulika na jitihada ya pamoja ya ufundishaji. Kwa pamoja wewe na wajumbe wengine mnatembelea kaya na kuongea na mtu mmoja mmoja na familia—ambapo baadhi yao kwa namna moja au nyingine tayari wameungana na shughuli zinazoendelea za ujenzi wa jumuiya—kweli za msigi zilizomo katika Ufunuo wa Bahá'u'lláh, zikiwasaidia kumtambua Yeye kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku ya leo. Hebu tufikirie mfano ambapo kwa kipindi fulani timu yako imewasaidia watu takriban thelathini kuikubali Hoja na kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í. Tunaweza kudhani kwamba kila mjumbe wa timu ametimiza wajibu wake wa kufundisha kwa uaminifu wa hali ya juu kabisa na kutokana tu na upendo kwa Bahá'u'lláh. Walakini, ingekuwaje kama mtazamo wa timu juu ya kile ilichokuwa ikikifanya usingekuwa thabiti katika hali zote?

Hebu tuseme kwamba, mwanzoni, mlijiona si kingine bali kama wauzaji. "Ufundishaji ni kama kuuza," mlijisemea wenyewe. "Imani ina mawazo bora kabisa yanayozunguka. Tutakuwa walimu wazuri kama tutaweza kuifungasha ipasavyo Imani na kuyauza mawazo haya mazuri kwa watu." Roho kumi zilijiunga na Imani kwa njia hii.

Sasa fikiria kwamba, baadaye kidogo, wewe na wajumbe wengine wa timu mkaona kile mlichokuwa mnakifanya kwa kiasi kikubwa huhusiana na kuwaingiza watu katika hoja endelevu ya kijamii. "Pamoja na hali mbaya ya ulimwengu," ninyi mlijisemea wenyewe, "kile kinachohitajika ni kuwaingiza watu wengi kadiri tuwezavyo, haraka iwezavyo—watu ambao watapata katika mafundisho ufumbuzi wa magonjwa ya wanadamu na ambao watafanya kazi kwa ajili ya uanzishaji wa umoja, kwa ajili ya uondoaji wa chukii, na kwa ajili ya hoja ya haki." Na kwa hiyo, ninyi kwa shauku kubwa mlianza kuwaalika wengine kujiunga nanyi katika kuendeleza mawazo muhimu kama vile amani, umoja, usawa wa kijinsia na ukomeshaji wa chuki. Watu kumi walijiunga na Imani kupitia jitihada hizi.

Baada ya muda kidogo, ninyi, bila shaka, bado mlikuwa na wasiwasi kuhusu hali ya ulimwengu na hitaji la kuongeza idadi ya watu ambao wangeweza kutumia Mafundisho ya Bahá'u'lláh kuubadilisha. Lakini timu yenu ilikuwa imeshakuza uelewa wa kina zaidi wa asili takatifu ya ufundishaji. Sasa kila mnapomuelezea mtu kweli za Imani, mlikuwa mnatambua vyema kwamba mnaongea na moyo wa mwanadamu, ambao ni mali ya Mungu. Kile mlichokuwa mnafanya, mngejikumbusha wenyewe, kilikuwa ni kutumia ufunguo wa matamshi yenu kufungua malango ya mji wa moyo huu na kuunganisha na Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Katika hali kama hizo watu wengine kumi walitangaza imani yao.

Baada ya kuwasaidia marafiki hawa thelathini kuikumbatia Hoja, timu yenu sasa inaanza jitihada yenye mpangilio kuimarisha ujuzi wao wa mafundisho, mkiwahamasisha wengi wao kadiri iwezekanavyo kuingia katika mchakato wa taasisi na kuwa wahusika wakuu katika jitihada za kujenga jumuiya katika kijiji au ujirani wenu. Je, mnadhani kutakuwa na tofauti yoyote miongoni mwa vikundi vitatu katika nguvu za ujihusishaji wao katika shughuli za Kibahá'í? Je, jitihada zenu zingekuwa zenye tija zaidi na kikundi chochote kimojawapo? Bila shaka, kutoka kimojawapo kati ya vikundi vitatu wangeibuka watu ambao walioandaliwa vyema na Bahá'u'lláh, wenye shauku mno ya kuchunguza zaidi Ufunuo Wake, kiasi kwamba kwa haraka wangeimarika na kujishughulisha na masuala ya jumuiya. Kile mnachoombwa, hata hivyo, ni kufikiria kuhusu kila kikundi kama kitu kimoja. Kwa wastani, mnadhani

kutakuwa na tofauti yoyote ya maana kati ya hivi vitatu? Jadilianeni suala hili katika kikundi chenu na andikeni maamuzi yenu katika nafasi iliyopo hapo chini.

Tukiendelea kufikiria kuhusu swali tulilouliza—yaani, ikiwa dhamiri yako kuhusu asili takatifu ya ufundishaji inaingiza katika vitendo vyako nguvu—hebu tuangalie mfano mwingine. Kama ilivyotajwa awali, shughuli nyingi za ujenzi wa jumuiya unazozifanya katika kijiji au ujirani wako zinahusu kuzikutanisha roho na Neno la Mungu na, kwa maana pana zaidi, inaweza kuonekana kama ufundishaji. Tuseme sasa wewe ni mjumbe wa timu inayojishughulisha kukaribisha kikundi baada ya kikundi, hususan vya vijana, kuingia katika mlolongo mkuu wa kozi za taasisi na kuanza kutembea kwenye njia ya huduma. Tuseme kwamba, pamoja na mitazamo inayofanana na hiyo hapo juu, unajihusisha katika mazungumzo na vikundi vitatu vya vijana, ambao wamekubali mwaliko wako. Tena, ukikifikiria kila kikundi kama kitu kimoja, je, unadhani kutakuwa na tofauti zozote kati yao, kwa mfano, kuhusiana na kiwango cha kujitoa wanachokionesha kwa ajili ya kufuatilia ukuaji wao wa kiroho na kiakili na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii?

## SEHEMU YA 18

Wakati malango ya mji wa moyo wa mwanadamu yanapofunguliwa na moyo unapounganika na Ufunuo wa Bahá'u'lláh, mchakato wa ndani wa mabadiliko huanza. Mabadiliko haya hayatokei papo hapo, bali hutokea taratibu kadiri tunavyojihusisha na usomaji na huduma kwa dhamira thabiti. Hata hivyo, hatupaswi kudharau jinsi kilivyo muhimu kitendo cha kumkubali Bahá'u'lláh kwa mchakato huu wa mabadiliko. Kulitambua Jua la Ukweli na kuruhusu mionzi yake kuingia na kuangaza moyo ni hatua moja muhimu sana ambayo mtu anaweza kuichukua katika maisha yake. Kwa kutafakari juu ya mabadiliko ambayo hufuatia utambuzi wa Bahá'u'lláh, tunaweza kuelewa vyema zaidi jinsi tunavyoweza kuwasaidia wengine kuchukua hatua hii muhimu. Je, unaweza kuandika sentensi moja au mbili kuhusu baadhi ya mabadiliko yanayotokea katika kila moja ya hali zifuatazo pale tunapomkubali Bahá'u'lláh na kuanza kutenda kufuatana na mafundisho Yake?

1. Mioyo yetu: ____________________________________________

2. Akili zetu: ____________________________________________

3. Fikra zetu: ____________________________________________

4. Tabia yetu: ____________________________________________

5. Uhusiano wetu na wanadamu wenzetu: ____________________________

6. Malengo yetu katika maisha: ___________________________________

7. Mtazamo wetu kuhusu ulimwengu: ________________________________

## SEHEMU YA 19

Tuliongelea kwa ufupi katika Kitabu cha 5 dhana ya nguvu pale tulipotafakari juu ya nguvu ya uwezeshaji wa kiroho. Mada hii inastahili tafakari zaidi katika muktadha wa mjadala wetu hapa. Katika ulimwengu wa kimwili, mabadiliko hutokea kupitia matumizi ya nguvu. Ili tuweze kujongea kutoka hatua moja hadi nyingine, ili mmea uweze kukua, ili taa iligeuze giza kuwa mwangaza, ili mito itiririke, na ili mawimbi yainuke na kupwa, nguvu inahitajika—nguvu zinatolewa na misuli ya mwanadamu, nguvu zinazozalishwa na jua, na umeme au na nguvu za mvutano. Ni muhimu kuuliza basi, ni nguvu za aina gani zinazoweza kuleta aina ya mabadiliko ambayo umeyaelezea katika sehemu iliyotangulia? Swali hili ni muhimu sana kwa uelewa wetu wa asili ya kiroho ya ufundishaji kiasi kwamba tutatenga sehemu inayobaki ya kitengo hiki kulipatia majawabu. Kwa kuanza, amua ni zipi kati ya nguvu zifuatazo zinaweza kuchangia kwenye mabadiliko ya kiroho kwa mtu binafsi na jamii:

______ Nguvu ya sala

______ Nguvu ya matendo safi na mema

______ Nguvu ya Neno la Mungu

______ Nguvu ya haki

______ Nguvu ya upanga

______ Nguvu ya umoja

______ Nguvu ya ukweli

______ Nguvu ya mfano

______ Nguvu ya maneno mema

______ Nguvu ya hoja zinazoshawishi

______ Nguvu ya fedha

______ Nguvu ya tabia nyoofu

______ Nguvu ya Agano

______ Nguvu ya utawala wa kisiasa

______ Nguvu ya ulalamikaji

______ Nguvu ya upendo

______ Nguvu ya ushawishi

______ Nguvu ya imani

______ Nguvu ya mawazo yanayojenga na yasiyo na ubinafsi

______ Nguvu ya bunduki

______ Nguvu ya ujuzi wa kweli

______ Nguvu ya mantiki

______ Nguvu ya utishaji

______ Nguvu ya huduma nyenyekevu kwa Hoja

## SEHEMU YA 20

Kutoka miongoni mwa nguvu zote ambazo huchangia kwenye mabadiliko ya kiroho moja hujitokeza kama ya kipekee, kama nguvu ya kimsingi nyuma ya zile nguvu zingine. Ni ipi hiyo?

Katika karne zote, kumekuwa na imani kwamba kuna kitu kiitwacho "kioevu" ambacho mara kinapotiwa katika shaba, au kwa kweli katika elementi nyingine yoyote ile, kingeigeuza kuwa dhahabu. Mchakato huu, ambao umetafutwa na wengi lakini kamwe haukupatikana, huitwa "ubadilishaji wa elementi". Katika mojawapo ya Nyaraka Zake, Bahá'u'lláh hutumia taswira hii kuonesha ukweli wa wa ndani kabisa kiroho:

> **"Nguvu ya imani ya watu kwa Mungu inaendelea kufa katika kila nchi; hakuna kingine isipokuwa dawa Yake ya uzima iwezayo kuirudisha. Uharibifu wa kutomcha Mungu unakula viungo muhimu vya jamii ya wanadamu; Kitu gani kingine isipokuwa kile kioevu cha Ufunuo Wake wenye nguvu kinachoweza kuisafisha na kuihuisha? Je, hili limo ndani ya uwezo wa mwanadamu, Ewe Hakim, kuathari katika elementi za msingi za chembe zozote ndogo kabisa na zisizogawanyika za maada mabadiliko kamili kabisa ya kukibadili kuwa dhahabu safi kabisa? Ingawa ni jambo la kutatanisha na gumu kama liwezavyo kuonekana, kazi kubwa zaidi iliyobaki ya kuzigeuza nguvu za kishetani kuwa nguvu za mbinguni ni ile ambayo tumewezeshwa kuitimiza. Nguvu yenye uwezo wa kuleta mabadiliko kama hayo hupita nguvu ya Kioevu chenyewe. Neno la Mungu, pekee, linaweza kudai upekee wa kujaliwa nguvu inayohitajika kuleta mabadiliko makubwa mno kama hayo na yenye kufika mbali."[16]**

Sasa kwa kuwa umekwisha soma kifungu hiki, je, ni nguvu ipi ungesema hujitokeza kama ya kipekee, kama nguvu ya kimsingi nyuma ya nguvu zingine za aina yoyote? _______

____________________________________________________________________________

Je, nguvu hii ina uwezo wa kutimiza nini? ________________________________________

____________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 21

Katika kifungu cha hapo juu, tunaambiwa kwamba, ingawa ubadilishaji wa elementi kuwa dhahabu safi unawezakuwa mgumu, kubadilisha nguvu ya kishetani kuwa nguvu ya mbinguni kwa hakika ni vigumu zaidi. Walakini, Neno la Mungu, na Neno la Mungu pekee, laweza kuleta mabadiliko ya kimsingi kama hayo. Lakini je, "Neno la Mungu" ni nini, lazima tuulize, lenye uwezo wa kuleta mafanikio makubwa mno kama hayo? Bahá'u'lláh husema:

> **"Ujue, aidha, kwamba Neno la Mungu—utukuzwe utukufu Wake—ni la juu zaidi na bora kabisa kwa kile ambacho fahamu zinaweza kukitambua, kwa kuwa limetakasika kutoka mali au kitu chochote. Linapita kabisa mipaka ya elementi zinazojulikana na limetukuka juu ya vitu vyote vya kiasili na vinavyotambulika. Lilidhihirika bila silabi au sauti yoyote na si kingine bali ni Amri ya Mungu ambayo hupenyeza viumbe vyote. Halijazuiliwa kamwe kutoka ulimwengu wa kuwa. Ni neema ya Mungu ipenyezayo vyote, ambayo kutoka humo neema zote**

**huanzia. Ni kitu ambacho kimewekwa mbali kabisa juu ya vyote vile ambavyo vimekuwepo na vitakavyokuwepo."[17]**

1. Neno la Mungu ni ____________ na ________________ kabisa kwa kile ambacho fahamu zinaweza kukitambua.

2. Neno la Mungu lime ____________________ kutoka __________________ au _____________________ chochote.

3. Neno la Mungu ___________________ mipaka ya __________________________ .

4. Neno la Mungu lime __________________ juu ya __________________ vyote vya kiasili na ___________________ .

5. Neno la Mungu lilidhihirika bila ________________ yoyote au ____________ .

6. Neno la Mungu ni _________________ ya Mungu.

7. Neno la Mungu, Amri Yake, hupenyeza _____________________________ .

8. Neno la Mungu, Amri Yake,________________ kamwe kutoka _________________ .

9. Neno la Mungu ni ________________ Yake ipenyezayo vyote, ambayo kutoka humo __________________ huanzia.

10. Neno la Mungu ni __________________ juu ya vyote vile __________________ na vyote vile ______________________ .

## SEHEMU YA 22

Taswira nyingine ambayo hutupa kianga cha nguvu ya Neno la Mungu ni ile ya uunganishaji wa silabi KU na WA. Katika Maandiko tunaambiwa kwamba Mungu aliunganisha silabi KU na WA pamoja, na akatoa amri "KUWA". Hivyo ndivyo muumbo wote ulivyotekea. Katika sala iliyofunuliwa na Bahá'u'lláh Yeye anamrejelea Mungu, Muumba wetu kama:

> **"Yule ambaye kupitia uashiriaji wa kidole Chake majina yote na ufalme wao vililetwa kwenye uhai, na sifa zote na milki yao viliumbwa, na Ambaye, bado kupitia uashiriaji mwingine wa kidole hicho hicho, ameunganisha silabi KU na WA na kuzifuma pamoja, zikidhihirisha kwavyo kile ambacho fikra za juu kabisa za wateule Wako ambao hufurahia ukaribu Wako zimeshindwa kukielewa, na kile ambacho hekima ya ndani kabisa ya wale miongoni mwa wapendwa Wako ambao wamejitoa kabisa Kwako wameshindwa kukielewa."[18]**

Katika Waraka mwingine, Bahá'u'lláh hutangaza:

> **"Kila kitu lazima kiwe na mwanzo na kila jengo mjenzi. Kwa kweli, Neno la Mungu ni Hoja iliyotangulia ulimwengu wa nasibu—ulimwengu ambao umepambwa kwa uzuri wa Mkale wa Siku, bado linaendelea kufanywa upya na kuhuishwa wakati wote. Ametukuka bila kipimo Mungu wa Hekima Ambaye ameinua muundo huu bora."[19]**

## SEHEMU YA 23

Sasa tumejifunza kwamba Neno la Mungu ni Amri Yake ipenyezayo vyote na neema na halikufanyizwa kwa silabi na sauti. Hata hivyo kuna maneno ambayo tunaweza kuyasoma na kuyasikia ambayo yana nguvu ya Neno la Mungu, yaani, yale ambayo hutamkwa na Mdhihirishaji. Haya yana nguvu ya kuumba, kuhuisha na kubadilisha, na kwa mantiki hii, yanarejelewa kama "Neno la Uumbaji". Bahá'u'lláh hutuambia:

> **"Kila neno litokalo kwenye kinywa cha Mungu limejaliwa ile nguvu kiasi kwamba linaweza kuingiza uhai ndani ya kila kiunzi cha mwanadamu, kama mkiwa miongoni mwa wale ambao huufahamu ukweli huu."[20]**

> **"Ewe rafiki yangu! Neno la Mungu ni mfalme wa maneno na athari yake ipenyezayo haipimiki. Daima limetawala na litaendelea kutawala milki ya kuwa. Yule Aliye Mkuu husema: Neno ndiyo ufunguo mkuu kwa ulimwengu mzima, kwa kuwa kupitia nguvu yake milango ya mioyo ya watu, ambayo kwa uhalisi ni milango ya mbinguni, hufunguliwa."[21]**

> **"Neno la Mungu limewasha moto katika moyo wa ulimwengu; itasikitishaje ikiwa mtashindwa kuwashwa kwa mwale wake!"[22]**

Hapo chini kuna maswali kadhaa ambayo hurejelea kwenye nukuu za sehemu hii, na sehemu zilizotangulia. Ingawa baadhi ya maswali yanakuhitaji tu kujibu "ndiyo" au "hapana" ukamiishaji wa zoezi zima utasaidia kuweka wazi uelewa wako juu ya nguvu ya Neno la Mungu.

1. Je, Neno la Mungu limefanyizwa kwa silabi na sauti? ____________________________

2. Je, Neno la Mungu limefanyizwa kwa kitu chochote kinachojulikana? _____________

3. Je, Neno la Mungu linaweza kutambuliwa na fahamu zetu? ______________________

4. Je, Neno la Mungu ni nini?

    a. Si kingine zaidi ya ________________________________________________

    b. Ni ________________________________________________ ya Mungu.

5. Je, inamaanisha nini kwamba Amri ya Mungu imepenyeza viumbe vyote? _________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

6. Je, kungekuwepo kitu chochote ulimwenguni kama kisingeletwa kwenye uhai kwa Amri ya Mungu? _______________________________________________________

7. Je, inamaanisha nini kwamba neema ya Mungu hupenyeza vyote? _______________

_______________________________________________________________________

8. Kingetokea nini kama neema ya Mungu ingezuiliwa kutoka ulimwengu wa kuwa? __

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

9. Kwa kuwa Neno la Mungu haliwezi kuhisiwa na viungo na fahamu zetu, je, jinsi gani tunaweza kulitambua? _____________________________________________

10. Nani ni "kinywa cha Mungu" ambaye kupitia kwake Mungu huzungumza? ________

11. Je, kila neno litamkwalo na Mdhihirishaji wa Mungu limejaliwa kitu gani? ________

_______________________________________________________________________

12. Ni zipi baadhi ya sifa bainifu za "uhai mpya" zilizoingizwa ndani ya kila mwanadamu kupitia Neno la Mungu? ____________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

13. Je, athari ya Neno la Mungu ni kubwa kiasi gani? ____________________________

14. Je, ni upi ufunguo mkuu kwa ulimwengu mzima? ______________________________

15. Je, Neno la Mungu hufanya nini kwa mioyo ya watu? __________________________

16. Je, ni kitu gani kilichouwasha moyo wa ulimwengu? ___________________________

17. Je, tunapaswa kuwashwa kwa mwale upi? ____________________________________

Sasa kariri nukuu ifuatayo:

> **"Hii ndiyo siku ambayo inatupasa tuseme. Imewapasa watu wa Bahá kujitahidi, kwa subira na ustahimilivu wa hali ya juu kabisa, kuwaongoza watu wa ulimwengu hadi kwenye Upeo Mkuu Kabisa. Kila mmoja huiita kwa sauti roho.**

**Roho za mbinguni lazima zihuishwe, kwa pumzi ya Neno la Mungu, miili iliyokufa kwa roho mpya."[23]**

## SEHEMU YA 24

Hebu tuchunguze uhusiano kati ya baadhi ya mawazo ambayo tumekwisha yajadili katika sehemu zilizotangulia. Bahá'u'lláh hutusihi kufungua mji wa moyo wa mwanadamu kwa ufunguo wa matamshi yetu. Mara malango ya mji huu yakifunguliwa na moyo kuunganishwa na Ufunuo Wake, mabadiliko ya ajabu huanza kutokea. Miongoni mwa nguvu zinazoyasukuma mabadiliko haya, nguvu ya Neno la Mungu inayowasilishwa kupitia maneno ya Mdhihirishaji haiepukiki kabisa. Je, hii humaanisha hivyo kwamba ni bora zaidi kwetu kutotumia maneno yetu wenyewe wakati wa ufundishaji na tuwatongolee tu wengine vifungu kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh?

Katika kujibu swali hili jikumbushe mwenyewe juu ya mwenendo wa mashabiki fulani wa kidini ambao hubeba nakala ya Kitabu Kitakatifu, ambacho kutoka humo huwahutubia watu. Kwa hakika, hii siyo njia ambayo sisi tungependa kuifuata. Katika usomaji wako wa Kitabu cha 2 ulishauriwa kutafuta mizania kati ya kunukuu moja kwa moja kutoka Maandiko au kutumia maneno yako mwenyewe kuelezea mafundisho na kanuni za Imani. Pasi na shaka, tangu wakati huo, umekuza uwezo huu kupitia vitendo vya huduma ulivyovifanya katika ujirani au kijiji chako. Someni nasaha zifuatazo za Bahá'u'lláh na tafakarini kwa mara nyingine tena juu ya jinsi, katika jitihada zetu za ufundishaji, tunavyopaswa tujifunze kutumia nguvu ya Neno la Mungu:

> **"Roho zilizotakaswa sharti zitafakari na kutaamuli mioyoni mwao kuhusiana na njia za ufundishaji. Kutoka maandiko ya ajabu, Maandiko ya mbinguni sharti wakariri vifungu vya maneno na vifungu vinavyohusu mifano mbalimbali, ili wakati wa mazungumzo yao waweze kutongoa aya takatifu kila fursa inapohitajika, kwa kuwa aya hizi takatifu ni kioevu chenye nguvu mno, talasimu kubwa na yenye nguvu mno. Athari zake zina nguvu mno kiasi kwamba msikilizaji hatakuwa na sababu ya kusita."[24]**

1. Bahá'u'lláh hutuambia __________________ na _____________________ mioyoni mwetu kuhusiana na _________________ za _____________________ .

2. Sharti _______________ vifungu vya maneno na ________________ vinavyohusu mifano mbalimbali kutoka __________________________ Maandiko matakatifu.

3. Tunapaswa tukariri vifungu kutoka Maandiko Matakatifu ili wakati wa ____________ yetu tuweze ______________ aya takatifu wakati kila _________________________ .

4. Tunapaswa tutongoe aya takatifu katika mazungumzo yetu kwa kuwa ____________ _______________ hizi ________________ ni _______________ chenye nguvu mno .

5. ________________ za aya hizi takatifu ____________________ kiasi kwamba ________________ hatakuwa na sababu ya ______________________ .

## SEHEMU YA 25

Bahá'u'lláh hutuambia tukariri vifungu vya maneno na vifungu kutoka Maandiko Matakatifu ili tuweze kuvitumia katika mazungumzo yetu kila fursa inapotokea. Kwa uwazi hii hurejelea kwanza kabisa kwenye Maandiko Yake mwenyewe, kwa kuwa Yeye ni Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku ya leo na, kama ya wale Wadhihirishaji wote waliotangulia kama vile Báb, matamshi Yake hufanya Neno la Uumbaji.

Lakini vipi kuhusu maneno ya 'Abdu'l-Bahá? Pamoja na washiriki wengine wa kikundi chenu, jadilianeni juu ya nguvu ambayo maneno Yake hutoa kwa msikilizaji. Fikiria athari ya Maneno Yake kwenye moyo wako mwenyewe, kwa mfano, ulipokuwa unayasoma katika vitabu vilivyotangulia vya mlolongo huu. Pengine utakumbuka, vile vile, umaizi ulioupata kutoka kitengo cha pili cha Kitabu cha 2 ambavyo kutokana na msingi wa mazungumzo na Nyaraka Zake vilikusaidia kukuza uwezo uhitajikao kujihusisha katika mazungumzo ya maana na yainuayo. Ingawa Maandiko Yake yanaweza yasichukuliwe kama aya takatifu zilizofunuliwa, yana daraja lake yenyewe. Kutoka wapi maneno Yake hupata nguvu yake? Je, haifai kwetu kunukuu vifungu kutoka Maandiko Yake katika mazungumzo yetu, kama tufanyavyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh?

Sasa fikiria maswali hayo hayo kuhusiana na maandiko ya Mlizi, mkikumbuka, kwa mfano, jinsi vifungu zilizonukuliwa katika vitabu vya awali vimeangazia fikra zenu juu ya mada mbalimbali. Baada ya kufanya hivyo, fanyeni majadiliano kama hayo hayo kuhusiana na miongozi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

## SEHEMU YA 26

Tumeona jinsi ilivyo muhimu kukariri vifungu kutoka maandiko katika jitihada zetu za kufundisha Hoja. Lakini tunajua pia kwamba katika kuelezea mafundisho ya Bahá'u'lláh, tunahitaji kutumia maneno yetu wenyewe vile vile, kwa kuwa hatuwezi kunukuu tu kwa watu kifungu hadi kifungu kutoka kwenye maandiko ya Imani. Nukuu sharti zifumwe katika mazungumzo na majadiliano yetu kwa namna ya kawaida. Swali kwa hiyo ni: Jinsi gani tunaweza kuhakikisha kwamba maneno yetu huizigusa mioyo ya wale ambao tunazungumza nao na kuwasaidia kumkaribia Bahá'u'lláh na kufikia fuko za Bahari kuu ya Ufunuo Wake?

Ni dhahiri jibu ni kwamba, ingawa tunatumia maneno yetu wenyewe, kile tunachosema sharti kiwiane kabisa na mafundisho. Siyo nadharia zetu wenyewe ambazo tutakuwa tunazitoa, bali Ujumbe wa Bahá'u'lláh katika umbo halisi kabisa kadiri iwezekanavyo. Hii, bila shaka, hutuhitaji sisi kujizamisha wenyewe katika maandiko na daima kuimarisha ujuzi na uelewa wetu wa Imani. Kuhusiana na hili, Mlinzi hutushauri:

> **"Kwa hakika njia bora kabisa ya ufundishaji ni kuthibitisha hoja zetu kwa kurejelea wakati wote kwenye maneno halisi ya Bahá'u'lláh na Bwana. Hii itaiokoa Hoja kutofafanuliwa vibaya na watu binafsi. Ni kile ambacho Miangaza hii mitakatifu husema ndicho ukweli na kwa hiyo sharti Wao ndiyo wanapaswa kuwa mamlaka ya matamshi yetu.**
>
> **"Hii, walakini, hainamaanishi kwamba uhuru wetu wa kujieleza umedhibitiwa. Daima tunaweza kupata njia mpya za kuufikia ukweli huo au kuelezea jinsi**

**unavyoathiri maisha na hali yetu. Kadiri ujifunzaji wetu ulivyo wa kina zaidi ndivyo zaidi tunavyoweza kuelewa maana ya Mafundisho."[25]**

**"Kukujiimarisha katika Hoja humaanisha kusoma maandiko ya Bahá'u'lláh na ya Bwana kwa ukamilifu kabisa hata kuweza kuyatoa kwa wengine katika umbo lake halisi. Kuna wengi ambao wana mawazo ya kubabiababia kuhusu kile ambacho Hoja humaanisha. Wao, kwa hiyo, huiwasilisha pamoja na aina zote za mawazo ambayo ni yao wenyewe. Wakati Hoja bado ingali katika siku zake za mwanzoni lazima tuwe waangalifu kabisa ili tusiangukie kwenye kosa hili na kuidhuru Hoja tuipendayo mno.**

**"Hakuna kikomo kwenye ujifunzaji wa Hoja. Kadiri tusomavyo maandiko ndivyo tuwezavyo kupata ndani mwake mambo yenye ukweli zaidi na ndivyo zaidi tutakavyoona kwamba mawazo yetu ya awali yalikuwa potofu."[26]**

Sasa soma kauli zifuatazo na amua kama ni za kweli. Usiridhike tu na kuwekea alama majibu. Mfululizo wa mawazo ungekusaidia kufikiri juu ya umuhimu wa kujifunza maandiko kwa utaratibu.

_____ Kujifunza maandiko ni kwa walioelimika sana tu. Wengine wanahitaji tu kuelezewa kiini cha mambo katika maneno rahisi.

_____ Sote sharti tujifunze maandiko. Hata watu wasiozoea kusoma wanaweza kujifunza, kwa msaada wa wengine, kifungu kimoja kwa wakati.

_____ Kadiri tujifunzavyo maandiko na kupata ufahamu wa Imani wa kina zaidi na zaidi, tunaweza kuelezea kwa uaminifu zaidi kweli zilizohifadhiwa katika Ufunuo, na kwahiyo maneno yetu yatakuwa na athari kubwa zaidi kwa msikilizaji.

_____ Kwa kujaribu kuwa waaminifu kwa maandiko wakati tufundishapo Hoja, tunajiwekea mipaka juu ya uhuru wetu wenyewe wa kufikiri na kujieleza.

_____ Kama sisi ni waaminifu kwa maandiko wakati tufundishapo Hoja, fikra zetu zitainuliwa kufikia kiwango cha juu zaidi; hatutatawaliwa kabisa wa mawazo ya wengine na kuzuiliwa na fikra finyu.

_____ Kama sisi ni waaminifu kwa maandiko wakati tufundishapo Hoja, tutavuviwa, na umaizi na majibu vitakuja akilini mwetu ambavyo tusingeweza kamwe kufikiria kabla.

_____ Pindi unaposoma kitabu au waraka uliofunuliwa na mmojawapo wa Wakuu wa Imani, hakuna sababu ya kurudia kusoma tena.

_____ Haidhuru ni mara ngapi mtu anakisoma kifungu chochote kutoka kwenye maandiko, mtu hupata maana mpya na umaizi mpya ndani yake.

_____ Mtu hajifunzi maandiko kulimbikiza tu wingi wa habari juu ya Imani. Jambo la msingi ni kiasi gani mtu hutafakari juu ya Maandiko na kujitahidi kuelewa maana iliyohifadhiwa humo.

_____ Tunapofundisha Imani, tusifiche kweli tunazozibuga kutoka maandiko kwa kuzichanganya na kila aina za mawazo ya kubabia babia kwa ajili ya kujipatia umaarufu wa muda.

_____ Tunapoingiza umaizi wa mafundisho katika mazungumzo yasiyo rasmi au tukijifunza mada yenye maana ya kiroho tunapomtembelea rafiki au jjirani, si tu wale tunaozungumza nao ambao hunufaika na lulu za hekima zinazopatikana katika bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Sisi pia tunaimarisha uelewa wetu wa kweli za ndani zaidi zilizomo katika maandiko Yake.

_____ Kadiri tunavyoendelea kusoma kozi za taasisi na kutekeleza vitendo vya huduma zinavozihamasishwa, sisi tunaendelea kuimarisha ujuzi wetu wa Imani huku tukikuza uwezo wetu kuhudumia jumuiya.

## SEHEMU YA 27

Kupatanisha maneno yetu na Mafundisho ya Bahá'u'lláh kama yalivyofafanuliwa na 'Abdu'l-Bahá na Mlinzi, pamoja na miongozo tunapokea kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, huyajalia nguvu kubwa. Nguvu hii huzidishwa kama tukijifunza hasa vifungu kutoka maandiko na kuyafuma katika mazungumzo yetu kwa njia ya kawaida na kwa hekima. Lakini maneno yetu lazima yakidhi vigezo vingine kama yanataka kugusa mioyo ya wale tunaozungumza nao. Hususan, lazima yawe na nguvu ya upendo, upendo ambao huhisiwa kwa dhati, siyo upendo wa mwonekano tu. Katika mojawapo ya mazungumzo Yake, 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Kama nakupenda, sina haja ya kuzungumzia wakati wote juu ya upendo wangu—utajua bila maneno yoyote. Kwa upande mwingine kama sikupendi, hilo pia utajua—na usingeniamini, hata kama ningekuambia kwa maneno elfu moja, kwamba nakupenda."**[27]

Upendo siyo tu kanuni fulani ya kinadharia ambayo mtu huzungumzia. Ni halisi, na wakati mtu ampendapo mwingine kwa kweli, fundo hujengeka kati ya mioyo ambalo kupitia hilo hisia bora na mawazo ya hali ya juu sana yaweza kutiririka. Roho moja yaweza kuiinua nyingine, na furaha huzijaza zote mbili.

Mírzá 'Abu'l-Fadl, Mbahá'í aliyejitoa ambaye aliaminiwa sana na 'Abdu'l-Bahá, wakati fulani alichanganua dhana ya upendo kwa wanadamu katika mazungumzo aliyoyatoa kwa kikundi cha marafiki. Alieleza jinsi ilivyo rahisi kwa yeyote kati yetu kukaa kwa raha mustarehe katika nyumba yenye bustani nzuri na kusema "Nawapenda wanadamu." Lakini, kulingana na Mírzá 'Abu'l-Fadl, upendo huwa halisi tu wakati unapojaribiwa. Ni pale tu tunapokuwa tumepigana vita vya upendo na mara kwa mara kujeruhiwa kwa ajili ya upendo, ndipo tunaweza kuitamka sentensi hiyo "Napenda" kwa mamlaka na uhakika. Hivyo, yeye aliendelea, mtu anayedai kwamba ana upendo moyoni mwake lazima ajijaribu yeye mwenyewe na kuona kama anakidhi vigezo vyote vya upendo wa kweli.

Ni vipi baadhi ya vigezo hivi? Ni dhahiri vinajumuisha uadilifu na ukweli, ukarimu na uhuru, msamaha na uaminifu. Unaweza kuona kwa urahisi kwamba vyote hivi ni vya lazima kwa upendo kuwepo. Kwani upendo usio na uadilifu ni nini zaidi ya unafiki? Ni yapi matokeo

ya upendo unapotawaliwa na wivu na masharti, na siyo na moyo mkunjufu na ukarimu? Ni upendo wa aina gani unaohusiana na ulipaji kisasi kuliko usamehevu? Inawezekanaje yeyote aamini upendo wetu, ikiwa sisi hatuaminiki?

Kwa uelewa huu wa upendo, hebu sasa tugeuzie umakinifu wetu kwa nguvu ya ufundishaji. Unapofundisha Hoja, unawasiliana na mwanadamu mwenzako. Haufundishi tu kinadharia. Fikiria kuhusu hisia ulizonazo kwa mtu umpendaye—rafiki kipenzi, mama na baba yako, kina-kaka na kina-dada, mume au mke, watoto wako. Hisia hizi ni halisi kabisa. Bila shaka, isingekuwa busara kuamini kwamba tungeweza kumpenda tusiyemjua kwa nguvu ile ile kama tuwapendavyo wale ambao wapo karibu nasi. Jambo muhimu kuelewa, walakini, ni kwamba kwa kufundisha tunadhihirisha upendo wetu kwa wanadamu, upendo ambao sharti utafsiriwe katika upendo thabiti kwa mtu mmoja mmoja wa mbari ya wanadamu. Haitoshi kwetu kuwa na upendo wa kinadharia tu kwa ajili ya utukuzaji dhahania wa wanadamu.

Swali muhimu la kuuliza kuhusiana na hili ni: kwa sababu gani tusimpende mtu, hata tusiyemjua, ambaye hata hivyo amevutika kwa kiasi cha kutosha kuja kusikiliza ujumbe wa Bahá'u'lláh? Katika kutafakuri swali hili, mfikirie 'Abdu'l-Bahá na Upendo Wake kwa wanadamu. Je, hakutiririsha upendo na wema kwa kila mwanadamu aliyekutana naye?

Ili kuongeza uelewa wako juu ya nguvu ya upendo katika kufundisha Hoja, amua kama yafuatayo ni kauli za kweli:

_____ Maneno ni maneno. Yana athari ile ile iwe unayasema kwa upendo moyoni mwako au la.

_____ Wakati maneno yanapovikwa upendo, yanakuwa na athari kubwa zaidi kwenye moyo wa msikilizaji.

_____ Tunaweza kumpenda tu mtu tunayemfahamu, kama vile mama au baba yetu, au rafiki kipenzi.

_____ Inawezekana kumpenda mtu tunayemfahamu kidogo tu.

_____ Kumuonesha upendo kila mwanadamu haiwezekani vinginevyo kwa kiasi fulani wewe ni mtakatifu.

_____ Kuwapenda wanadamu humaanisha kumpenda kila mwanadamu kwa kiwango kile kile.

_____ Kwamba mtu usiyemfahamu huchukua muda kuanzisha mazungumzo naye kuhusu Imani, hilo pekee husababisha upendo moyoni mwako kwake.

_____ Ni kinyume kusema, "nawapenda wanadamu lakini sitaki kumfundisha yeyote na kuwapa fadhili kubwa ambazo ni matokeo ya kumkubali Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku ya leo."

_____ Tusipofundisha Hoja, ni kwa sababu hatuna upendo wa kutosha kwa wanadamu.

_____ Si kwamba wale wanaosita kufundisha Hoja hawawapendi wanadamu. Inawezekana kuna vigezo vingine, kama vile woga, kutojiamini au aibu, ambavyo humzuia mtu aliyejawa na upendo kufundisha.

_____ Tunapaswa tuwafundishe marafiki zetu tu na siyo wale tusiowafahamu.

_____ Tunapaswa tuwapende wale wote tunaowafundisha.

_____ Ikiwa tunahisi kwamba hatuwapendi wanadamu kiasi cha kutosha hatupaswi kufundisha.

_____ Kitendo cha ufundishaji huongeza upendo wetu kwa wanadamu wenzetu. Kwa hiyo, tusifanye kutokuwa na upendo wa kutosha kama kisingizio cha kutofundisha.

_____ Ni upedo wetu kwa Mungu unaotusukuma kubeba wajibu mtakatifu wa kufundisha Imani, na upendo wetu Kwake hujenga mioyoni mwetu upendo kwa wanadamu.

## SEHEMU YA 28

Tumesema kwamba tunapofundisha, tunatafsiri upendo wetu kwa wanadamu katika upendo kwa mmoja au zaidi wa wajumbe wake binafsi. Nguvu ya upendo hujidhihirisha pale inapoelekezwa juu ya kitu au mtu. Sharti tukumbuke, hata hivyo, kwamba upendo wenyewe hauna mipaka. Upendo hauna kikomo, mipaka, ni wa milele. Upendo huu wa milele hauwezi kuelezwa ipasavyo unapokuwa unadhibitiwa na malengo finyu na yenye vizuizi. Tunapompenda mtu, ‘Abdu’l-Bahá hutuambia, “acha uwe kwa mwonzi wa Upendo usio na Mwisho! Acha uwe katika Mungu, na kwa ajili ya Mungu!” Upendo kwa Mungu “umetakasika zaidi ya dhana na fikra za watu.” Tunapaswa “tutawanye mwangaza wa upendo usio na mipaka juu ya kila mwanadamu” tunayekutana naye, ‘Abdu’l-Bahá husema. Hebu tukariri nukuu ifuatayo:

> **“Ewe mwale wa upendo wa Mungu! Mwonzi lazima umimine mwangaza na jua lazima lichomoze; mwezi mpevu lazima ung’ae na nyota lazima zimetemete. Kwa kuwa wewe ni mwonzi, msihi Bwana akuwezeshe kutoa mwangaza na wongofu, kuziangazia peo na kuuteketeza ulimwengu kwa moto wa upendo wa Mungu. Natumaini kwamba utaweza kulifikia daraja kama hilo, la, kulipita.”**[28]

## SEHEMU YA 29

Kumaliza kitengo hiki, tunapaswa tujikumbushe juu ya jambo la muhimu ambalo wote tumejifunza maishani mwetu: kwamba, bila msaada mtakatifu, hakuna kiwezacho kutimizwa. Tufundishapo Hoja, hivyo, daima tunapaswa tutambue juu ya msaada mtakatifu na kuomba nguvu kutoka majeshi ya Umati wa Juu. Hapo chini kuna vifungu vichache tu kati ya vingi kutoka Maandiko juu ya mada hii. Pengine ungependa kuvikariri, kama bado hujafanya hivyo hapo mwanzoni.

**"Kwa haki ya Mungu! Yeyote afunguaye midomo yake katika Siku hii na kulitaja jina la Bwana wake, majeshi ya uvuvio mtakatifu yatamshukia kutoka mbingu ya jina Langu, Ajuaye—Vyote, Mwenye Hekima—Kabisa. Juu yake pia utashuka Umati wa juu, kila mmoja akiinua juu kalisi ya mwanga uliotakasika. Hivyo ndivyo ilivyoamriwa hapo kabla katika milki ya Ufunuo wa Mungu, kwa amri ya Yule Ambaye ni Mtukufu—Kabisa, Mwenye Uwezo—Kabisa."**[29]

**"Yeye, kwa kweli, atamsaidia kila mmoja amsaidiaye Yeye, na atamkumbuka kila mmoja amkumbukaye Yeye. Kwa hili hushuhudia Waraka huu ambao hutawanya wangavu wa wema wa upendo wa Bwana wako, Mtukufu—Kabisa, Mshurutisha—Vyote."**[30]

**"Sema: Jihadharini, Enyi watu wa Bahá, msiache wenye nguvu duniani wawanyang'anye nguvu zenu, au wale ambao huutawala ulimwengu kuwajaza hofu. Wekeni imani yenu kwa Mungu, na kabidhini mambo yenu kwenye ulinzi Wake. Yeye, kwa kweli, kupitia nguvu ya ukweli, atawajalia washindi, na Yeye, kwa kweli, ni mwenye uwezo kufanya kile Apendacho, na mikononi Mwake zimo hatamu za nguvu za uwezo."**[31]

**"Kwa Mungu Ambaye zaidi Yake hakuna Mungu mwingine! Ikiwa yeyote atainuka kwa ajili ya ushindi wa Hoja Yetu, yeye Mungu atamjalia ushindi ingawa maelfu ya maadui watashirikiana dhidi yake. Na kama upendo wake Kwangu ukiwa imara zaidi, Mungu atasimamisha mamlaka yake juu ya nguvu zote za duniani na mbinguni. Hivyo ndivyo tulivyopulizia roho yenye uwezo katika sehemu zote."**[32]

**"Yeye atawaauni kwa majeshi yasioonekana, na kuwasaidia kwa majeshi ya uvuvio kutoka Umati wa juu; Atawatumia marashi mazuri kutoka Paradiso ya juu kabisa, na kuwapeperushia juu yenu pumzi safi ambayo hutoka kwenye bustani ya mawaridi ya Kundi la juu. Atapulizia katika mioyo yenu roho ya uzima, kuwafanya muingie katika Safina ya wokovu, na kuwafunulia dalili na ishara Zake dhahiri. Kwa kweli, hii ndio neema tele. Kwa kweli, huu ndio ushindi ambao hakuna awezaye kuukana."**[33]

**"Enyi watumishi wa Kizingiti Kitakatifu! Majeshi ya ushindi ya Umati wa Mbinguni, yaliyopangwa na kuongozwa katika Milki za juu, yamesimama tayari na yenye matarajio ya kusaidia na kuhakikisha ushindi kwa yule mpanda farasi jasiri ambaye kwa kujiamini humchochea farasi wake katika uwanja wa huduma. Heri ni yake yule mpiganaji jasiri, ambaye akiwa na silaha yenye nguvu ya Ujuzi wa kweli, huharakia uwanjani, huyatawanya majeshi ya ujinga, na kuyasambaratisha majeshi ya makosa, ambaye huinua juu Bendera ya Mwongozo Mtakatifu, na hupiga Parapanda ya Ushindi. Kwa haki ya Bwana! Yeye amefikia mafanikio matukufu na kupata ushindi wa kweli."**[34]

## MAREJEO


1. *Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2010, chapisho la 2015), na. 177.1, uk. 283.

2. *Nyaraka za ‘Abdu’l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá’í, 1915, chapisho la 1940), tol. 2, uk. 473, Kiingereza.

3. *Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 142.9, ku. 232–33, Kiingereza.

4. Kutoka barua ya 27 Machi 1933 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa Baraza la Kiroho la Mahali, iliyochapishwa katika *Habari za Kibahá’í*, na. 73 (Mei 1933), uk. 2.

5. *Nyaraka za ‘Abdu’l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá’í, 1916, chapisho la 1930), tol. 3, ku. 716–17, Kiingereza.

6. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofuniliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, chapisho la 2021), na. 13.4, uk. 241, Kiingereza.

7. Bahá’u’lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas: Kitabu Kitakatifu Kabisa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1993, chapisho la 2021), aya. 38, uk. 36; pia Buga *Kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1983, chapisho la 2017), LXXI, aya. 1, uk. 165, Kiingereza.

8. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXLIV, aya. 1, uk. 355.

9. Kama hapo juu, CLVIII, aya. 1, uk. 388.

10. Kama hapo juu, CLIV, aya. 2, uk. 374.

11. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 13.9, ku. 242–43.

12. *Nyaraka za ‘Abdu’l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá’í, chapisho la 1909, 1930), tol. 1, uk. 194, Kiingereza.

13. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, CXV, aya. 3, uk. 273, Kiingereza.

14. Kama hapo juu, CXXXIX, aya. 5, uk. 344.

15. Kama hapo juu, CXXIX, aya. 6, ku. 318–19.

16. Kama hapo juu, XCIX, aya. 1, ku. 226–27.

17. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 9.10, uk. 173, Kiingereza.

18. *Sala na Tafakari za Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, chapisho la 1987, 2008), CLXXIX, aya. 5, uk. 303, Kiingereza.

19. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 9.12, uk. 174.

20. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, LXXIV, aya. 1, uk. 160, Kiingereza.

21. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 11.30, uk. 214.

22. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXLVII, aya. 2, uk. 358.

23. Bahá'u'lláh, kama ilivyotajwa katika kitabu cha Shoghi Effendi, *Majilio ya Haki Takatifu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 2006, 218), aya. 114, uk. 125, Kiingereza.

24. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 13.18, uk. 246.

25. Kutoka barua ya 16 Februari 1932 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu mmoja, na kuchapishwa katika *Umuhimu wa Kujiongezea Elimu Yetu Zaidi na Ufahamu wa Imani*, makusanywa ya Dondoo kutoka Maandiko ya *Bahá'u'lláh*, Báb na 'Abdu'l-Bahá na barua za Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, makusanyo na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 2021), na. 103, ku. 48–49.

26. Kutoka barua ya 25 Aprili 1926 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu mmoja, kama hapo juu, na. 93, uk. 44; pia katika "Nyumba ya Haki ya Ulimwengu: Makusanyo yaliyoandaliwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu" (Februari 2021), aya. 58.13.

27. Kutoka Mazungumzo yaliyotolewa 16–17 Oktoba 1911, kuchapishwa katika *Paris Talks: Hotuba zilizotolewa na 'Abdu'l-Bahá, 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 2006, 2016), na. 1.13, uk. 7.

28. Kutoka Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá.

29. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXIX, aya. 3, uk. 317.

30. Bahá'u'lláh, kama ilivyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Majilio ya Haki Takatifu*, aya. 109, uk. 115.

31. Kama hapo juu, aya. 113, uk. 124.

32. Bahá'u'lláh, kama ilivyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Utaratibu wa Kiutawala wa Bahá'u'lláh, barua zilizochaguliwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1991), uk. 106.

33. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 157.4, ku. 259–60.

34. Kama hapo juu, na. 208.1, ku. 365–66.



# Sifa na Mielekeo Muhimu kwa ajili ya Ufundishaji

## Kusudi

Kutafakari juu ya sifa na mielekeo inayohitajika ili kufundisha Imani kwa ufanisi

## SEHEMU YA 1

Katika kutembea njia ya huduma iliyowekwa na mlolongo huu wa kozi, siyo tu umepata maarifa, stadi na uwezo vinavyohitajika bali pia umepata umaizi kuhusu baadhi ya sifa za kiroho na mielekeo ihitajikayo kufikia maendeleo thabiti. Tumetafakari juu ya mielekeo na sifa chache kama hizo katika kozi zilizotangulia, lakini hapa tutafikiria kuhusu zile kadhaa mahsusi, kwa kuwa zinahusiana na kitendo kitakatifu cha ufundishaji. Katika suala hili, kile ambacho hatupaswi kusahau, kama ilivyosisitizwa katika kitengo kilichotangulia, ni kwamba "kuwa" na "kutenda" ni vipengele viwili vinavyokamilishana na visivyotenganishika vya maisha ya kiroho. Jitihada zetu za kukamilisha hali yetu ya ndani na kukuza sifa za kiroho, muhimu kwa hali yetu ya kuwa, lazima ijidhihirishe katika uga wa huduma. Lazima tuinuke kufundisha, hivyo, kwa kuamini kwamba, kwa kufanya hivyo, sifa za kiroho ambazo zinatakiwa ziainishe kitendo hiki kitakatifu zitaimarishwa zaidi ndani mwetu. Kwa mujibu huu, orodhesha baadhi ya sifa ambazo unafikiri tunapaswa kujitahidi kuzidhihirisha kwa kiwango kikubwa zaidi na zaidi kama tunataka kuwa vyombo vyenye ufanisi uongezekao kwa ajili ya uenezaji wa Imani.

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

Katika sehemu inayofuata utapewa nukuu fupi zinazohusiana na sifa kadhaa za kiroho, ambazo baadhi yake bila shaka umezitaja hapo juu. Maswali na mazoezi yaliyomo katika kila sehemu yatakusaidia kuchunguza jinsi maendeleo ya sifa fulani huongeza ufanisi wako katika kufundisha Hoja. Ni muhimu kuweka wazi katika hatua hii kwamba majadiliano yetu hapa hayatahusiana na ufikiaji ukamilifu bali na kujitahidi kuelekea ukamilifu. Kwa mfano, katika sehemu inayofuata tutatoa mawazo jinsi uongezaji wa utakaso wa moyo wa mtu uongezavyo jitihada katika uga wa ufundishaji, hilo halimaanishi kwamba mtu hawezi kufundisha kama hajafikia kiini cha utakaso. Kwa kawaida, Maandiko hutuelekeza kwenye ukamilifu, na ikiwa hatulifahamu lengo, ni kwa namna gani tutajitahidi kulifikia?

## SEHEMU YA 2

Katika mojawapo ya Nyaraka Zake akitoa mwito juu yetu kueneza mafundisho, 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Kusudi ni hili: Dhamira ya mwalimu lazima iwe safi, moyo wake huru, nafsi yake imevutiwa, fikra yake yenye amani, azma yake thabiti, wema wake uliotukuka na katika upendo wa Mungu kurunzi ing'aayo."[1]**

Katika Waraka mwingine, Yeye hutusihi:

**“. . . muwe watakatifu juu ya, na mliotakasika kutoka ulimwengu huu na wakazi wake; acheni dhamira yenu ifanye kazi kwa manufaa ya wote; kateni mwambatano wenu na dunia na kama kiini cha roho, muwe wepesi na wororo. Ndipo kwa azma thabiti, moyo safi, roho yenye furaha, na ulimi fasaha, tumieni muda wenu katika uenezaji wa kanuni takatifu . . .”[2]**

Kwa nini unafikiri utakaso wa moyo na usafi wa dhamira ni vya lazima sana katika ufundishaji? Itakuwaje ikiwa dhamira zetu si safi lakini ni mahiri sana katika kujifanya na kuwathibitishia wengine kwamba ni safi? Baadhi ya najisi zinazokuja kwa urahisi akilini kuhusu ufundishaji ni hisia ya kujikweza, tamaa ya kutambulika, na tamaa ya makuu. Je, unaweza kuelezea jinsi gani kila moja ya hizi zinavyoweza kuathiri kitendo cha ufundishaji?

1. Hisia ya kujikweza: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

2. Tamaa ya kutambulika: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

3. Tamaa ya makuu: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

## SEHEMU YA 3

Barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi hueleza:

**“Bwana hutuhakikishia kwamba tunapojisahau wenyewe, na kujitahidi kwa nguvu zetu zote kutumikia na kufundisha Imani, tunapokea msaada mtakatifu. Siyo sisi tutendao kazi, lakini sisi ni vyombo vitumikavyo kwa wakati huo kwa kusudi la kufundisha Hoja Yake.”[3]**

Katika barua nyingine, yeye hueleza:

**“Roho moja tu iliyopevuka, yenye uelewa wa kiroho na ujuzi wa kina sana wa Imani, inaweza kuwasha moto nchi nzima—ni kuu mno nguvu ya Hoja kufanya kazi kupitia njia safi na isiyo na ubinafsi.”[4]**

Katika jitihada ya kuyafungamanisha maisha yetu na roho ya mafundisho, sote tunajaribu kujiondoa wenyewe ubinafsi na kujitahidi kutokuwa na ubinafsi. Katika safari hii kuelekea kutokuwa na ubinafsi, lazima tutambue kwamba inawezekana kuangukia katika mtego wa umimi hata kama nia ya mtu ni safi. Mtu anaweza kwa kweli kuwa na shauku katika maendeleo na usitawi wa wengine, bado akasukumwa na tamaa ya kuwa katikati ya kila jambo. Katika kulifikiria wazo hili "mimi nawasaidia wengine", mtu ambaye amekamatwa katika mtego huu atasisitiza juu ya "mimi" na siyo juu ya "wengine" au juu ya kitendo cha kusaidia. Jifikiria wewe mwenyewe unapozungumza na rafiki yako kuhusu Imani. Zipi kati ya kauli zifuatazo zingewasilisha fikra na hisia zako kama ungelikuwa unajaribu kwa utambuzi kuepukana na ubinafsi—kukwepa kuwa wewe ni kitovu cha kila kitu?

______ Mungu angefungua moyo wake na kumjalia uelewa wa kweli.

______ Natumaini kwamba mapungufu yangu mwenyewe hayatamzuia kuutambua ukweli wa Imani.

______ Kufundisha ni jambo zuri. Najisikia vizuri ninapomthibitishia mtu ukweli.

______ Baada ya yote niliyomfanyia, kumwelezea mambo kwa uangalifu mno, ni bora angekuwa Mbahá'í.

______ Natumaini kwamba rafiki yangu atamtambua Bahá'u'lláh na kuhisi furaha ile ile niliyoihisi mimi katika kuitumikia Hoja Yake.

______ Ee Mungu, tafadhali ingiza fikra sahihi akilini mwangu na unipe maneno sahihi ili niweze kushirikiana mafundisho kwa namna ambayo itaugusa moyo wake.

## SEHEMU YA 4

'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Inueni mioyo yenu juu ya wakati huu na tazameni siku zijazo kwa macho ya imani! Leo mbegu inapandwa, punje ya nafaka huangukia juu ya ardhi, lakini tazameni siku itawadia ambapo itainuka kuwa mti mtukufu na matawi yake yatasheheni matunda. Shangilieni na furahini kwamba siku hii imepambazuka, jaribuni kutambua nguvu yake, kwa kuwa kwa hakika ni ya ajabu! Mungu amewavika taji la heshima na mioyoni mwenu ameweka nyota angavu; kwa kweli mwangaza wake utauangaza ulimwengu mzima!"**[5]

Ushauri wa Mlinzi kwetu ni:

> **"Mnapaswa, kwa hiyo, kujitahidi kadiri muwezavyo, kubeba ndani mwenu kurunzi ya imani, kwa kuwa kupitia kwayo hakika mtapata mwongozo, nguvu na hatimaye mafanikio."**[6]

Kwa hakika mngekubali kwamba mara tu mtu amtambuapo Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa wakati huu, cheche ya imani inakuwa imewashwa moyoni mwake. Pia mngekubali, basi, kwamba wale wanaofundisha lazima wawe vyombo ambavyo kupitia humo cheche hii huwashwa. Lakini itakuwaje kama mwale wa imani hauwaki ndani ya mioyo yetu wenyewe? Ni kwa kitu gani tutawasha ile cheche katika moyo wa msikilizaji?

Tunaweza kuingia katika mazungumzo ya kuvutia mno na kutoa kauli zenye ufasaha kabisa, lakini, bila imani, haya yatakuwa na matokeo kidogo, kwa kuwa msikilizaji anaweza kuhisi ama tunaamini hasa yale tusemayo au la. Na kadiri kurunzi ya imani iwakavyo kwa wangavu zaidi mioyoni mwetu, ndivyo uwezekano ulivyo mkubwa zaidi wa kuwasaidia wengine kumtambua Bahá'u'lláh. Ni katika kitu gani, hata hivyo, tunapaswa kuwa na imani tunapoingia katika uga wa ufundishaji? Je, mnaweza kutaja vitu vichache? Baadhi ya mifano imetolewa kuwasaidia.

1. Imani katika nguvu ya msaada mtakatifu
2. Imani kwamba mafundisho ya Bahá'u'lláh ndio hasa yanayohitajika na wanadamu
3. Imani katika uwezo wa kila roho kumtambua Bahá'u'lláh
4. ____________________
5. ____________________
6. ____________________
7. ____________________
8. ____________________
9. ____________________
10. ____________________

## SEHEMU YA 5

'Abdu'l-Bahá hutusihi:

> **"Zungumza, kwa hiyo; zungumza kwa sauti na ujasiri mkuu katika kila mkutano. Unapokaribia kuanza mazungumzo yako, mgeukie kwanza Bahá'u'lláh, na omba mathibitisho ya Roho Mtakatifu, kisha fungua midomo yako na sema chochote kinachokujia moyoni mwako; hii, hataivyo, kwa ujasiri mkubwa kabisa, heshima na imani."**[7]

Na katika barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi, tunasoma:

> **"Mwalimu wa Kibahá'í lazima ajiamini kabisa. Humo ndimo ilimo nguvu yake na siri ya mafanikio yake. Ingawa bila msaada, na haidhuru utepetevu wa watu wakuzungukao unavyoweza kuwa, sharti uwe na imani kwamba majeshi ya Ufalme yapo upande wako, na kwamba kupitia msaada wake huna budi kuyashinda majeshi ya giza ambayo yanaikabili Hoja ya Mungu. Kwa hiyo, stahimili, uwe na furaha na mwenye imani."**[8]

Ili kukabiliana na hali mpya, kutojali kasoro zetu wenyewe, kuzungumza kuhusu Imani na wale ambao tumekutana nao hivi punde, kushiriki na wanadamu wenzetu kile ambacho tunafikiria ni chenye thamani kabisa ilhali tukitambua kwamba kinaweza kukataliwa—hii yote huhitaji ujasiri. Tunapata ujasiri, bila shaka, tunapomwamini Mungu na kuweka matumaini yetu yote juu Yake. Kujua kwamba Yeye atatuongoza na kutusaidia hutupa nguvu kufanya mambo ambayo vinginevyo tungeyaogopa. Hutokea nini kama tusipokuwa jasiri

tunapofundisha Hoja? Je, tutapoteza fursa? Toa baadhi ya mifano juu ya jinsi gani ujasiri unahitajika katika ufundishaji.

Kile tunachopaswa kutambua ni kwamba, ingawa tunahitaji ujasiri kufundisha, kitendo chenyewe cha kufundisha huongeza ujasiri wetu. Ili kukusaidia kukumbuka hili, pengine ungependa kukariri nukuu ifuatayo, kama bado hujaikariri:

> **"Chanzo cha ujasiri na nguvu ni uendelezaji wa Neno la Mungu, na uthabiti katika Upendo Wake."[9]**

## SEHEMU YA 6

'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Kazi ya ufundishaji katika hali zote sharti ifuatiliwe na waumini kwa bidii kwasababu mathibitisho ya Mungu huitegemea. Ikiwa Mbahá'í atajizuia kujihusisha kikamilifu na kazi ya ufundishaji, kwa nguvu zote na kwa moyo wote bila shaka atanyimwa baraka za Ufalme wa Abhá. Hata hivyo, shughuli hii inapaswa itumike kwa hekima—siyo ile hekima ambayo humtaka mtu kuwa mkimya na msahaulifu wa wajibu kama huo, bali ile imtakayo mtu kuonesha ustahimilivu mtakatifu, upendo, wema, subira, tabia njema na matendo matakatifu."[10]**

Na katika kifungu kingine Yeye hueleza:

> **"'Siyo kila kitu mtu ajuacho kinaweza kufichuliwa, wala siyo kila kitu anachoweza kufichua kinaweza kufirikiwa kama cha wakati unaofaa, wala sio kila tamko la wakati unaofaa linaweza kufikiriwa kama linalingana na uwezo wa wale walisikiao.' Hiyo ndiyo hekima kamili ya kuzingatiwa katika shughuli zako. Usiwe msahaulifu wa hilo, kama unapenda kuwa mtu wa vitendo katika hali zote.**

**Kwanza, chunguza maradhi na tambua ugonjwa, kisha amuru tiba, kwa kuwa hiyo ndiyo njia kamili ya tabibu mwenye ustadi."[11]**

Ujasiri lazima urekebishwe na hekima. Hii haimaanishi kwamba hekima inapaswa iuzuie ujasiri. Vyote viwili sharti viende sambamba. Tunapokuwa na ujasiri na hekima, kwa ushujaa tunaingia katika uwanja wa vitendo, na kwa uamuzi timamu na fikra safi, tunasonga mbele. Nini cha kusema na nini siyo cha kusema, namna bora ya kushughulikia masuala nyeti, na jinsi ya kujibu maswali—maamuzi yote haya sharti yafanywe kwa busara. Hekima, walakini, isiwe kisingizio cha kubweteka. Tusiangukie kwenye tabia ya daima kusema: "Isingekuwa busara kufanya hili. Isingekuwa hekima kufanya lile." Hapo chini kuna hali chache ambamo unaweza kujikuta. Je, unafikiri ni ipi itakayokuwa njia ya busara kabisa ya kuishughulikia kila hali?

1. Unajadili Imani na watu wawili. Kadiri mazungumzo yanavyoendelea, inakuwa dhahiri kwamba mmoja kati yao anavutiwa na Imani lakini yule mwingine havutiwi. Wewe utafanyaje?

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

2. Unakutana na mtu kwenye mkusanyiko na unaanza mazungumzo naye kuhusu Imani. Ingawa anakusikiliza kwa makini, hasemi chochote, wala haulizi maswali yoyote. Wewe utafanyaje?

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

3. Dada mmoja ambaye anaonekana kuvutiwa sana na Imani anakualika nyumbani kwake, ili aweze kujifunza zaidi kuhusu Imani. Unawasilisha sura mbalimbali za mafundisho, na ziara inaonekana kuwa inaenda vizuri. Anakwambia kwamba anapenda alichokisikia na anafikiri kwamba Imani ndiyo jibu la matatizo ya jamii ya wanadamu. Halafu anakuomba vipeperushi vichache kuhusu Imani aweze kuvisambaza kwenye mkutano wa kisiasa ambao yeye atahudhuria siku inayofuata. Wewe utafanyaje?

______________________________

______________________________

______________________________

4. Unashiriki katika kampeni ya majuma mawili katika kijiji chako. Kusudi ni kuongeza idadi ya wale wanaoshughulika katika jitihada za ujenzi wa jumuiya na kuzialika roho pokevu kuikumbatia Hoja. Bila shaka, familia nyingi tayari zinatambua shughuli za Kibahá'í kijijini hapo, au hata kujihusisha nazo kwa namna fulani, na unatumia siku za kampeni ukitembelea kaya na kuongea pamoja na wana-familia juu ya mada zinazoendana na upokevu wao. Nyakati za jioni, mikusanyiko ya wazi kwa kila mtu kijijini hapo hufanyika, ambapo vipengele mbalimbali vya mafundisho ya Imani na athari zake juu ya maisha ya jumuiya zinaongelewa.

Jioni moja, mtu mmoja anayehudhuria mkutano anakuuliza swali kuhusiana na sheria mahsusi ya Kibahá'í. Unamjibu, lakini yeye hakubaliani na maelezo yako. Washiriki wengine wachache wa kampeni kisha wanajaribu kuongelea suala hilo, lakini, baada ya muda kidogo, inakuwa dhahiri kwamba, yeye anajaribu kuidharau Imani mbele ya wale waliohudhuria. Wewe utafanyaje?

5. Wewe ni mjumbe wa timu inayofanya ziara za nyumbani katika ujirani kwa matumaini ya kuongeza idadi ya watoto wanaoshiriki katika madarasa kwa ajili ya elimu yao ya kiroho. Familia nyingi zinatambua kuhusu madarasa ambayo tayari yameshanzishwa, na wanafurahia maendeleo haya katika ujirani na wana furaha kujifunza zaidi. Wakati wa ziara zako, unajikita zaidi juu ya baadhi ya dhana za kielimu zinazopatikana katika maandiko ya Kibahá'í, ambazo huchochea majadiliano yenye uchangamfu pamoja na wazazi. Katika kaya moja, walakini, mgeni mmoja aliyekuwa amewatembelea alionesha wasiwasi, akisema kwamba wewe pengine ulikuwa unajaribu kuwabadili dini watoto walio katika madarasa ili waingie katika Imani. Wewe utafanyaje?

6. Kijana mmoja ambaye amekuwa akisoma kozi za taasisi kwa kipindi fulani na kuhudumu kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi ameamua kujiandikisha katika Imani. Walakini wazazi wake wana wasiwasi kuhusu uamuzi wa mtoto wao. Wewe utafanyaje?

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

## SEHEMU YA 7

Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Iwapo yeyote miongoni mwenu anashindwa kuufahamu ukweli fulani, au anajitahidi kuuelewa, muoneshe wazi, unapokuwa unazungumza naye, moyo wa wema mkuu nia njema. Msaidie kuuona na kuutambua ukweli, bila kujiona wewe mwenyewe, hata kwa kiasi kidogo, bora kuliko yeye, au kuwa aliyejaliwa zaidi."[12]**

Katika kifungu kingine, Yeye anatuasa:

**"Andamaneni na watu wote, Enyi watu wa Bahá, kwa moyo wa urafiki na upatano. Kama mkiutambua ukweli fulani, kama mna johari, ambayo wengine wamenyimwa, shirikini nao katika lugha ya wema mkuu kabisa na nia njema. Kama ikikubaliwa, kama ikitimiza kusudi lake, lengo lenu limefikiwa. Kama yeyote akiikataa, mwacheni yeye mwenyewe, na msihini Mungu amuongoze. Jihadharini msije mkamtendea isivyo vyema. Ulimi mwema ni sumaku ya mioyo ya watu. Ni mkate wa roho, unavika maneno kwa maana, ni chemchemi ya mwangaza wa hekima na uelewa."[13]**

Sisi sote tunajitahidi kuonesha wema wa upendo na subira katika shughuli zetu na watu. Lakini tusichanganye wema na mambo mengine. Kwa mfano, wakati mwingine kile kinachoonekana kuwa wema kinaweza, kwa kweli, kuwa hali ya ubaba. Mtu ambaye anapata shida kuutambua uwezo wa watu na mara nyingi huwatendea wema, lakini kana kwamba wao ni watoto, huo ni ubaba. Unafiki pia unaweza kujionesha wenyewe kama wema; mtu anaweza kuonesha wema wa upendo wa hali ya juu kabisa lakini hasa akiwa na maslahi yake mwenyewe akilini. Kama vile wema, subira wakati mwingine waweza kutumika vibaya. Mathalani, inaweza kuwa kisingizio cha kutowajibika. Ili kufikiria zaidi juu ya mawazo haya, fanya zoezi hili hapo chini.

1. Unamwelezea mtu fulani mafundisho ya Imani kwa wema mwingi. Lakini mwishoni anapoonesha namna fulani ya kutokubaliana na wewe, unakereka. Je, wema wako ulikuwa wa kweli? ______________________

2. Unapokuwa unalezea Imani kwa wale ambao wana elimu ndogo rasmi kuliko wewe, unakatisha mara nyingi na kusema: "Je, mnaelewa, wapendwa?" Je, huu ni wema au ubaba? ___________________

3. Unamtambulisha Imani mtu mmoja mwenye elimu ndogo rasmi. Unaamua kwamba mawazo mengi ya Kibahá'í ni magumu mno kwa yeye kuyaelewa, hivyo unaupunguza Ujumbe wa Bahá'u'lláh hadi kufikia kwenye mawazo machache rahisi. Je, huu ni wema au ubaba? ________________________

4. Unamtambulisha Imani mtu mmoja mwenye elimu ndogo rasmi. Ingawa huchukua muda, unampa maelezo ya kina ya kweli za lazima, ukisoma naye vifungu husika kutoka Maandiko na kujadiliana maana zake. Je, hii ni subira au ubaba? ___________

5. Mmoja wa majirani zako anaonekana kuwa mpokevu kwa Imani, hivyo unaamua kumhusisha katika mfululizo wa majadiliano. Wakati wa mazungumzo yenu na kwa wema mkubwa, unamsaidia kupata utambuzi wa umuhimu wa mafundisho ya Kibahá'í na kulea uelewa wake mpaka anamtambua Bahá'u'lláh. Baada ya kujiandikisha katika jumuiya, unaendelea kumlea na kumsaidia kadiri anavyoendelea kujifunza zaidi kuhusu mafundisho na kuanza kuyashiriki pamoja na wengine. Je, huu ni ubaba? _______________________

6. Wakati wa kampeni ya kutembelea kaya katika ujirani wa karibu, unakutana na baba ambaye anaonesha shauku ya kujifunza kuhusu Imani. Baada ya mazungumzo mafupi, anakuambia kwamba amefurahia alichokisia na anakuomba vitabu vya kusoma. Unampa kitabu kidogo cha utambulisho na unaamua kwamba, kwa kuwa anaonekana ametingwa, utasubiri miezi michache kabla ya kumtembelea tena. Je, hii ni subira au kutowajibika? ________________________________

Je,unaweza kufikiria hali zingine ambamo kunaweza kuwa na ubaba au unafiki fulani katika umbo la wema, au kutowajibika katika umbo la subira?

## SEHEMU YA 8

Bahá'u'lláh hutamka:

**"Kama wakiinuka kufundisha Hoja Yangu, lazima waruhusu pumzi ya Yule Asiyezuilika iwaamshe, na lazima waieneze mbali duniani kwa azma ya juu, wakiwa na fikra ambazo zimekaziwa kabisa Kwake, na kwa mioyo ambayo imejitenga kabisa na huru kutokana na vitu vyote, na kwa roho ambazo zimetakasika kutokana na ulimwengu na uchafu wake. Imewapasa wachague kama maandalizi bora kabisa kwa ajili ya safari yao kumtegemea Mungu, na kujivika wenyewe kwa upendo wa Bwana wao, Aliyetukuka—Kabisa, Mtukufu—Kabisa. Kama wakifanya hivyo, maneno yao yatawashawishi wasikilizaji wao."**[14]

'Abdu'l-Bahá husema:

**"Hawa watafanya kazi bila kukoma, mchana na usiku, hawatajali majaribu wala majonzi, hawatakubali kupumzika katika jitihada zao, hawatatafuta starehe, hawatajali raha zote na faraja, na, wakijitenga na bila mawaa, wataweka wakfu**

**kila wakati upitao haraka wa maisha yao katika uenezaji wa manukato matakatifu na utukuzaji wa Neno takatifu la Mungu.”[15]**

Tunajua kutoka usomaji wetu wa Kitabu cha 2 kwamba kujitenga ni hitaji la ufundishaji wenye furaha. Wakati tunatumaini kwamba huduma tunayoitoa huzaa matokeo stahiki, tunatambua kwamba kama tunajifungamanisha mno na matokeo, kama tunaathiriwa mno na sifa au kukosolewa, tutapoteza furaha ambayo huharakisha hatua zetu. Ukamilishaji wa sentensi hizo hapo chini utakusaidia kufikiria zaidi juu ya maana ya kujitenga pale tunapoingia katika uga wa ufundishaji.

1. Tuinukapo kufundisha Hoja, inatupasa turuhusu ________________________ ________________________________________________ ituamshe.

2. Tuinukapo kufundisha Hoja, fikra zetu zinapaswa ____________________ ________________________________ .

3. Tuinukapo kufundisha Hoja, mioyo yetu inapaswa ____________________ ________________________ , na huru kutokana na ________________________ .

4. Tuinukapo kufundisha Hoja, roho zetu zinapaswa _____________________ _____________________________________________________ .

5. Inatupasa tuchague kama maandalizi bora kabisa kwa safari yetu ________________ ______________________ .

6. Inatupasa tujivike wenyewe _______________________________ .

7. Na baada ya kuingia uga wa huduma, tunapaswa tufanye _____________________ , mchana na usiku.

8. Tunapaswa tusijali ________________ wala _______________ , sharti tusitafute _______________ , na tusijali ______________________________ yoyote.

9. Tukijitenga na bila mawaa, tunapaswa _____________________________ __________________ wa maisha yetu katika _____________________________ ____________________ na ___________________________________________ .

## SEHEMU YA 9

Bahá’u’lláh hutuambia:

**“Pazeni sauti na muwaite watu kwa Yule Ambaye ni Bwana Mwenye enzi wa malimwengu yote, kwa ari na bidii kubwa mno kiasi kwamba watu wote waweze kuwashwa kwa moto wenu.”[16]**

Shoghi Effendi anatusihi:

> **“. . . hebu tuinuke kufundisha Hoja Yake kwa uadilifu, kusadikisha, uelewa na nguvu. Acha huu uwe wajibu mkuu na muhimu sana kwa kila Mbahá’í. Hebu tuufanye kuwa shauku kubwa inayotawala maisha yetu.”**[17]

Kama tunataka kufanikiwa katika jitihada zetu za kuongoza idadi kubwa ya watu kwenye bahari ya Ufunuo wa Bahá’u’lláh, lazima tusukumwe na shauku kali ya kufundisha Imani. Mioyo yetu lazima iwashwe kwa shauku, vinginevyo tutawasilishaje furaha ya kuwa Wabahá’í, kama sisi wenyewe hatuna furaha na shauku? Lakini katika shauku yetu ya kushiriki Ujumbe wa Bahá’u’lláh na wengine, sharti tuwe waangalifu kutovuka mipaka stahiki na kuwafukuza wale tunaotaka kuwafundisha. Neno ambalo mtu aghalabu hulisikia kuhusiana hili ni “uongoaji”, ambalo humaanisha kumwekea mtu shinikizo lisilofaa kubadili Imani yake. Wabahá’í wanakatazwa kabisa kuongoa. Walakini, katika kuepukana na uongoaji, tusiwe watepetevu mno na tusioweza kushawishi kiasi kwamba jitihada zetu za ufundishaji zinakuwa hazina matokeo.

Ili kukusaidia kufikiri juu ya tofauti kati ya shauku katika ufundishaji na uongoaji, soma sentensi zifuatazo na amua ni katika hali gani ungekuwa unavuka mipaka stahiki. Ziwekee alama ya “VM”. Katika hali zipi usingekuwa na shauku kabisa kiasi kwamba usingekuwa mwenye ufanisi? Ziwekee alama ya “BS”. Katika hali zipi ambapo uendeaji wako ungekuwa wa shauku na ndani ya mipaka inayofaa? Ziwekee alama ya “S”.

_____ Umevutiwa mno na Imani kiasi kwamba kila fursa inapojitokeza unaingiza katika mazungumzo yako, kwa namna ya kawaida na kwa hekima, kanuni na mafundisho ya Kibahá’í. Pale panapofaa, unataja Chanzo cha mawazo yako kuwa ni mafundisho ya Bahá’u’lláh.

_____ Una shauku mno kiasi kwamba hata kama watu hawataki kusikiliza mazungumzo yako juu ya Imani, wewe unawalazimisha kukusikiliza.

_____ Hutaki watu wakufikirie kwamba wewe una msimsamo mkali kuhusu dini yako, hivyo hata kama wakikuuliza kuhusu Imani, unatoa jibu fupi tu. Wakiendelea kuuliza tena, ndipo hatimaye unawapa kitabu na kuwaambia wakisome wao wenyewe.

_____ Kampeni imeandaliwa kufundisha Imani katika vijiji kadhaa ambako watu ni wazi na wapokevu sana. Timu yako inaamua kuwa njia bora kabisa ni kwenda kutembelea nyumba hadi nyumba na kuitambulisha Imani kiasi kwamba, kwa kweli, watu wengi wangechukia kama ungemtembelea jirani mmoja na usingewatembelea wao.

_____ Kampeni shadidi imeanzishwa hivi karibuni katika kijiji jirani kuchunguza pamoja na wale walioingia katika Imani hivi karibuni mada za kuongeza ufahamu wao wa mafundisho. Wewe unazitembelea kaya chache lakini, kila unapokwenda, unaambiwa na wana-familia wengine kwamba wale unaowatafuta hawapo. Wewe unaondoka huku umevunjika moyo.

_____ Kampeni shadidi imeanzishwa hivi karibuni katika kijiji jirani kuchunguza pamoja na wale walioingia katika Imani hivi karibuni mada za kuongeza

ufahamu wao wa mafundisho. Ingawa huwakuti nyumbani wengi wa wale unaowatafuta, wewe unawasalimia wana-familia wengine unaowakuta na, kwa kujua kwamba watu katika kijiji hiki ni wa wazi na wapokevu, unawauliza kama wangependa kujihusisha katika mazungumzo kuhusu Imani.

_____ Wewe ni mjumbe wa timu ya ufundishaji katika kijiji jirani ambako watu wana fursa ndogo ya kupata huduma za elimu rasmi na afya, hivyo timu inaamua kwamba njia bora kabisa ni kusisitiza juu ya mambo yote mazuri yanayoweza kufanywa na Imani kwa ajili yao. Unawaahidi kwamba endapo watakubali kuwa Wabahá'í, utawasaidia kuanzissha shule kwa ajili ya watoto wao na kliniki ndogo ya afya.

_____ Wewe ni mjumbe wa timu ya ufundishaji katika kijiji jirani ambako watu wana fursa ndogo ya kupata elimu rasmi. Walakini una imani katika uwezo wao wa kiroho na hukwepi kufanya nao mazungumzo ya kina juu ya mafundisho ya Bahá'u'lláh. Unawaeleza wajumbe wa halmashauri ya kijiji jinsi kozi za taasisi, ambazo zimeegemezwa kwenye mafundisho haya, zinavyoweza kuwasaidia kujenga uwezo wa kufanya kazi kwa ajili ya kuboresha jumuiya. Unaahidi kurudi na kukisaidia kikundi kidogo cha vijana katika kujifunza kozi ya kwanza.

_____ Unaanza kila mkutano pamoja na wale wenye kuvutiwa kujifunza Imani kwa kuwapa kadi ya kujitangaza na unawaalika wajiunge na wawe wajumbe wa jumuiya ya Kibahá'í wakati wowote wao wakapokuwa tayari.

_____ Aghalabu unaanza kila mkutano pamoja na wale wenye kuvutiwa kujifunza Imani kwa kuwaambia kuwa ujumbe wa Bahá'u'lláh ni kwa ajili ya jamii nzima ya wanadamu na kwamba ndiyo furaha kushiriki baadhi ya mafundisho Yake pamoja nao. Pia unataja kwamba katu wasisite kuuliza maswali yoyote yanayokuja akilini mwao, ambayo wewe ungejaribu kuyajibu kwa uwezo wako wote. Kuelekea mwishoni mwa mkutano, pale inapofaa, unaelezea nini maana ya kuingia katika Imani, ikikumbukwa, bila shaka, kwamba hilo ni suala la mtu binafsi la kutafakariwa na kila mtu, bila shinikizo.

_____ Wewe huanza kila mkutano na wale wanaovutika kwenye Imani kwa kuwaelezea kwamba kusudi la mikudsnyiko hiyo siyo kuwabadili dini. Ungependa tu kushiriki nao mawazo machache. Ni muhimu kwamba wao wachukue muda wa kutosha kuchunguza ukweli kabla ya kufikiria uwezekano wa kujiandikisha katika jumuiya ya Kibahá'í.

_____ Umekuwa ukimfundisha rafiki mmoja kwa muda sasa na unaanza kuona cheche ya imani katika moyo wake, hivyo siku moja unamkaribisha kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í.

_____ Umekuwa ukimfundisha rafiki mmoja kwa muda sasa na unaanza kuona cheche ya imani katika moyo wake, hivyo unaendelea kumkaribisha katika shughuli za Kibahá'í ukidhani kwamba siku moja atakuwa Mbahá'í.

_____ Wewe ni mjumbe wa timu inayohiriki katika kampeni ya kufundisha Imani katika ujirani wako. Wewe huchangii hasa katika majadiliano na mipango

lakini unatumia muda wako mwingi ukiangalia simu yako ya kiganjani. Kampeni inapoanza, unaacha kuangalia simu yako mara moja moja kuona kinachoendelea na kutingisha kichwa katika kukubaliana na wajumbe wengine wa timu ambao wanaendelea na majadiliano katika mazungmzo pamoja na watu katika ujirani.

_____ Wewe ni mjumbe wa timu inayohiriki katika kampeni ya kufundisha Imani katika ujirani wako. Timu yako inakwenda mahali pa hadhara, na wewe unamsimamisha kila mtu anayekupita na kumuuliza: "Je, umewahi kusikia juu ya Bahá'u'lláh?"

_____ Unashiriki katika kampeni ya kuongeza nguvu za jitihada ya ujenzi wa jumuiya katika ujirani mmoja. Kama sehemu ya awamu ya kwanza ya kampeni, kikundi chako—kinachojumuisha marafiki wachache ambao wamehamia hapo hivi karibuni—kinatembelea ujirani na kujifahamisha na mazingira, kama vile shule, bustani, vituo vya kijamii ambako ungeweza kukutana na vijana wenye shauku ya kuitumikia jamii ya wanadamu. Kufuatana na kinachojifunza, kikundi kinaandaa mpango wa kufanya shughuli kadhaa: kutumia muda katika mazingira haya, kufanya uwasilishaji katika shule ya sekondari ya eneo hilo, kufanya mikusanyiko ya jioni na kutembelea kaya za watu binafsi ambao huonesha shauku kuingia katika mchakato wa kielimu unaoendelezwa na taasisi. Unapokutana na vijana hao, unajadiliana nao tabia maalum ya kipindi cha ujana na maana ya kutembea kwenye njia ya huduma ambapo wanaweza kujifunza kuwasaidia wengine, hususan wale ambao ni wadogo zaidi yao wenyewe, katika kupata maarifa, stadi na sifa za kiroho. Unamwalika kila mtu ambaye angependa kujifunza zaidi kuendelea na mazungumzo katika mikusanyiko ambayo wewe umepanga kufanya kila jioni. Mnajiandaa kumsaidia yeyote anayetaka kuanza masomo yao ya mlolongo mkuu wa kozi na kuambatana nao katika vitendo vya huduma watakavyovifanya. Pia mnatambua kwamba baadhi wataikubali Imani hivi punde, na ninyi hamtajizuia kuwakaribisha kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í.

_____ Unashiriki katika kampeni ya kuongeza nguvu za jitihada ya ujenzi wa jumuiya katika ujirani mmoja. Kama sehemu ya awamu ya kwanza ya kampeni, kikundi chako—kinachojumuisha marafiki wachache ambao wamehamia hapo hivi karibuni—kinatumia muda mrefu katika bustani, shuleni na katika vituo vya kijamii wakiongea na vijana na kuwakaribisha kwenye mikusanyiko inayofanyika nyakati za jioni. Unawahakikishia kwamba wewe utakuwepo muda wa kutosha kwa ajili ya kuimba pamoja na kufahamiana, ukipuuzia kusudi la mkusanyiko huo, ambalo ni kujadiliana nao jinsi wanavyoweza kuelekeza nguvu zao katika kuihudumia jumuiya yao. Wewe unaamini kwamba kama ukiteka shauku yao kwa njia hii na kujenga nao mafundo ya urafiki, itakuwa rahisi kuingia katika mazungumzo kuhusu tabia maalum za kipindi cha ujana na umuhimu wa kutembea kwenye njia ya huduma. Wakati idadi ndogo tu ya wale wanaohudhuria mikusanyiko ya jioni hubaki pindi wanapoelewa kwa nini wamealikwa, wewe unaamua kwamba itakupasa kuvutia idadi kubwa zaidi ikiwa unataka kutimiza malengo uliyoyatazamia.

_____ Unashiriki katika kampeni ya juma moja kuzitembelea familia nyingi katika kijiji chako zenye vijana wadogo waliopo katika madarasa ya watoto au vikundi vya vijana chipukizi. Timu yako inapanga idadi kubwa ya kaya na kuzialika familia zinazoonekana kuwa pokevu kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í. Unaamua kwamba njia bora kabisa ingekuwa kutaja mawazo mawili tu ambayo unadhani yangewavutia wenyeji, ukiepukana na mada ambazo ingawa ni muhimu, zingeweza kuibua maswali; kisha utawakariisha wana-kaya wa kila nyumba kujiandikisha.

_____ Unashiriki katika kampeni ya juma moja kuzitembelea familia nyingi katika kijiji chako zenye vijana wadogo waliopo katika madarasa ya watoto au vikundi vya vijana chipukizi na unawakaribisha wale ambao ni wapokevu kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í. Timu yako inatanabahi kwamba familia nyingi inazozitembelea zina shauku ya kuongelea mafundisho ya Kibahá'í, baadhi wakiikubali Hoja upesi na wengine wakiuliza maswali ambayo wangependa kuchunguza zaidi. Wewe unatambua kwamba kampeni hii ni sehemu ya mchakato wa muda mrefu unaoendelea wa upanuzi na uimarishaji, na hivyo unatumia muda wa kutosha na kila familia, ukijibu maswali yanayoibuka na kuongeza uelewa wao wa mafundisho ya Imani. Kwa namna hii, mbali na kuchangia kwenye ukuaji kwa maana ya kiidadi na kwenye uzidishaji wa shughuli, kila ziara huimarisha mizizi ya Imani katika jumuiya.

## SEHEMU YA 10

Kama ilivyotajwa hapo awali, msisitizo ambao tumeuweka juu ya sifa za kiroho katika majadiliano yetu ya ufundishaji haumanishi kwamba sharti tuwe wakamilifu ili tuweze kufundisha Hoja. Tunaagizwa, badala yake, kuinuka na kuitumikia Imani wakati kila mara tukitafakari juu ya hali yetu ya ndam na kujitahidi kudhihirisha kwa kiwango kikubwa zaidi na zaidi sifa kama vile usafi wa moyo, kutojipendelea, imani, ujasiri, busara, wema wa upendo, na kujitenga. Bila shaka, kuna sifa zingine ambazo zinahitaji umakinifu wetu—ukarimu, wema, na uthabiti, tukizitaja chache. Lakini uchunguzi wetu hapa ungekuwa na kasoro kama tusingejadiliana sifa ya unyenyekevu.

Njia za unyenyekevu, bila shaka, ni ngumu kuelezeka. Ni pale tunapompenda Mungu kabisa na kuwa wasahaulifu wa "nafsi", tukinyenyekea kwenye Mapenzi Yake, ndipo maneno na vitendo vyetu hujazwe uwezo. 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Mwalimu, wakati afundishapo, lazima yeye mwenyewe awe amewashwa kikamilifu, ili matamshi yake, kama vile mwale wa moto, yaweze kuwa na ushawishi na kuuteketeza utando wa nafsi na shauku. Pia, lazima awe mnyenyekevu kabisa na mdhilifu ili wengine waweze kuadilishwa, na mpole kabisa na asiye na makuu ili aweze kufundisha kwa lahani ya Umati wa juu—vinginevyo ufundishaji wake hautakuwa na matokeo."[18]**

Na katika jitihada yetu ya kuwasaidia wengine kuutambua ukweli wa Hoja, 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

**"Kulingana na mafundisho matakufu katika Kipindi hiki Kitakatifu sharti tusimtweze yeyote na kumuita mjinga, tukisema: 'Wewe hujui, lakini mimi najua.' Bali, tunapaswa tuwaangalie wengine kwa heshima, na tunapojaribu kuelezea na kuonesha, sharti tuzungumze kana kwamba tunachunguza ukweli, tukisema: 'Hapa mambo haya yapo mbele yetu. Hebu tuchunguze tuweze kuamua wapi na kwa jinsi gani ukweli unaweza kupatikana.' Mwalimu hapaswi kujifikiria mwenyewe kama mjuzi na wengine kama wajinga. Fikra kama hiyo huleta kiburi, na kiburi hakisaidii kuleta ushawishi. Mwalimu asijione kuwa na ubora wowote nafsini mwake; sharti azungumze kwa wema, udhilifu na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa, kwa kuwa kauli kama hiyo hushawishi na kuelimisha roho."**[19]

Kuna tofauti gani kati ya shauku iliyotajwa katika nukuu ya kwanza hapo juu na shauku iliyojadiliwa katika sehemu iliyofuata?

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

Pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako, jadilini jinsi unyenyekevu unavyoongeza ushawishi wa maneno yetu. Andikeni mawazo yenu machache.

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 11

Mjadala wetu katika sehemu iliyopita huibua kipengele kingine kinachohusu unyenyekevu ambao unastahili umakinifu wetu. Ni kweli kwamba lazima tuendelee kujitahidi kukamilisha tabia zetu na kuboresha hali zetu za ndani, tukitambua kwamba ufanisi wa jitihada zetu za kufundisha hutegemea na sifa za kiroho tunazozidhihirisha. Walakini kamwe tusidhani, hata kwa kitambo kidogo, kwamba mafanikio yetu katika uga wa ufundishaji ni matokeo ya ustahiki wetu wenyewe. Unyenyekevu hutulinda tusipate hisia ya kujikweza.

Daima tunapaswa tutenganishe mafanikio yetu katika ufundishaji wa Hoja na sisi wenyewe. Nafasi yoyote tuliyonayo katika kuisaidia roho kumtabua Bahá'u'lláh ni karama iliyojaliwa kwetu na Mungu. Yeye huwachagua wale ambao kupitia kwao atatenda kazi. Tunaweza tu kutumaini kuwa njia ambayo kwayo Yeye hutenda kazi na kujitahidi kujipatia zile sifa ambazo zitatuwezesha kuwa vyombo Vyake. Katika Maneno Yaliyofichwa tunasoma:

**"Jinyenyekeze mbele Yangu ili kwa hisani nipate kukutembelea. Inuka kwa ajili ya ushindi wa hoja Yangu ili bado ungali duniani uweze kupata ushindi."**[20]

Kifungu kifuatacho kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kinatupa onya:

> **"Pengine sababu kwa nini hukupata kutimiza mengi mno katika uga wa ufundishaji ni kwa kiwango ulivyoangalia udhaifu wako mwenyewe na unyonge kueneza Ujumbe. Bahá'u'lláh na Bwana wote wawili wametuhimiza mara kwa mara kutojali mapungufu yetu wenyewe na kuweka imani yetu yote kwa Mungu. Yeye atatusaidia kama tu tukiinuka na kuwa njia amilifu kwa ajili ya neema ya Mungu. Je, unafikiri ni walimu ambao huongoa na kubadilisha mioyo ya watu? La, kwa hakika sivyo. Wao ni roho safi tu ambao huchukua hatua ya kwanza, na kisha kuiruhusu roho ya Bahá'u'lláh kuwasukuma na kuwatumia. Kama yeyote kati yao angediriki kufikiria hata kwa sekunde moja kwamba mafanikio yanatokana na uwezo wake mwenyewe, kazi yake ingekoma na anguko lake huanza. Hii kwa kweli ndio sababu ya kuanguka kwa roho nyingi mno hodari baada ya huduma za ajabu walizofanya ghafla walijikuta wenyewe wasiofaa kabisa na pengine kutupwa kando na Roho ya Hoja kama roho zisizofaa. Kigezo ni kiwango ambacho kwacho tupo tayari kuruhusu mapenzi ya Mungu kutenda kazi kupitia kwetu.**
>
> **"Acha kuangalia kasoro zako, kwa hiyo; uwe na imani kamili kwa Mungu; acha moyo wako uwake kwa shauku ya kutumikia dhima Yake na kuutangaza mwito Wake; na utaona jinsi ufasaha na nguvu ya kubadilisha mioyo ya wanadamu vitakavyokuja kama jambo la kawaida.**
>
> **"Shoghi Effendi kwa hakika atasali kwa ajili ya mafanikio yako kama utainuka na kuanza kufundisha. Kwa kweli kitendo tu cha kuinuka kitakupatia msaada na baraka za Mungu."[21]**

Je, unaweza kutoa mifano michache jinsi gani kiburi na ufidhuli hutufanya tusifae kufundisha Hoja?

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

Sasa, ili kufikiria zaidi kuhusu sura tofauti tofauti zinazoweza kuchukuliwa na kiburi kuhusiana na ufundishaji, fanya zoezi lifuatalo:

1. Jitihada ya pamoja inafanyika kuwafundisha Imani watu binafsi na familia wanaojihusisha na shughuli za ujenzi wa jumuiya katika ujirani mmoja. Washiriki wamegawanywa katika timu na wanaombwa kutumia njia ambayo imethibitisha kuwa inafaa katika matukio yaliyotangulia. Mshiriki mmoja, hata hivyo, hahisi kuwa njia hiyo humwezesha kutumia vile anavyovichukulia kama vipaji vyake bora kabisa. Lipi kati ya majibu yafuatayo huonesha utovu wa kiburi kwa upande wake?

_____ Kukataa kushiriki katika jitihada hiyo kwa sababu haimruhusu kutumia vipaji vyake kama apendavyo.

_____ Kushiriki katika jitihada kwa furaha, akifanya kazi bega kwa bega na washiriki wenzake kwa njia yoyote ile ihitajikayo na akitumia uwezo wake mwingine.

_____ Kujaribu kutafuta kasoro kwa jitihada ya pamoja, akisema kwamba hii haitumii mbinu nzuri kwa sababu haichoti vipaji na uwezo wote wa washiriki.

2. Kikundi cha marafiki kinachohudumu katika ujirani husikia kuhusu mbinu ya ufundishaji ambayo inaleta matokeo mazuri sana katika ujirani mwingine katika eneo hilo. Lipi lipi kati ya yafuatayo lingekuwa jibu linalofaa kabisa, kwa kikundi, ambalo halioneshi kiburi wala utovu wa hekima?

_____ Kufikia uamuzi bila kuichunguza mbinu yenyewe, kwamba isingewezekana kabisa kufanyika katika ujirani wao kwa kuwa mazingira ni tofauti.

_____ Kufikia uamuzi kwamba, kwa kuwa mbinu hiyo imefanya kazi katika sehemu moja, lazima ifanye kazi sehemu nyingine na lazima ichukuliwe na kutumika kwa haraka bila mabadiliko.

_____ Kuichunguza mbinu hiyo kwa uangalifu ili kuona kama mbinu nzima au sehemu yake inayoweza kufanya kazi katika mazingira mapya na, kwa msingi huo, kuichukua mbinu hiyo na halafu kuirekebisha ipasavyo kufuatana na jinsi tajiriba inavyoonesha.

3. Mtu mmoja kutoka ujirani ambako mchakato wa ujenzi wa jumuiya uliopiga hatua kubwa, anatembelea ujirani ulio karibu kwa ombi la asasi za Imani. Huko kazi zinaendelea lakini hazijapiga hatua sana na yeye ameombwa kuwasaidia marafiki katika jitihada zao. Ni lipi kati ya yafautayo huonesha utovu wa kiburi kwa upande wake?

_____ Kuwaambia kwa uwazi marafiki katika ujirani huo kwamba yeye ametumwa na asasi na anawasilisha orodha ndefu ya maagizo ya mambo wanayopaswa kuyafuata.

_____ Kuongelea kwa mfululizo na kuyasifu sana maendeleo yanayofanyika katika eneo lake na bila kutoa fursa kwa wale wa ujirani aliowatembelea kushiriki tajiriba kutoka uhalisia wao wenyewe.

_____ Kusikiliza yale ambayo marafiki katika ujirani wanataka kusema kuhusu tajiriba yao, kushirikiana nao katika upangaji na utendaji, na kushirikishana,

kadiri ifaavyo, yale walichojifunza katika ujirani anakoishi yeye ambayo yangeweza kuwa yenye msaada kwao katika kuamua hatua zao zinazofuata.

4. Kampeni itaanza hivi karibuni katika ujirani ili kuwaleta vijana wengi zaidi na zaidi katika mazungumzo kuhusu jinsi wanavyoweza kukuza vipaji na uwezo wao na kuchangia kwenye uboreshaji wa jumuiya zao. Wale wanaoonesha shauku watakaribishwa kusoma kozi za taasisi ili kujenga uwezo wao kwa ajili ya huduma. Washiriki wote katika kampeni wamegawanywa katika timu za wawili wawili. Katika timu moja, mtu mwenye uzoefu mkubwa anaungana na mtu mwenye uzoefu mdogo ambaye bado anahitaji kujenga ujasiri na kujiamini ugani. Ni lipi kati ya yafautayo huonesha utovu wa kiburi kwa upande wa mjumbe huyo wa timu mwenye uzoefu zaidi?

_____ Humkatiza mara kwa mara mjumbe mwenye uzoefu mdogo kila anapojaribu kuongea na vijana na hatimaye anayatawala mazungumzo yote.

_____ Humwachia mjumbe mwenye uzoefu mdogo azungumze zaidi wakati wa mazungumzo na vijana, wakati huo akinukuu makosa anayofikiri yanafanyika, ili aweze kuongea naye baadaye kuhusu kasoro zake na kumfundisha jinsi mazungumzo yanavyopaswa kufanyika.

_____ Kuanzisha sehemu kubwa ya mazungumzo lakini mara moja anamwachia mjumbe mwingine azungumze, akimsaidia kadiri anavyoendelea kujiamini katika kuzungumza na vijana.

## SEHEMU YA 12

Katika sehemu zilizopita tumechunguza unyenyekevu kwa namna mbili, kama sifa ambayo huyapa mazungumzo yetu ushawishi, na hutulinda dhidi ya mitego tunayoweza kukutana nayo katika jitihada zetu za kukua kiroho. Bado kuna mchango mwingine muhimu ambao unyenyekevu huufanya kwenye maisha yetu ambao hasa unahusiana na ufundishaji. Unyenyekevu hutuwezesha kuyaendea yote tuyafanyayo, hususan jitihada zetu katika huduma kwa Hoja kwa mwelekeo wa kujifunza. Bila mwelekeo huu, tunaelekea kuwa vipofu kwa ujinga wetu wenyewe na kuamini kwamba tunajua kile ambacho hatukijui. Tabia istahiliyo sifa kabisa ya wale watembeao kwa unyenyekevu katika njia ya Mungu ni utayari wao wa kujifunza.

Kwa nini, tunaweza kuuliza, kuwa na mwelekeo wa wazi wa kujifunza ni muhimu sana kwetu sisi ambao tunatamani kufundisha Hoja ipasavyo? Ili kujibu swali hili, tafakari juu ya kile unachokijua kuhusu ufundishaji. Je, unajua wakati wote mbinu inayofaa kabisa ya ufundishaji unayopaswa kuitumia? Je, unajua unachopaswa kusema na jinsi ya kukisema katika kila hali inayojitokeza kwako? Je, unafikiri inawezekana kujifunza katika kozi moja au mbili yale yote unayohitaji kuyajua kuhusu kitendo kitakatifu kabisa? Je, ufundishaji unaweza kufupishwa hadi kwenye fomyula? Kwa hakika unakubali kwamba jibu kwa maswali haya ni “hapana” na kwamba njia pekee ifaayo katika kuongeza ufanisi wa mtu katika ufundishaji ni kujitwalia hali ya ujifunzaji.

Kadri tunavyojitahidi kufundisha Hoja kwa ufanisi zaidi na zaidi tunapaswa kuwa waangalifu tusiingie katika mtego wa kubishana na wengine kwenye jumuiya juu ya mbinu na

njia za ufundishaji. Tusipokuwa waangalifu, tunaweza kuingia kwa urahisi katika mabishano ya aina hii, kila mmoja wetu akiamini kwamba tumegundua fomyula sahihi na kwamba, vinginevyo ufundishaji ufanyike katika njia yetu, "mafanikio" hayawezekani.

Tunaweza kuepukana na mwenendo kama huo tunapotambua kwamba ufundishaji wa Hoja ni jambo ambalo mtu sharti ajifunze. Tunajikomboa wenyewe kutoka vizuizi tunavyojiwekea wenyewe pale tunapoona katika kila jitihada ya ufundishaji fursa ya kujipatia umaizi na kuongeza uelewa wetu wa nguvu husika za kiroho. Majadiliano yetu na Wabahá'í wenzetu huwa na manufaa zaidi pale tunapobadilishana mawazo, tunaposhirikishana tajiriba na kuchanganua sababu zinazochangia mafanikio ya ufundishaji wenye ufanisi. Kila mmoja wetu anahamasishwa

> **"kutafakari kipindi hadi kipindi juu ya njia zifaazo za kufundisha Imani katika mazingira yao. . . Roho ambazo zimepewa baraka ya imani zina shauku ya asili kushiriki zawadi hii na ndugu, marafiki, wanafunzi wenza, wafanyakazi wenza, na wale ambao hawakuwa wamekutana nao kabla, kupitia mazungumzo wakitafuta kila mahali na kila wakati sikio sikivu. Mazingira na hali tofauti tofauti huchangia zenyewe kwenye mbinu tofauti, na marafiki wanapaswa kujishughulisha katika mchakato unaoendelea wa ujifunzaji kuhusu kile kinachofaa zaidi mahali walipo."[22]**

Soma hali zilizowasilishwa hapo chini. Ungeitikiaje kwa kila moja kama unaamua kuona kila jitihada ya ufundishaji kuwa fursa ya kujifunza?

1. Unaamua kufanya mkutano wa kila juma nyumbani kwako kujadili Imani. Unaamua kuwaalika takribani watu kumi ambao, katika matukio tofauti tofauti, walionesha shauku. Kwa kila mkutano, unachagua mada fulani na kuandaa na kutoa mazungumzo mafupi juu yake, baada ya hapo unafungua mkutano kwa ajili ya maswali. Halafu mnakuwa na kipindi cha ukarimu ambapo mnasalimiana na kufahamiana zaidi na kuimba nyimbo. Baada ya majuma machache, ni watu wawili tu ambao bado wanaendelea kuja. Unaamua:

   _____ Unahitaji kuifanya mikutano hiyo ya kuburudisha na changamani zaidi.

   _____ Unapaswa kuachana na mikutano hiyo ya kila juma katika mipango yako ya ufundishaji; halikuwa wazo zuri hata hivyo.

   _____ Unapaswa ujaribu muundo tofauti katika mikutano michache ijayo, labda kujifunza pamoja na wageni wako nukuu chache juu ya mada maalum, ukiwaruhusu kulifahamu Neno Takatifu, na kisha kujenga juu ya tajiriba hiyo.

   _____ Unapaswa kuwatafuta wale wote ambao hawaji tena na kuwauliza kwa nini waliacha kuhudhuria mikutano hiyo.

2. Ulipokuwa unajifunza kuhusu Imani, kulikuwa na kanuni chache ambazo zilikugusa zaidi: kwa hiyo sasa unahisi kuwa njia bora ya kufundisha watu ni kuwawasilishia kanuni hizo hizo. Hata hivyo, kwa jumla, unabaini kwamba watu unaoongea nao hawavutiwi na mawazo unayoeleza. Unaamua:

_____ Unahitaji mazoezi zaidi katika uwasilishaji wa kanuni hizi.

_____ Unapaswa kuwatafuta watu walio kama wewe mwenyewe na kuwafundisha wao tu.

_____ Wewe kiasili siyo mwalimu na unapaswa kuhudumia Imani katika njia nyingine.

_____ Unapaswa ujaribu, katika siku zijazo, kuelewa masuala yanayoshughulisha akili za wale unaokutana nao, na kuingiza mafundiso husika ya Imani katika mazungumzo yako pamoja nao.

3. Wewe ni sehemu ya timu ambayo imeamua kuelekeza jitihada zake juu ya kundi maalum na kushiriki nao ujumbe wa Bahá'u'lláh. Baada ya muda kidogo, unatanabahi kutokana na maswali wanayouliza kwamba wote wanaonekana kuwa na ugumu kwa dhana iliyoenea kuhusu Mungu. Timu inaamua:

_____ Ni bora kutoongelea kuhusu mada hii. Ikiwa watu wanaanza kuongelea mada hii katika maongezi yenu, wewe mara moja unaongelea mada nyingine.

_____ Watu ambao wana ugumu na dhana ya Mungu siyo wapokevu kwa Imani, hivyo haupaswi kupoteza muda kujaribu kuwafundisha.

_____ Utamuomba mtu mwenye tajiriba zaidi aambatane nawe na aongee na wale unaowatembelea kuhusu uwepo wa Mungu. Kama hilo halifanikiwi, basi utawaacha na hutawang'ang'aniza zaidi.

_____ Baada ya kusoma baadhi ya vifungu husika kutoka maandiko, timu yako itaandaa pamoja tamko fupi kuwasaidia wale unaowatembelea kuelewa kile ambacho Bahá'u'lláh anatufundisha kuhusu Mungu. Utasikiliza mwitikio wao, utatafakari juu ya matokeo yake, na kurudi kwenye Maandiko kwa ajili ya kutafuta majibu ya maswali yaliyoibuka, na kurekebisha tamko lako kufuatana na umaizi ambao timu imeupata kutoka tajiriba na vifungu mlivyojifunza pamoja. Utaendelea kufanya hivi hadi jitihada zako zitakapoanza kuleta matokeo yanayoridhisha.

4. Wewe ni sehemu ya timu ambayo imeshiriki katika kampeni kadhaa za ufundishaji zenye ufanisi mkubwa katika ujirani mmoja. Idadi ya kutosha ya familia zimekubali Hoja. Ukitambua jinsi ilivyo muhimu kwa wao kujiongezea ujuzi wao wa Imani, timu yako imetembelea takriban kaya zao zote mara kwa mara na kujadili mada zilizoongelewa katika kitengo cha tatu cha Kitabu cha 2 pamoja na wana-kaya. Timu sasa inajiuliza jinsi ya kusonga mbele kwa namna ambayo itafanya yote mawili, kuongeza dhamira yao kwa Imani na kuwawezesha kushiriki mafundisho ya Bahá'u'lláh na wengine. Timu inaamua:

_____ Mtaandaa pamoja orodha ya hotuba thelathini juu ya mada tofauti tofauti na kuwasilisha mada mpya kwa kila ziara, mkifuatalia orodha yenu kwa uaminifu kuhakikisha mnamaliza mada zote mlizochagua.

_____ Utaipa kila familia kitabu kidogo kuhusu Imani na kuwaomba wasome idadi kadhaa ya kurasa hadi mtakapokutana tena. Wakati wa ziara yako, hivyo, utajadiliana nao juu ya maswali yoyote waliyo nayo.

_____ Una wasiwasi kuhusu kutumia mbinu ambayo itachukua muda mrefu sana. Hivyo, badala ya kuendelea kuzitembelea familia moja moja, utawakaribisha kwenye mkutano wa kila juma nyumbani kwa mtu mmoja kujadili Imani. "Wale ambao kweli wana shauku ya kujifunza watakuja," mnaambizana.

_____ Utafikiria juu ya mada moja ya msingi inayohusiana na Imani ambayo wao wangependa kujifunza zaidi na utatafuta vifungu vinavyohusiana na mada katika maandiko. Halafu utaitembelea familia mojawapo kushiriki vifungu ulivyovichagua na kujadiliana mawazo pamoja nao. Baadaye, utatafakari juu ya matokeo ya mkutano huo, utarejelea kwenye maandiko, utarekebisha vifungu ikibidi, na kutumia teuzi lililopitiwa upya katika ziara kwa familia nyingine. wakati huo huo, kutokana na maoni yaliyotolewa katika ziara kwa familia ya kwanza, utachagua seti nyingine ya mawazo na vifungu ili kusoma pamoja nao katika ziara yako ya pili. Utaendelea kwa namna hii hadi utakapokuwa umeanzisha ruwaza ya ziara za mara kwa mara zilizojikita kuzungukia mlolongo wa mada. Wakati huo huo, utachunguza pamoja na familia jinsi mada hizo hizo zingeweza kujadiliwa na majirani, ndugu na marafiki zao.

## SEHEMU YA 13

Mazoezi katika sehemu iliyotangulia yalitusaidia kuona, iwe tunajihusisha katika jitihada za ufundishaji binafsi au katika juhudi za pamoja, jinsi maswali muhimu yanavyoibuka kadiri tunavyotenda na kutafakari juu ya matokeo ya vitendo vyetu. Seti moja ya maswali yatakayoibuka mara kwa mara wakati tunapochukua mwelekeo wa ujifunzaji unahusu jinsi tunavyouendea ufundishaji na mielekeo ya kudumisha katika kutekeleza kitendo hiki kitakatifu. Je, tuwe washupavu sana? Je, tuwe wenye hadhari na wahafidhina? Je, tutoe Ujumbe wa Bahá'u'lláh mara moja kwa kila mtu tunayekutana naye au tubague? Je, tuongelee juu ya Imani moja kwa moja kama dini ya jamii ya wanadamu kwa wakati huu, au tuyakite mazungumzo yetu kwenye majadiliano ya jumla juu ya kanuni ambazo zinakubaliwa na watu kwa urahisi? Je, tuvitaje vile vipengele vya mafundisho ambavyo tunajua vitakuwa changamoto kwa msikilizaji, au tuache mada hizo kwa ajili ya baadaye, baada ya mtu kukubali Imani? Ili kuwa wenye ushawishi, je, tuufanye uwasilishaji wetu mzito na wa kuelemea, au tuzungumze kwa shauku ndogo kadiri iwezekanavyo?

Katika kifungu cha hapo chini, Mlinzi anatupa ushauri wenye thamani sana katika hili. Baadhi ya maneno yanaweza kuwa mageni kwenu, hivyo kabla hamjajifunza nukuu hiyo, pengine mngependa kupitia upya orodha ifuatayo ya maana zao:

| | |
|---|---|
| A uchokozi: | Kusababisha hasira au mtafaruku mkubwa |
| A utepetevu: | Goigoi |
| A kushupaa: | Kujawa na shauku iliyokithiri au yenye makosa |
| A kukithiri: | Zaidi ya kawaida au istahiliyo |

| | |
|---|---|
| Huru: | Enye mawazo mapana na huru; siyewekewa mipaka na mila au kanuni |
| Ufasiri: | Maelezo ya maana au kusudi; uwasilishaji wa mada |
| A hadhari: | Angalifu |
| Suluhifu: | A kuridhia kupatanishiwa |
| Mlei: | Mtu asiye na utaalam wa kikasisi |
| A kudharau: | Kuonesha utovu wa heshima au kiburi; kebehi |
| Chonga: | Punguza kidogo kidogo |
| Toa: | Kutoa ili ikubaliwe; toa zawadi |
| Asiyeridhiana: | Asiyefanya au kuruhusu maafikiano; asiyeshindwa; thabiti |

Sasa soma nukuu kutoka maandiko ya Mlinzi:

> **"Lazima wasiwe wachokozi wala watepetevu, wenye kushupaa wala wenye uhuru uliokithiri, katika ufasiri wao wa mambo ya kimsingi na bainifu ya Imani yao. Lazima wawe wenye hadhari au jasiri, lazima watende kwa haraka au kwa subira, lazima watumie njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, lazima wawe washindani au wasuluhifu, kwa kulingana kabisa na upokevu wa kiroho wa roho wanayokutana nayo, awe sharifu au mtwana, wa kaskazini au kusini, mlei au kasisi, bepari au mjamaa, mtawala au mwana-mfalme, fundi mchundo au ombaomba. Katika uwasilishaji wao wa Ujumbe wa Bahá'u'lláh wasisite wala kukawia. Wasiwe wenye dharau kwa maskini wala waoga mbele ya wakuu. Katika ufasiri wao wa kanuni zake wasisisitize mno wala kuuchongachonga ukweli ambao wao wanautetea, iwe msikilizaji wao ni mfalme, au akiwa mkuu wa kanisa, au mwana-siasa, au mchuuzi, au mtu wa mtaani. Kwa wote kadhalika, wakubwa au wadogo, tajiri au maskini, lazima watoe, kwa mikono ya wazi, kwa moyo mwangavu, kwa ulimi wenye ufasaha, kwa uvumilivu usio na kikomo, kwa utiifu usioridhiana, kwa hekima kuu, kwa ujasiri usiotikisika, Kikombe cha Wokovu katika wakati wa hatari mno kama hu . . ."[23]**

1. Shoghi Effendi hutuambia kwamba, tunapofundisha Hoja, sharti tusiwe ________________________ wala _______________ katika ______________________ wa mambo ya ______________________ na __________________________ ya Imani.

2. Tusiwe _____________________ wala ________________________ katika ufasiri wetu.

3. Lazima tuwe wenye _________________ au ________________, lazima tutende ________________ au _______________, lazima tutumie njia ya ________________ au _______________, lazima tuwe ______________________ au ____________________ kwa kulingana kabisa na ___________________________ wa roho tutakayokutana nayo.

4. Tunapofundisha Hoja, lazima tutende kwa __________________________ kabisa na _________________________________ wa roho tutakayokutana nayo, awe sharifu au _________________________, wa kaskazini au _______________________, mlei au

________________ , bepari au ________________ , mtawala au ________________ , fundi mchundo au ___________________ .

5. Katika kuwasilisha Imani tusi ____________________ wala ____________ .

6. Tusiwe _____________________ kwa masikini wala _________________ mbele ya wakuu.

7. Katika ufasiri wetu wa kanuni za Imani, tusi ________________ wala ______________ ukweli ambao tunautetea, iwe msikilizaji wetu ni ______________ , au ___________________ , au _______________ , au ______________________ , au _______________________________ .

8. Kwa wote kadhalika, lazima tutoe kwa mikono ya _____________ kwa moyo __________________ , kwa ulimi ________________ , kwa uvumilivu ___________________ , kwa utiifu ____________________ , kwa hekima _________________ , kwa ujasiri _______________________ , Kikombe cha Wokovu katika wa hatari mno kama huo.

## SEHEMU YA 14

Sasa hebu tuchunguze nukuu hiyo hapo juu kwa ukaribu zaidi na kujaribu kugundua baadhi ya athari zake katika vitendo.

1. Nukuu hiyo inatuambia kwamba tufundishapo Hoja, tusiwe wachokozi katika uwasilishaji wetu. Hapo chini kuna hali chache. Weka “U” mbele ya zile hali ambamo uwasilishaji wako ni wa uchokozi.

_____ Ili kumuonesha muumini mcha Mungu wa Imani nyingine kwamba jamii ya wanadamu ina uhitaji wa Mdhihirishaji mpya, unaanza uwasilishaji wako kwa kumuonesha mambo yote yale ambayo ni makosa katika dini yake.

_____ Unamueleza muumini mcha Mungu wa Imani nyingine kwamba Wadhihirishaji wa Mungu ni kama vioo vinavyoakisi mwangaza wa jua. Wao huakisi sifa za Mungu na kufunua sifa Zake takatifu. Ingawa Vioo vyaweza kutofautiana, vyote huakisi Mwangaza wa Jua lile lile. Kwa namna hii, pole pole unamsaidia kufahamu kwamba kumkubali Bahá’u’lláh hakumaanishi kuwakataa Wadhihirishaji waliokuja kabla Yake.

_____ Unamfundisha mtu ambaye hana hakika kama anamuamini Mungu. Unaanza kwa kumwambia kwamba Bahá’u’lláh ni Mdhihirishaji Mkuu Kabisa wa Mungu.

_____ Kikundi kidogo kimekusanyika nyumbani kwako. Wengi wale waliopo bado hawajaonesha shauku yoyote ya kutosha katika Imani na unajaribu kutambulisha mafundisho kwao kwa namna ambayo itavutia umakinifu wao. Katika majadiliano yenu unasema kwa msisitizo kwamba, siku zijazo, kila mtu atakuwa Mbahá'í.

_____ Unaanza uwasilishaji wako kwa mtu ambaye ana starehe zote za maisha kwa kusema kwamba utajiri ni utando kati ya mtu na Mungu.

_____ Unakutana na kasisi ambaye anavutiwa hasa kujifunza juu ya Imani na anakuomba umuelezee baadhi ya mafundisho ya Bahá'u'lláh. Jambo la kwanza unalomwambia ni kwamba, katika Zama hizi, Mungu amekomesha ukasisi.

2. Tunapofundisha Hoja, tusiwe watepetevu. Ni ipi kati ya hali zipi zifuatazo unakuwa goigoi mno. Ziwekee alama ya "T".

_____ Mtu mmoja anakuuliza ni nini hasa cha kipekee kuhusu Imani ya Kibahá'í. Unajibu: "Imani ya Kibahá'í ni kama dini zingine zote. Kiini chake ni kuwa mwema na kupendana."

_____ Mbinu yako ya kuwafundisha wengine ni kujaribu kuwaonesha kwamba Imani ya Kibahá'í ni mkusanyiko wa kanuni njema ambazo kila mtu anaweza kuzikubali. "Usimamishaji wa amani," unasema, kwa mfano, "nani asiyeamini katika hilo?" Pindi wanapovutiwa na Imani kwa njia hii, unaachana nao, wakati mwingine ukiwaambia kwamba wanaweza kupata kitabu cha kusoma kama wakipenda. Hivyo ndivyo daima wewe hufanya.

_____ Mtu mmoja ambaye yupo karibu kuikubali Imani anakuuliza juu ya fedha na michango. Jibu lako lote ni, "hakika, kama kila kitu maishani, kiasi cha fedha kinahitajika kwa ajili ya kuendeshea mambo. Lakini utachangia tu kama ukitaka."

_____ Mtu mmoja ambaye yupo karibu kuikubali Imani anakuuliza juu ya fedha na michango. Wewe unamuambia kwamba uchangiaji kwenye mifuko ya Akiba ya Imani ni wajibu mtakatifu wa kila muumini na unamuelezea umuhimu wa kiroho wa kujitoa dhabihu, ambao humaanisha kuachilia kile kilicho duni zaidi na kupokea kile kilicho bora zaidi. "Uchangiaji kwenye mifuko", unasema, "ni sehemu muhimu ya kazi yetu ya kujenga ulimwengu bora zaidi."

_____ Rafiki mmoja ambaye amekuwa akijifunza Imani kwa kipindi sasa hukuomba umuelezee dhana ya Agano la Milele. Wewe unasema kwamba ni jambo rahisi sana: "Kuna mapatano kati ya Mungu na wanadamu. Kutoka wakati hadi wakati, Yeye humtuma Mdhihirishaji Wake, na sisi tunamtambua Yeye na kujaribu kwa uwezo wetu wote kufanya yale asemayo."

_____ Rafiki mmoja ambaye amekuwa akijifunza Imani kwa kipindi sasa hukuomba umuelezee dhana ya Agano la Milele. Wewe unasema kwa kifupi kwamba, baada ya kuwaumba wanadamu kutokana na upendo Wake kwetu, Mungu ameahidi kamwe hatatuacha peke yetu bali angeifanya Amri na Kusudi Lake

vijulikane kwetu wakati hadi wakati kupitia Wadhihirishaji Wake; na sisi, badala yake, tunaahidi kumtambua Mdhihirishaji wa Siku yetu na kufuata mafundisho Yake.

3. Tufundishapo Hoja, tusiwe wenye kushupaa katika uwasilishaji wetu. Hapo chini kuna hali kadhaa. Weka " S" kando ya zile ambamo uwasilishaji wako ni wa kushupaa.

_____ Mtu mmoja ambaye anaichunguza Imani anakuuliza nini maana ya kuwa Mbahá'í. Wewe unamuambia kwamba kuwa Mbahá'í si jambo dogo. "Lazima utoe kila kitu kwa ajili ya Imani," unaeleza. "Ni kusuka au kunyoa."

_____ Unaanzisha mkutano nyumbani kwako na watu wachache ambao wamekuja kwa mara ya kwanza kusikiliza juu ya Imani kwa kuwaomba washikane mikono na kuimba "Alláh-u-Abhá".

_____ Unaanza kumfundisha muumini thabiti wa imani nyingine kwa kumwambia kwamba wakati wa dini yake umepita na umekwisha. Anapaswa aachane dini yake. "Bahá'u'lláh, Mjumbe wa Mungu kwa siku ya leo, amekuja," unamwambia. "Unapaswa kutupilia mbali yaliyopita".

_____ Unamuelezea Imani mtu mmoja. Yeye hakubaliani na hoja mojawapo uliyotoa. Unaanza kubishana naye ukisema kwamba utamuonesha kutoka Maandiko matakatifu ya dini yake kwamba yeye amekosea.

_____ Unamuelezea Imani mtu mmoja. Yeye hakubaliani na hoja mojawapo uliyotoa. Unaweza kuona kwamba yeye ametekwa sana na hisia kali juu ya somo hilo. Unatambua wasi wasi wake na kusema: "Tunaweza kujadiliana hoja hii maalum siku nyingine kama unapenda. Lakini kuna mambo mengi mno ambayo tunakubaliana. Kwa leo hebu tuyachunguze mambo hayo pamoja."

_____ Unaelezea sheria za Imani kwa rafiki mmoja. "Utii wa sheria za Mungu ndio kiini cha dini," unasema. "Sababu ya ulimwengu kuwa katika hali mbaya mno hivi leo ni kwamba jamii ya wanadamu haifuati sheria za Bahá'u'lláh. Kila mtu ambaye hafuati sheria Zake atahukumiwa katika ulimwengu ujao."

_____ Unaelezea sheria za Imani kwa rafiki mmoja. "Bahá'u'lláh anatuambia kwamba sheria Zake ni taa za majaliwa Yake yenye upendo," unasema. "Sheria Zake huangazia njia yetu na kutuongoza kwenye furaha ya kweli. Hata hivyo, sisi siyo wakamilifu na wakati mwingine tunafanya makosa. Lakini tunapomkubali Bahá'u'lláh, na kadiri tunavyosali Kwake, Yeye Mwenyewe hutusaidia kushinda udhaifu wetu na hutupa nguvu kutii sheria Zake."

4. Wakati tufundishapo Imani, sharti tusiwe wenye uhuru uliokukithiri. Amua ni zipi kati ya hali zifuatazo unakuwa mwenye uhuru mno. Ziwekee alama "H.

_____ Mtu mmoja ambaye anaichunguza Imani anakuuliza kama kuna viongozi wowote katika jumuiya ya Kibahá'í. Wewe unajibu: "Sisi hatuna mapadri wala makasisi ambao huja kati yetu na Mungu. Sote tunaishi kulingana na dhamiri yetu wenyewe. Hakuna mtu anayetuambia nini cha kufanya."

_____ Mtu mmoja ambaye anaichunguza Imani anakuuliza kama kuna viongozi wowote katika jumuiya ya Kibahá'í. Wewe unaeleza: "Jumuiya huendesha mambo yake kupitia mfumo wa kiutawala wa ulimwengu mzima, ambao hujumuisha halmashauri kwenye ngazi za kitaifa na mahali ziitwazo Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na ya Mahali. Halmashauri hizi huchaguliwa bila kugombea wala kufanya kampeni na katika mazingira matakatifu ya sala. Pia kuna kikundi cha waumini mashuhuri ambao huteuliwa kuwa washauri kwa Mabaraza haya na kuwatia moyo na kuwahimiza waumini wenzao. Asasi zote hizi zipo chini ya chombo cha kimataifa cha utawala cha Imani ya Kibahá'í kiitwacho Nyumba ya Haki ya Ulimwengu."

_____ Mtu mmoja ambaye unamfundisha Imani anakuuliza jinsi ambavyo mtu anatarajiwa kujihusisha na utawala wa Kibahá'í. Wewe unajibu: "Vyema, unajua, Imani ya Kibahá'í lazima iwe na mfumo fulani wa utawala, hivyo tuna kitu kinachoitwa Mabaraza ya Kiroho yenye wajumbe tisa kila moja. Vyombo hivi vya kuchaguliwa, husimamia masuala ya Imani katika ngazi ya mahali na ya kitaifa, lakini unapaswa tu kuyatii kadiri utambuzi wako unavyokuamuru."

_____ Unamfundisha mtu mmoja Imani nay eye anasema kwamba anapenda kila kitu alichosikia isipokuwa kwamba Wabahá'í hawaamini katika ufufuko. Wewe unasema; "Hilo ni sahihi kabisa kwa kuwa Wabahá'í huamini katika umoja katika anuwai. Hiyo humaanisha anuwai ya fikra pia."

_____ Mtu mmoja anakuuliza jinsi Wabahá'í wanavyoeneza Imani yao. Wewe unasema tu kwamba Wabahá'í hawawashawishi watu kubadili dini. "Sisi 'tunaishi tu maisha' na watu wanapotuuliza maswali, tunawaeleza kuhusu Imani."

_____ Mtu mmoja ambaye amesoma kuhusu Imani na ameonesha shauku kwayo, anakuomba kuelezea kile kinachohitajika kwa wale wanaojiandikisha katika jumuiya ya Kibahá'í. "Dini ni jambo binafsi," wewe unasema. "Ni njia ya maisha. Ni kitu ambacho unaweza kukihisi tu moyoni mwako. Katika Imani ya Kibahá'í, bila shaka kuna sheria chache, lakini unahitaji kuzitii tu kadiri dhamiri yako inavyokuamuru."

_____ Mtu mmoja ambaye amesoma kuhusu Imani na ameonesha shauku kwayo, anakuomba kuelezea kile kinachohitajika kwa wale wanaojiandikisha katika jumuiya ya Kibahá'í. Wewe unajibu: "Kiini cha dini ni kumjua Mungu kupitia Mdhihirishaji Wake, kuendelea kuwa thabiti katika upendo Wake, na kufuata mafundisho Yake. Upendo wetu kwa Mungu unafika hadi kwenye muumbo Wake; tunaipenda jamii ya wanadamu na tunatimiza wajibu wetu kwa Imani kwa kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa jamii."

_____ Unaongea na baadhi ya marafiki juu ya mada ya elimu ya watoto. Halafu unasema: "Imani ya Kibahá'í hufundisha kwamba watoto huzaliwa wema na, ukiwapenda na kuwasaidia kukuza kile ambacho Mungu amekiweka ndani mwao, watakuwa vizuri."

_____ Unaongea na baadhi ya marafiki juu ya mada ya elimu ya watoto. Halafu unasema: "Imani ya Kibahá'í hutuambia kwamba watoto wana uwezo wa

kuwa wema, lakini pia wana mielekeo ambayo lazima idhibitiwe. Wanahitaji elimu ili waweze kufuata njia iliyo sahihi na kukuza uwezo mkubwa ambao kwao kila mmoja amejaliwa.”

5. Amua ni yapi kati ya majibu yafuatayo yangekuwa ya kufaa kwa kila moja ya hali za hapo chini, wakati unapojaribu kuamua namna ya kuuendea ufundishaji wa Imani. Chaguo moja au zaidi linaweza kuhusika katika kila hal.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | Kuwa mwenye hadhari | e. | Kutumia njia ya moja kwa moja |
| b. | Kuwa shupavu | f. | Kutumia njia isiyo ya moja kwa moja |
| c. | Kutenda kwa haraka sana | g. | Kuwa washindani |
| d. | Kuwa na subira | h. | Kuwa wasuluhifu |

__________ Mwanamke mmoja anakuja Bahá’í Senta akiwa amesisimka sana. Anasema kwamba amesoma kitu fulani mtandaoni juu ya Imani na anataka kujua zaidi juu ya Bahá’u’lláh. Anaelezea kwamba wakati wote alihisi ndani kabisa ya moyo wake kwamba Mungu kamwe asingeitelekeza jamii ya wanadamu na kwamba Yeye angetutumia Mdhihirishaji mwingine.

__________ Wewe na familia yako mmehamia katika kijiji ambako hamfahamiani na yeyote. Siku moja, muda mfupi baada ya kuwasili kwenu, jirani yenu anakuja nyumbani kwenu kuwakaribisha na anajitambulisha mwenyewe. Katika kufanya hivyo, anaweka wazi kwamba wana-kijiji wote wa kijiji hicho wameunganika sana katika dini yao na kwamba hawataki jinsi hizi dini “zingine” zinavyokuja na kuwatenganisha watu

__________ Wewe na familia yako mmehamia katika kijiji ambako hamfahamiani na yeyote. Siku moja, muda mfupi baada ya kuwasili kwenu, jirani yenu anakuja nyumbani kwenu kuwakaribisha na anajitambulisha mwenyewe. Yeye anaviona baadhi ya vitabu vya Kibahá’í mezani na anakuuliza, “Imani ya Kibahá’í ni nini?”

__________ Umejiunga na shirika moja la watu wanaopenda kuendeleza amani. Mtu mmoja kati yao anayevutiwa hususan na mawazo unayooyaeleza katika mikutano anaamini kabisa kwamba njia pekee ya kupata mabadiliko yenye maana katika jamii ni kupitia hatua za kizalendo za kisiasa. Yeye anahakikisha anaongea na wewe kila wakati shirika linapokutano.

__________ Mmoja wa watu unaofanya nao kazi amekuambia mara kadhaa kwamba yeye haamini katika Mungu. Lakini anavutiwa na mawazo mengi unayoelezea kuhusiana na masuala ya kijamii, kwa mfano, usawa wa wanawake na wanaume na haja ya elimu kwa watu wote.

__________ Kwenye mkutano wa kijiji uliohudhuriwa na machifu kadhaa wa eneo hilo, unatoa baaadhi ya mawazo juu ya elimu ya watoto. Baadaye, mmoja wa machifu wa kijiji hicho anakuja kuzungumza na wewe. Anasema kwamba anajua wewe ni Mbahá’í na amependa mengi ya mapendekezo uliyoyatoa. Amevutiwa kujifunza zaidi kuhusu Imani.

__________ Rafiki mmoja aliyejiunga na jumuiya hivi karibuni anakupeleka nyumbani kwake kukutana na familia yake. Wao wanampinga kwa kuwa kwake Mbahá'í na wanajaribu kumfanya aachane na Imani.

__________ Rafiki mmoja aliyejiunga na jumuiya hivi karibuni anakupeleka nyumbani kwake kukutana na familia yake. Anakuambia kwamba wao wote wamesisimka sana juu ya Imani na wanataka kusikia zaidi.

6. Jaribu kufikiria ni mielekeo ipi inaweza kuwepo, na sifa zipi za kiroho zinakosekana, ikiwa mtu

– anawabeza masikini: ________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

– ni mwoga mbele ya wakuu: ____________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

7. Toa mfano wa jinsi, wakati wa kuelezea kweli za Imani, mtu anaweza.

– kusisitiza kupindukia juu ya ukweli: ______________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

– kuuchongachonga ukweli: _____________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

## SEHEMU YA 15

Mwongozo ufuatao kutoka kwa Mlinzi hutukumbusha kwamba, kama ilivyo katika mambo yote, tunapaswa tumuangilie 'Abdu'l-Bahá tunapojaribu kuamua mbinu ifaayo zaidi ya ufundishaji katika hali yoyote:

> **"Hebu vile vile tukumbuke mfano ambao Bwana wetu mpendwa ameuweka wazi mbele yetu. Mwenye hekima na busara katika mbinu Zake, aliye macho na mwangalifu katika maongezi Yake ya mwanzoni, mvumilivu na mkarimu katika matamshi Yake yote ya hadhara, mwenye hadhari na mtaratibu katika ukunjuaji wa kanuni muhimu za Hoja, mwenye shauku katika kusihi Kwake, lakini makini katika hoja, jasiri katika toni, thabiti katika imani, mwenye heshima katika mwenendo**

**Wake—hizo ndizo zilivyokuwa sifa bainifu za uwasilishaji bora wa Mpendwa wetu wa Hoja ya Bahá'u'lláh."**[24]

1. Kadiri unavyojitahidi kufuata mfano wa 'Abdu'l-Bahá, utajitahidi kuwa namna gani katika mbinu yako ya ufundishaji? ____________________

2. Utajaribu kuwa namna gani unapokutana na mtu kwa mara ya kwanza? ____________________

3. Nini kitayaainisha maneno yako kuhusu Imani utakapoongea hadharani? ____________________

4. Utawafahamishaje watu juu ya ukweli wa Hoja? ____________________

5. Utajaribu kuwa mtu wa namna gani:

   – Katika kusihi kwako? ____________________

   – Katika hoja yako? ____________________

   – Katika toni yako? ____________________

   – Katika imani yako? ____________________

   – Katika mwenendo wako? ____________________

Sasa kariri nukuu hiyo hapo juu.

## SEHEMU YA 16

Tulianza kitengo hiki kwa kujikumbusha kwamba "kuwa" na "utendaji" ni vipengele viwili vinavyokamilishana na visivyowez kutenganishika vya maisha ya kiroho. Hafalu tulizitenga sehemu kadhaa kwa ajili ya kuchunguza baadhi ya sifa za kiroho ambazo lazima sote tujitahidi kuzikuza kadiri tunavyojishughulisha na shughuli ya mara kwa mara na yenye mpangilio. Majadiliano yetu juu ya unyenyekevu yalituongoza kufikiria juu ya mwelekeo wa ujifunzaji ambao ni muhimu sana wakati wa kufundisha Imani. Pia tulipata umaizi juu ya jinsi mielekeo mingine inavyoweza kuathiri namna tunavyouendea ufundishaji. Hebu sasa twende hatua moja zaidi na tuchunguze asili ya uhusiano wetu na wale tunaowafundisha. Uhusiano huu unapaswa uwe wa namna gani? Je, maandiko yanatuambia nini kuhusu jambo hili?

Dhana ya kwanza ambayo yumkini huja akilini ni undugu. Kwa udhahiri, katika muktadha wa jitihada za ufundishaji za mtu binafsi, uwezo wa kuanzisha mafundo ya urafiki na watu ni wa lazima. Uwezo huu huu pia ni wa muhimu sana katika ushiriki wetu katika kampeni ya pamoja—kwa mfano, tunapowaalika vijana kusoma kozi za taasisi kama njia ya kuongeza uwezo wao kwa ajili ya huduma, tunapokuwa tunaunda madarasa mapya kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto na vikundi kwa ajili ya uwezeshaji kiroho wa vijana chipukizi,

tunapozitembelea kaya za wale waliojiunga hivi karibuni katika Imani katika ujirani na vijiji vyetu na kuchunguza mada mbalimbali pamoja nao, na tunapojishughulisha na jitihada za ufundishaji wa moja kwa moja miongoni mwa makundi pokevu kwa ujumbe wa Bahá'u'lláh. Katika hali zote hizo, uwezo wetu wa kuanzisha uhusiano wenye upendo hutuamulia jinsi tutakavyowaendea wale tunaokutana nao, namna tunavyowailiana nao, na kama tunaweza kuigusa mioyo yao.

Swali ambalo tunahitaji kujiuliza ni namna ya kukuza uwezo huu wa lazima. Hulka zetu, bila shaka, ni tofauti. Baadhi yetu, ama kama matokeo ya malezi yetu au mwelekeo wa kiasili, huona vyepesi kupata marafiki. Baadhi wanaweza kuanza mazungumzo na watu wasiowajua kabisa. Wengine wana aibu na huliona jambo hili kama changamoto.. Hata hivyo, haidhuru tabia yetu ilivyo, sharti tutambue kwamba kupitia jitihada yenye dhamiri, tunaweza kujifunza kuandamana na watu kwa moyo wa undugu. Maandiko hutoa ushauri mwingi na wa thamani juu ya mada hili, mifano michache tu ya ushauri huo imetolewa hapo chini. Vifungu vya maneno vinavyoainishwa na alama za nukuu vimechukuliwa moja kwa moja kutoka kwenye maandiko yenyewe. Inapendekezwa kwamba uyasome mawazo hayo mara kadhaa na yajadiliwe pamoja na washiriki wengine wa kikundi chenu.

> Tunaambiwa tutawanye "giza la utengano" na "kuwaona watu wote kama marafiki". Tunatarajiwa "kuwa wamoja na watu wote". Tunapaswa tugeuzie macho yetu kuelekea "mbingu ya utukufu wa kale" na kuvichukulia viumbe vyote kama "ishara ya Mungu", kwa kuwa ni kutokana na neema na uwezo Wake "kwamba kila kiumbe kiliingia ulimwenguni.
>
> Tumeagizwa "kushirikiana kwa undugu wenye mahaba na watu tusiowajua na rafiki hali kadhalika", tukidhihirisha kwa wote "wema wa upendo wa hali ya juu kabisa", na kutojali "kabisa kiwango cha uwezo wao" kutouliza kamwe kama "wanastahili kupendwa".
>
> Kama yeyote "akitudhihaki na kutukejeli" sisi, "tumwendee kwa upendo". Kama akitulundikia "lawama" juu yetu, sisi "tumsifu". Ikiwa atatupa "sumu ifishayo", sisi tumpe "asali bora kabisa badala yake". Ikiwa "atatishia" maisha yetu, tunapaswa sisi tumpe "tiba itakayomponya milele". Ikiwa atakuwa chanzo cha "maumivu", sisi tuwe "dawa" yake. Na akiwa kama "miiba", sisi tuwe kama "mawaridi na mimea tiba yenye ladha tamu".
>
> Tunaombwa kufanya jitihada kubwa, kwamba "koo na jamaa wote wa ulimwengu, hata maadui", waweke "imani yao, mategemeo na matumaini yao" ndani mwetu. Kama roho "hufanya makosa mara elfu mia moja", bado sharti aweze "kutumaini kusamehewa", ili "asikose tumaini wala kuhuzunika".
>
> Lazima "tuhimiliane kwa nguvu mmoja kwa mwingine na kutafuta maisha ya milele", na tuwe "rehema na baraka zilizotumwa" na Mungu.
>
> Tunaambiwa kuonesha "wema na urafiki, huruma na adabu" kwa watu wote, ili tuweze kuwa mithili ya "maji yaburudishayo kwa kila mwenye kiu" na kama "mkate wa mbinguni kwa kila mwenye njaa". Tunapaswa "kuonesha upole ambao si wa ulimwengu huu" Tunapaswa tufikirie "upendo na undugu mwema kama furaha za mbinguni", na kuuchukulia "uadui na chuki kama mateso ya moto wa jahanamu."

Lazima tuwe waangalifu “kutoidhuru roho yoyote wala kuufanya moyo wowote uhuzunike”. Sharti “tusizikirihishe hisia za mwingine, hata kama akiwa mtenda maovu” na anayetutakia “mabaya”. Tunahimizwa tusiviangalie “viumbe”, bali tugeukie kwa “Muumba wao.”

Tunaitwa “kujitoa dhabihu” wenyewe kwa ajili ya “usitawi wa wote” na “kujitahidi usiku na mchana” “kuboresha usitawi wa wanadamu”. Sharti tuomboleze sana “kwa ajili ya machozi” yaliyomwagwa na viumbe wa Mungu na tulie kwa “huzuni” ya watoto Wake. Sharti “tuachilie mbali starehe na raha zetu” ili tuweze kuwa “chanzo cha utulivu wa ulimwengu.”.

Tunaambiwa tuwe “baba wenye upendo kwa yatima, na kimbilio kwa wasiojiweza, na hazina kwa masikini, na tiba kwa wagonjwa.” Sharti tuwe “wasaidizi wa kila muathirika wa udhalimu, walezi wa walionyimwa.” Sharti tufikirie “nyakati zote juu ya kutoa huduma fulani kwa kila mwana-jamii wa mbari ya wanadamu.”

Sharti “tujitahidi” kufanya kila tuwezalo “kutakasa mioyo na akili za watu” na “kujitihadi kuifurahisha kila roho”. Sharti “tumtendee wema fulani kila mtu tunayekutana naye” na “kuwa wenye manufaa fulani kwake.” Lazima tujitahidi “kuboresha tabia ya wote, na kuzielekeza upya akili za watu.” Kazi yetu ni “kuwaita” watu kwa Mungu na “kuwaalika” wanadamu “kufuata mfano wa Kundi la juu”.

Tunaagizwa kuwaleta “wale walioachwa nje katika duara la marafiki wa karibu kabisa”. Tunapaswa “tuwaamshe wale waliolala” na kuwafanya “wazembe wawe makini”. “Katika giza la ulimwengu” sharti tuwe “miale angavu”. “Katika mchanga wa mateso ya milele” sharti tuwe “chemchemi za maji ya uzima” na “mwongozo kutoka kwa Bwana Mungu”.

Pengine sasa ungependa kukariri nukuu ifuatayo kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá:

**“Na kwenu, Enyi wapendwa wa Mungu, imarisheni hatua zenu katika Hoja Yake, kwa ile dhamiri kiasi kwamba hamtatikiswa hata kama majanga ya kuogofya kabisa yangeushambulia ulimwengu. Msifadhaishwe na chochote, kwa hali zozote zile. Muwe mliosimikwa kwa uthabiti kama milima mirefu, muwe nyota ambazo hupambazuka juu ya upeo wa uzima, muwe taa angavu katika mikusanyiko ya umoja, muwe roho nyenyekevu na dhalili mbele ya marafiki, muwe maasumu moyoni. Muwe alama za mwongozo na miale ya mwangaza ya ucha Mungu, mkijitenga na ulimwengu, mkiung’ang’ania mpini wa uhakika na wenye nguvu, mkieneza mbali roho ya uzima, mkipanda Safina ya wokovu. Muwe vyanzo vya ukarimu, mahali pa mapambazuko ya siri za uwepo, mahali ambako uvuvio hushukia, mahali pa kuchomoza wangavu, roho ambazo hudumishwa na Roho Mtakatifu, zikimpenda sana Bwana, zikijitenga na vyote ila Yeye, takatifu juu zaidi ya sifa bainifu za wanadamu, zikivikwa sifa za malaika wa mbinguni, ili muweze kujishindia majaliwa ya juu kabisa kuliko yote, katika wakati huu mpya, zama hizi za ajabu.”[25]**

## SEHEMU YA 17

Tunapoandamana na watu wote kwa moyo wa undugu, na kupitia jitihada zetu kuishi Maisha kufuatana na mafundisho, tunawavutia wengine kwenye Hoja. Bila shaka, hatutarajiwi kuwa wakamilifu, wala hatudai kuwa hatuna kasoro. Walakini kadiri tunavyoakisi sifa zilizowekwa katika mafundisho ndivyo tunavyokuwa njia zifaazo kwa ajili ya kueneza manukato matakatifu. Ni kwa namna hii kwamba mara nyingi tunazungumza juu ya ufundishaji kwa kupitia mfano. Lakini sharti tuwe waangalifu kwamba kirai "ufundishaji kwa kupitia mfano" kisiwe kisingizio cha kutofundisha. Ni kweli kwamba tunahitaji kuwa makini sana juu ya hali yetu ya ndani, kwa tabia zetu, kwa matendo yetu, na kwa unyofu wa mwenendo wetu. Hii, hata hivyo, isitufanye tusipoteze mwelekeo juu ya ukweli kwamba ni kwa kupitia ufunguo wa matamshi yetu kwamba tutafungua malango ya mji wa moyo wa mwanadamu. Ili kulifafanua jambo hili, hebu tuangalie seti mbili za nukuu kutoka maandiko na tujaribu kuzielewa pamoja. Kwanza tusome nukuu zifuatazo:

> **"Yeyote ainukaye miongoni mwenu kufundisha Hoja ya Bwana wake, mwache, kabla ya yote, aifundishe nafsi yake mwenyewe, ili kauli yake iweze kuvutia mioyo ya wale ambao humsikiliza. Vinginevyo ataifundisha nafsi yake mwenyewe, maneno ya mdomo wake hayataushawishi moyo wa mtafutaji."[26]**

> **"Jambo moja na jambo moja tu bila kushindwa na pekee litakaloipatia Hoja hii takatifu ushindi wa uhakika, yaani, kadiri maisha yetu wenyewe ya ndani na tabia ya faragha zinavyodhihirisha katika sura zake mbalimbali wangavu wa zile kanuni za milele zilizotangazwa na Bahá'u'lláh."[27]**

> **"Yeyote ainukaye, katika Siku hii, kuisaidia Hoja Yetu, na kuyaita majeshi yenye tabia istahiliyo sifa na mwenendo mnyofu kumsaidia, ushawishi utiririkao kutokana na kitendo kama hicho, kwa hakika kabisa, utaenezwa kote ulimwenguni."[28]**

> **"Acheni *matendo* yenu yautangazie ulimwengu kwa sauti kubwa kwamba kwa hakika ninyi mu Wabahá'í, kwa kuwa ni matendo ambayo huzungumza na ulimwengu na ni chanzo cha maendeleo ya wanadamu.**

> **"Kama tu Wabahá'í wa kweli maneno hayahitajiki. Matendo yetu yatausaidia ulimwengu, yataeneza ustaarabu, yatasaidia maendeleo ya sayansi, na kusababisha sanaa kukua. Bila matendo hakuna chochote kinachoweza kutimizwa katika ulimwengu wa kimwili, wala maneno bila kusaidiwa kumuendeleza mtu katika Ufalme wa kiroho. Siyo kwa maneno matupu tu kwamba wateule wa Mungu wamefikia utakatifu, bali kwa maisha yenye subira ya huduma amilifu wameleta mwangaza ulimwenguni."[29]**

Sasa jifunze nukuu zifuatazo:

> **"Ni kwenye nyakati kama hizi kwamba marafiki wa Mungu hujipatia wasaa, hujitwalia fursa, huharakia na kujipatia tuzo. Kama kazi yao inahusika tu na mwenendo mwema na ushauri, hakuna kitakachotimizwa. Lazima wazungumze kwa sauti kubwa, wafafanue shuhuda, waweke hoja zilizo dhahiri, watoe maamuzi yasiyokanushika kuusimamisha ukweli wa udhihirisho wa Jua la Uhalisi."[30]**

**“Basi usiangalie kiwango cha uwezo wako, angalia fadhili zisizo na mipaka za Bahá’u’lláh; fadhili Yake huvizingira vyote, na neema Yake ni kamili.”[31]**

**“Geuzia uso wako kuelekea Ufalme wa Mungu, omba majaliwa ya Roho Mtakatifu, zungumza, na mathibitisho ya Roho yatakuja.”[32]**

**“Enyi wapendwa wa Mungu! Msijipumzishe wenyewe vitandani mwenu, bali, jiamsheni wenyewe mara mumtambuapo Bwana wenu, Muumba, na sikilizeni mambo yaliyomsibu, na harakieni kumsaidia. Legezeni ndimi zenu, na tangazeni bila kukoma Hoja Yake. Hili litakuwa bora zaidi kwenu kuliko hazina zote za wakati uliopita na za wakati ujao, kama mkiwa miongoni mwa wale wanaoufahamu ukweli huu.”[33]**

**“Kama marafiki wakati wote wangengojea mpaka wamekuwa wastahilifu kabisa kufanya kazi yoyote maalum, kazi ya Hoja ingekaribia kusimama! Lakini kitendo chenyewe cha kujitahidi kuhudumu, hata kama mtu angejihisi hastahili, huvutia baraka za Mungu na humuwezesha mtu kuwa mwenye kufaa zaidi kwa kazi hiyo.**

**“Leo hitaji ni kubwa mno kwa wanadamu kusikia Ujumbe Mtakatifu, kwamba waumini lazima wajitose katika kazi hii, popote pale na kwa vyovyote vile wawezavyo, bila kujali kasoro zao wenyewe, lakini daima wakijali hitaji kubwa sana la wanadamu wenzao kusikia mafundisho katika saa yao ya giza totoro la taabu.”[34]**

Kama tukitenganisha seti ya kwanza ya nukuu kutoka vifungu vingine vyote juu ya mada ya ufundishaji—ni mifano yake michache tu ambayo imetolewa katika seti ya pili—na kukazia tu juu yao, tungeweza kuishia kuzitumia kama kisingizio cha kutofundisha. Tunaangukia kwenye mtego huu pale tunapofikia uamuzi kimakosa, kwamba kazi yetu kubwa ni kuboresha hali yetu wenyewe ya ndani na kuwa watu bora zaidi na zaidi hadi tufikie mahali ambapo tunakuwa wakamilifu mno kiasi kwamba hatuhitaji maneno kufundisha, kwa sababu wengine watavutiwa nasi na watafanya kila wanaloweza kuichunguza Imani wao wenyewe. Lakini tunajua kwamba ‘Abdu’l-Bahá, ambaye aliishi maisha ya matendo ya mfano zaidi kuliko yoyote yale ya kwetu, alitumia uwezo wa matamshi Yake na, katika kila fursa iliyofaa, alizungumza juu ya Imani.

Jambo muhimu kutambua ni kwamba mada kuu ya seti ya kwanza ya nukuu siyo jinsi ya kufundisha Imani. Vifungu hivi hutufunulia zile kweli za ndani kabisa za kiroho kuhusu maana ya hali yetu ya ndani. Vinatukumbusha kwamba tabia istahiliyo sifa na mwenendo mnyofu huongeza uwezo wa vitendo vyetu na kutuonya kuwa vitendo vyetu haviwezi kupinga maneno yetu. Kama mtu anakwenda kufundisha uaminifu, kwa mfano, mtu huyo anapaswa ajitahidi kwa kweli kuwa uaminifu.

Kwa jumla, siyo busara kutwaa somo pana, la undani sana, kama vile ufundishaji, na kufikia maamuzi juu yake kwa kuzingatia nukuu moja au mbili.

Tukiwa na mawazo haya akilini, hebu turudi nyuma kwenye vifungu vya hapo juu na kutafakari juu yao wakati tunajaza nafasi zilizo wazi katika sentensi za hapa chini kwa maneno yanayofaa.

1. Yeyote ainukaye kufundisha Hoja ya Bwana wake, mwache, kabla ya yote, ________
________________________________________________________________________
__________________________________________________________ .

2. Vinginevyo mtu huifundisha nafsi yake mwenyewe, ____________________________
__________________________________________________________ .

3. Jambo moja na jambo moja tu bila kushindwa na pekee litakaloipatia Hoja hii ushindi wa uhakika, yaani, ________________________________________________________
________________________________________________________________________
____________________________________________________________________ .

4. Yeyote ainukaye, katika Siku hii, kuisaidia Hoja ya Mungu, na kuyaita ______________________________________________________ , ushawishi utiririkao kutokana na kitendo kama hicho, kwa hakika kabisa, ____________________________
______________ .

5. Ni vitendo ambavyo ________________________________________ na ni chanzo cha
_________________________________________ .

6. Kama tu Wabahá'í wa kweli, ___________________________________________ . Matendo yetu sharti yautangazie ulimwengu kwa sauti kubwa kwamba
__________________________________________ .

7. Matendo yetu sharti ___________________________________ , sharti ______________
_________________________ , sharti ________________________________________ , na ________________________________________________________ .

8. Bila matendo, ____________________________________________________________
_____________________________ , wala _____________________________________ .

9. Siyo kwa maneno matupu tu kwamba wale walio karibu na Mungu wamefikia utakatifu, bali kwa _____________________________________________________ .

10. Kama kazi yetu inahusika tu na mwenendo mwema na ushauri,____________________
_________________ . Lazima ______________ kwa sauti kubwa, __________________ shuhuda, __________________ hoja zilizo dhahiri, ______________________ kuusimamisha ukweli wa udhihirisho wa Jua la Uhalisi.

11. Sharti tusiangalie kiwango cha uwezo wetu, bali ______________________________
______________________________________ .

12. Sharti tugeuzie nyuso zetu kuelekea Ufalme wa Mungu, ____________________ __________________________________________, tuzungumze, na __________ ________________________________________________________.

13. Sharti tusipumzike vitandani mwetu, bali tunapaswa __________________________ mara tumtambuapo Bwana wetu, Muumba, na tusikiapo mambo yaliyomsibu, na ____________________________________________________________.

14. Tulegeze ndimi zetu na ________________________________________ _______________. Hili ni bora kwetu kuliko ________________________________ ____________________________________________.

15. Kama wakati wote tungengojea mpaka tumekuwa wastahilifu kabisa kufanya kazi yoyote maalum, ________________________________________________________ ______________________________.

16. Kitendo chenyewe cha kujitahidi kuhudumu, hata kama tunajihisi kuwa hatustahili hata kidogo, _______________________________________________________________.

17. Leo hitaji ni kubwa mno kwa wanadamu kusikia Ujumbe Mtakatifu, kiasi kwamba lazima, ________________________________________, popote pale na kwa vyovyote vile tuwezavyo, _______________________________________________________, lakini daima tukijali ____________________________________________________ _________________ katika katika saa yao ya giza totoro la taabu.

## SEHEMU YA 18

Hebu tumalizie kitengo hiki juu ya sifa za kiroho na mielekeo ambayo huanisha jitihada zetu za ufundishaji kwa kukumbuka mfano uliowekwa na ‘Abdu’l-Bahá wakati wa safari Zake huko Magharibi. Kifungu cha hapo chini kilichoandikwa na Mlinzi kinachoelezea namna ‘Abdu’l-Bahá alivyotoa Ujumbe wa Baba Yake kwa wale aliokutana nao, kitatuandaa kwa kitengo kifuatacho ambacho tutachunguza kitendo chenyewe cha ufundishaji.

> **“Wakati wa safari hizi ‘Abdu’l Bahá alionesha nguvu, ujasiri, umakini, kujitoa wakfu kwa kazi aliyojipangia kufanikisha ambavyo vilisisimua mshangao na upendo wa wale waliobahatika kuviona kwa karibu vitendo Vyake vya kila siku. Bila kujali mandhari na vitu vya kipekee ambavyo kwa kawaida huteka hisia za wasafiri na ambavyo wasafiri wenzake aghalabu walitamani Yeye kuvitembelea, bila kujali vile vile raha Yake na afya Yake; akitumia kila wakia wa nguvu Zake siku hadi siku kuanzia alfajiri hadi usiku kabisa; akikataa kwa msisitizo zawadi zozote au michango kwa ajili ya matumizi Yake ya safari; wakati wote asiyeshindwa katika kuwasaidia Kwake wagonjwa, wenye huzuni na walioonewa; asiye na maridhiano katika uteteaji Wake wa makabila na matabaka yaliyodhalilishwa; mwingi mithili ya mvua ukarimu**

**Wake kwa mafukara; mwenye kudharau mashambulizi dhidi Yake na watetezi makini na shupavu wa imani na madhehebu, mwenye kustaajabisha katika uwazi Wake wakati wa kufafanua, jukwaani na katika madhabahu, Dhima ya kinabii ya Yesu Kristo kwa Wayahudi, juu ya chimbuko Takatifu la Uislamu katika makanisa na masinagogi, au ukweli wa Ufunuo Mtakatifu, na hitaji la dini kwa wayakinifu, wapagani au wasio na dini; asiyeyumba katika kumtukuza Kwake Bahá'u'lláh wakati wote na ndani ya hifadhi ya vikundi na madhehebu anuwai; thabiti katika kukataa Kwake, mara kadhaa, kujipendekeza kwa watu wenye nyadhifa na utajiri kote Uingereza na Amerika; na mwisho lakini siyo kwa umuhimu asiyelinganishika katika unyumbulikaji, uhalisi na ukunjufu wa huruma na wema wa upendo Wake ulioneshwa kwa marafiki na wageni kadhalika, waumini kwa wasioamini, matajiri kwa masikini, wakubwa kwa wadogo, ambao Alikutana nao, kwa ukaribu sana au bila kutarajia, iwe melini, au wakati wa kutembea mitaani, bustanini na kwenye viwanja vya umma, kwenye tafrija au dhifa, makazi duni au makasri, katika mikusanyiko ya wafuasi Wake au mikutano ya wasomi, Yeye, ambaye ni mfano halisi wa kila njema ya Kibahá'í na mfano wa kila wazo la Kibahá'í, aliendelea kwa kipindi cha miaka mitatu iliyosongamana kuupigia baragumu ulimwengu uliokuwa ummezama katika uyakinifu na ambao tayari ulikuwa katika kivuli cha vita, uponyaji, kweli zilizotolewa na Mungu zilizomo katika Ufunuo wa Baba Yake."[35]**

Baada ya kusoma kifungu cha hapo juu kwa mara nyingine tena, andika sentensi kadhaa zinazoelezea sifa na mielekeo zinazoainisha jinsi 'Abdu'l-Bahá alivyochangamana na watu na alivyoyaendea mazungumzo Yake kuhusu Imani—kwa mfano, "Yeye alionesha nguvu, ujasiri, na umakini."

1. ______________________________
2. ______________________________
3. ______________________________
4. ______________________________
5. ______________________________
6. ______________________________
7. ______________________________
8. ______________________________
9. ______________________________
10. ______________________________

# MAREJEO

1. *Nyaraka za Mpango Mtakatifu: Zilizofunuliwa na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1993, toleo la 2006), na. 8.13, uk. 54, Kiingereza.

2. Kama hapo juu, na. 10.10, uk. 72, Kiingereza.

3. Kutoka barua ya 8 Novemba 1956 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu binafsi, iliyochapishwa katika *Ufundishaji wa Imani ya Kibahá'í: Makusanyo na Tamko lililoandaliwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (Mona Vale: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 1995), na. 156, ku. 84–85, Kiingereza.

4. Kutoka barua ya 6 Novemba 1949 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu binafsi, iliyochapishwa katika *Nguvu ya Msaada Mtakatifu: Makusanyo ya Dondoo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh, Báb na 'Abdu'l-Bahá na barua za Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, zilizokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Ingleside: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í Australia, 2020), na. 8, uk. 40, Kiingereza.

5. Kutoka Mazungumzo yaliyotolewa 4 Novemba 1911, (kuchapishwa katika Hekima ya 'Abdu'l-Bahá) *Hotuba zilizotolewa na 'Abdu'l-Bahá 1911–1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, chapisho la 2016), na. 21.6, uk. 76.

6. Kutoka barua ya 1 Septemba 1933 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu binafsi, iliyochapishwa katika *Ufundishaji wa Imani ya Kibahá'í*, na. 92, uk. 69.

7. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, chapisho la 2015), na. 216.1, uk. 372, Kiingereza.

8. Kutoka barua ya 30 Juni 1937 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu mmoja, iliyochapishwa katika *Nguvu ya Msaada Mtakatifu*, na. 7, uk. 37.

9. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitab-i-Aqdas*, (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1988, chapisho la 2021), na. 10.10, uk. 192, Kiingereza.

10. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 213.1, uk. 371, Kiingereza.

11. Kama hapo juu, na. 214.2, uk. 372, Kiingereza.

12. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1983, chapisho la 2017), V, aya. 3, uk. 7, Kiingereza.

13. Kama hapo juu, CXXXII, aya. 5, ku. 326–27.

14. Kama hapo juu, C, aya. 1, ku. 227–28.

15. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 204.2, uk. 347.

16. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXLII, aya. 5, uk. 351.

17. Kutoka barua ya 24 Novemba 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabáh'i wa Amerika, iliyochapishwa katika *Utawala wa Kibaha'i: Jumbe zilizoteuliwa 1922–1932* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1974, chapisho la 1998), uk. 69.

18. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 217.1, uk. 373.

19. Kama hapo juu, na. 15.3, ku. 46–47.

20. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa*, (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2003, chapisho la 2022), Kiarabu na. 44, uk. 13.

21. Kutoka barua ya 31 Machi 1932, iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu mmoja, iliyochapishwa katika *Nguvu ya Msaada Mtakatifu*, na. 66, ku. 35–36.

22. Kutoka ujumbe wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara, uliochapishwa katika *Mpango wa Miaka Tisa, 2022–2031: Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (West Palm Beach: Palabra, Shirika la Uchapishaji, 2022), na. 6.10, uk. 48.

23. Kutoka barua ya 5 Juni 1847 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, iliyochapishwa katika *Chimbuko la Imani* (Kiingereza): *Jumbe kwa Amerika, 1947–1957* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1965, chapisho la 2014), ku. 25–26.

24. Kutoka barua ya 24 Novemba 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'i wa Amerika, iliyochapishwa katika *Utawala wa Kibahá'i: Jumbe Zilizochaguliwa 1922–1932*, ku. 69–70.

25. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 199.6, ku. 334–35, Kiingereza.

26. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXVIII, aya. 6, uk. 313, Kiingereza.

27. Kutoka barua ya 24 Septemba 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'i wa Amerika, iliyochapishwa katika *Utawala wa Kibahá'i: Jumbe zilizochaguliwa 1922–1932*, uk. 66, Kiingereza.

28. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXXI, aya. 4, uk. 325, Kiingereza.

29. Kutoka Mazungumzo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá 8 Novemba 1911, yaliyochapishwa katika Hekima ya 'Abdu'l-Bahá, na. 26.5–6.

30. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 212.1, uk, 370.

31. Kama hapo juu, na. 153.3, uk. 249.

32. Kama hapo juu, na. 153.4, uk. 250.

33. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CLIV, aya. 2, uk. 374.

34. Kutoka barua ya 4 Mei 1942 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu mmoja, iliyochapishwa katika *Ufundishaji wa Imani ya Kibahá'í*, na. 104, uk. 72.

35. Shoghi Effendi, *Mungu Yu Nasi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1974, chapisho la 2022), ku. 446–48.



# Kitendo cha Ufundishaji

## Kusudi

Kuongeza uwezo
kutambua na kulea upokevu na
kukuza uwezo wa kufanya uwasilishaji wa Imani wenye mantiki,
unaowiana na hali, iwe sehemu ya jitihada za ufundishaji binafsi
au katika muktadha wa kampeni ya pamoja

## SEHEMU YA 1

Baada ya kuchunguza asili ya kiroho ya ufundishaji katika kitengo cha kwanza, na sifa na mielekeo ya lazima kwa wale wanaofundisha, katika cha pili, sasa tunageuzia umakini wetu kwenye kitendo cha ufundishaji chenyewe. Kwa jumla tunatekeleza kitendo hiki kitakatifu katika mojawapo ya miktadha miwili: katika jitihada zetu kama watu binafsi na katika juhudi ya pamoja mashinani. Bila shaka, kama sehemu ya kiini kiendeleacho kukua cha marafiki katika ujirani na vijiji vyetu ambacho kinajihusisha na shughuli za kujenga jumuiya zinazopuma, tumekutana na watu binafsi wengi kutoka usuli tofauti tofauti—wanafunzi wa elimu ya juu na vyuoni, wazazi na ndugu wa watoto na vijana chipukizi wanaoshiriki katika programu za kielimu za taasisi, walimu, wakulima, machifu wa vijiji na viongozi wengine wa mitaa, kwa kuwataja baadhi—na tumeona shauku ambayo baadhi yao wameonesha katika kujifunza zaidi kuhusu Imani. Ushiriki wetu katika mchakato wa taasisi, vile vile, umetumika kuimarisha ndani mwetu uwezo uhitajikao kuongoza roho kuelekea bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh, hasa ule unaotuwezesha kuelezea uelewa wetu wa dhana za kina na kuchunguza uhalisia wa kiroho katika mazungumzo ya maana. Mbali na uwezo huu, kuna mwingine mmoja ambao ni wa lazima kwetu kuukuza, kwa yote mawili, wakati tunapofuatilia jitihada zetu binafsi za ufundishaji na tunaposhiriki katika jitihada za pamoja—yaani, uwezo wa kutambua na kulea upokevu kwa ujumbe wa Bahá'u'lláh. Tutaangalia umuhimu wa kujenga uwezo huu katika sehemu zitakazofuata. Kwanza, hata hivyo, hebu tutafakari juu ya mameno yafuatayo ya Bahá'u'lláh, ambayo huenda ungependa kuyakariri:

> **"Pindi mnapokutana na roho yenye kiu, mpe anywe kutoka kikombe cha uhai wa milele; na pindi mnapolikuta sikio sikivu, mtongoleeni aya za Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye Huruma. Legezeni ndimi zenu kwa maneno mema na, endapo mtawapata watu wenye mwelekeo kuelekea Hifadhi ya Mungu, waiteni kwenye ukweli . . ."[1]**

## SEHEMU YA 2

Dhana muhimu ambayo wale wanaopenda kukuza uwezo wa kutambua na kulea upokevu wanapaswa kuelewa ni kwamba ufundishaji ni zaidi ya utangazaji tu wa Imani.

Utangazaji ni shughuli ya lazima na istahiliyo sifa kabisa, inayofanywa na watu binafsi kwa kiwango kinachotofautiana cha urasimu, jumuiya na asasi zao. Shughuli kama hiyo hutumika kuwafahamisha watu malengo na maadili bora ya Hoja na husaidia kuimarisha mielekeo chanya kwa Imani. Kufundisha hujumuisha kipengele cha utangazaji, lakini kusudi lake kuu ni kuzisaidia roho kumtambua Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa wakati huu, katika kuongeza ujuzi wao wa Ufunuo Wake, na katika kuthibitishwa katika imani yao walioipata hivi karibuni. Inawezekana, bila shaka, kwamba kupitia kitendo cha utangazaji, roho moja pokevu hasa inaweza kupendezwa na Imani na, baada ya uchunguzi kidogo, ikaamua kujiunga. Hata hivyo, hatupaswi kutarajia, angalau katika hatua hii ya historia ya mwanadamu, kwamba utangazaji pekee utafungua mioyo ya watu wengi sana kwa Bahá'u'lláh—hili, haidhuru mradi unaandaliwa kwa mbwembwe kubwa kiasi gani au jinsi ambavyo tukio lingeweza kutekelezwa kitaalamu. Ufundishaji ni zaidi ya kutoa taarifa na kuwaacha watu wao wenyewe. Unahusisha maongezi. Huhitaji maongezi kati ya roho zilizothibitishwa na zile ambazo zipo radhi kusikiliza na kuchunguza ukweli wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Ili kuchunguza zaidi kipengele hiki, hebu tutazame mfano ufuatao.

Njia moja ifaayo ya kufundisha Imani ni kupitia fayasaidi. Fayasaidi ni mikutano kunjufu na ya ukaribu sana inayofanyika nyumbani kwa mtu ambapo wale wanaopenda kujua zaidi kuhusu Imani wanakaribishwa. Mikutano hiyo inatoa fursa nzuri sana kwa ajili ya kubadilishana mawazo na maongezi yenye tija ambayo yanaweza kuwaongoza watu kumpokea Bahá'u'lláh. Hata hivyo, kama hakutakuwa na umakini, fayasaidi unaweza kugeuka kwa urahisi kuwa tukio la utangazaji.

Sasa, kwa kusudi la mfano wetu, tuseme wewe unafanya fayasaidi kila juma nyumbani kwako. Unaanza kila mkutano kwa kuwakaribisha wageni wako na kumuomba Mbahá'í mmoja aseme sala. Halafu mzungumzaji mkuu aliyealikwa hutoa hotuba kwa muda wa nusu saa au dakika arobaini na tano juu ya mada maalum kuhusu Imani. Mwishoni, unauliza kama kuna maswali yoyote, na kwa kawaida kuna moja au mawili, ambayo mzungumzaji hujaribu kuyajibu. Halafu viburudisho hutolewa, na wageni wako huondoka. Wewe ungekubali kwamba mkutano kama huo ingawa una faida zake, hususan ungechukuliwa kama tukio la utangazaji?

Hebu tuchulie kwamba baada ya muda kidogo, unaamua kubadili mwenendo wa mikutano. Hivyo, kwa kila fayasaidi, unamwalika rafiki mmoja au wawili wenye vipaji kufanya tumbuizo fupi la muziki baada ya mazungumzo, akitumaini kwamba uingizaji wa muziki ungeinua hali ya kiroho ya tukio hilo. Je, unadhani kwamba kwa kufanya hivi umebadilisha fayasaidi kutoka utangazaji na kuwa tukio la ufundishaji?

Ni zipi baadhi ya mbinu ambazo zingekusaidia kuifanya fayasaidi iwe shughuli ya ufundishaji zaidi?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

## SEHEMU YA 3

Sasa, tukiwa na tofauti kati ya ufundishaji na utangazaji akilini, hebu tufikirie jinsi tunavyoweza kuzibaini roho pokevu, zile ambazo mioyo yao inatafuta ukweli. Bila shaka, tunahitaji kusali kwa bila kukoma, ili Mungu atuongoze kwa zile ambazo Yeye Ameziandaa kupokea Ujumbe Wake. Lakini kisha sharti tuwe tayari kuzitambua pale tunapokutana nazo. Hili siyo jambo rahisi mara zote. Hata katika suala la jitihada za pamoja za ufundishaji miongoni mwa kundi lenye upokevu mkubwa, si kila mmoja atataka kuusikia ujumbe na kuukumbatia ukweli wake; ni juu yetu kuzitafuta zile roho ambazo zipo tayari kuitikia mwito wa Bahá'u'lláh.

Mtu mpokevu si lazima aonekane anayetafuta Imani, au hata mwenye kuvutiwa hasa na dini. Kwa kweli, ni muhimu kutambua kuwa upokevu na kupenda dini siyo kitu kimoja. Kile

kinachohitajika ni hali ambamo mtu yupo tayari kujifunza kuhusu mafundisho na kuchunguza ukweli kwa kiwango fulani cha uwazi. Kadiri tunavyoendelea kupata tajiriba katika ufundishaji, na kadiri uwezo wetu wa kiroho unavyonolewa zaidi na zaidi, uwezo wetu wa kuhisi hali hii huongezeka.

Ingawa haiwezekani kuweka kanuni thabiti kuhusu kile kinachomfanya mtu awe mpokevu, tunaweza kubaini baadhi ya vigezo vinavyochangia. Vigezo hivi aghalabu huwafanya watu kuwa wapokevu zaidi kwa nyakati fulani katika maisha yao kwa kipindi fulani cha muda. Huu ni ukweli kuhusu watu binafsi na watu wote. Jadili mada hii pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako na andikeni baadhi ya vigezo hivi ambavyo wewe unadhani vinaweza kuathiri upokevu wa watu, kama vile mfano ufuatao:

Kutambua utovu wa haki ulioenea ulimwenguni ____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

Inapendekezwa kwamba, kabla ya kuendelea na sehemu inayofuata, mtafakari juu ya kifungu hiki kilichoandikwa na Shoghi Effendi. Kinaongelea kuhusu uhusiano uliopo kati ya msukosuko wa zama hizi na upokevu kwa Hoja.

> **"Fursa ambazo msukosuko wa zama hizi hutoa, pamoja na huzuni zote uziamshazo, woga ambao huuchochea, ukatishaji tamaa ambao huuleta, utatanishi ambao huufanyiza, hasira ambazo huziamsha, maasi ambayo huyachochea, manung'uniko ambayo huyasababisha, moyo wa utafutaji usiopumzika ambao huuamsha, lazima, kwa jinsi hiyo hiyo, vitumike kwa kusudi la kueneza mbali na kwa mapana elimu ya nguvu ya wokovu ya Imani ya Bahá'u'lláh, na kwa ajili ya uandikishaji wafuasi wapya katika jeshi litanukalo daima la wafuasi Wake."[2]**

Tunaweza kuona kwa uwazi kabisa kwamba misukosuko ya ulimwenguni kote ambayo Mlinzi aliielezea miongo mingi iliyopita iliongezeka tu kadiri muda unavyopita na kadiri utaratibu wa zamani unavyoendelea kumomonyoka. Hapo chini kuna baadhi ya hali ambazo kwazo misukosuko hii huiibua. Jadili pamoja na kikundi chako matokeo ya kila moja kwa jitihada zetu za ufundishaji.

- Huzuni ambazo huziamsha
- Woga ambao huuchochea
- Ukatishaji tamaa ambao huuleta
- Utatanishi ambao huufanyiza

– Hasira ambazo huziamsha
– Maasi ambayo huyachochea
– Manung'uniko ambayo huyasababisha
– Moyo wa utafutaji usiopumzika ambao huuamsha

## SEHEMU YA 4

Tunapowapata watu ambao ni wapokevu, tunaingia kwenye mazungumzo nao, wakati mwingine kwa muda mfupi kidogo na wakati mwingine endelevu, ambapo kusudi lake ni kuwasaidia kulitambua Daraja la Bahá'u'lláh. Lakini je, kiini cha mazungumzo haya kingekuwa nini? Tungesema nini kwa wale tunaowafundisha?

Jibu kwa swali hili kwa vyovyote vile si rahisi. Tayari unajua, kutokana na tajiriba uliyopata hadi sasa katika kushiriki mafundisho na kanuni za imani na marafiki zako na familia katika jumuiya yako, kwamba hakuna fomyula tunayoweza kujifunza na kuirudia kwa kila mtu katika kila hali. Watu ambao tumefanya nao mazungumzo ya ukaribu kama hayo, kila mmoja yumo katika hali maalum ya kiroho na mahitaji na maswali mbalimbali. Kadiri tunavyojitahidi kufundisha Hoja, sharti daima tutafakari jinsi gani kweli za Imani zinavyoweza kuelezwa kwa kila mtafutaji—nini kisemwe, na katika mtiririko upi mawazo yaelezwe.

Walakini, wakati tunapaswa tuzifahamu tofauti za mtu mmoja mmoja, tusifanye lile kosa la kuzisisitiza kupita kiasi kwa kiwango cha kupoteza mwelekeo wa umoja wa kimsingi wa uwepo wa wanadamu. Jinsi watu waitikiavyo Ujumbe wa Bahá'u'lláh hufuata ruwaza fulani, na ruwaza hizi huonekana hasa miongoni mwa wale watu utamaduni na usuli mmoja. Kama wewe ni mwanafunzi, kwa mfano, na unaanza kufundisha miongoni mwa rika lako, pole pole utapata uwasilishaji wa kutambulisha Imani ambao utawatosheleza takriban marafiki zako wote. Tondoti za yale unayosema zitabadilika, kwa kuwa kila wakati, maswali tofauti huulizwa na shauku mbali mbali huoneshwa. Lakini ruwaza ya kimsingi itabakia ile ile.

Mnapoanza kufikiria kimpangilio juu ya jinsi mtakavyoilezea Imani kwa wengine, mnaweza kuona inafaa kufikiria sura mbili za ujumbe mtakaouwasilisha. Ya kwanza ni taarifa. Msikilizaji, kwa kawaida, atapenda kujua mambo kadhaa ya ukweli juu ya Imani. Ilianza lini? Jumuiya ya Kibahá'í ni kubwa kiasi gani? Imeenea kiasi gani? Je, Wabahá'í wanaamini katika maisha baada ya kifo? Ni zipi kanuni za kimsingi za Imani ya Kibahá'í? Kama mnavyouweza kuona, idadi ya kweli zinazohusiana na Imani ni kubwa mno. Taarifa mtakazompa mtu kwa wakati fulani itategemea na aina ya mazungumzo yenu. Lakini kuna baadhi ya kweli ambazo mtafutaji kwa kawaida anahitaji kujifunza katika hatua za mwanzoni za uchunguzi wake, na ni jambo la kujielimisha hasa kufikiria kuhusu hizi. Katika nafasi hapo chini, andika baadhi ya taarifa ambazo unafikiri ungependa kuzitoa. Usijikalifu sana katika kutengeneza orodha yako. Utaombwa uipitie tena na kuirekebisha baada ya kujadiliana hoja zingine chache katika sehemu zinazofuatazo.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Sasa linganisha orodha yako na zile za washiriki wezako katika kozi hii.

## SEHEMU YA 5

Katika sehemu iliyotangulia, tulichunguza kipengele kimoja cha ujumbe tunaouwasilisha kwa watu katika jitihada zetu za kufundisha Imani, yaani, taarifa. Lakini tunajua kwamba ufundishaji unahusisha mambo mengi zaidi kuliko utoaji tu wa taarifa. Fikiria, kwa mfano, ukweli wa msingi kabisa kwa itikadi ya Kibahá'í, kwamba Bahá'u'lláh ni Mdhihirishaji wa Mungu kwa wakati huu. Kauli "Wabahá'í huamini kwamba Bahá'u'lláh ni Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku ya leo" pekee ni kipengele tu cha taarifa, bila shaka kipengele hiki ni taarifa muhimu kabisa katika ulimwengu. Walakini, je, tamko hili pekee linatosha kuwasaidia watu wengi kulitambua Daraja la Bahá'u'lláh?

Sasa fikiria jambo ambalo, ingawa linahusu ukweli huu, siyo taarifa tu, yaani, ile dhana kwamba "Bahá'u'lláh ni Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku ya leo". Wakati sehemu ya taarifa inahitaji tu kutolewa na kupokelewa, kulizingatia wazo hili huhitaji uelewa. Je, Bahá'u'lláh humaanisha nini kwa "Mungu" na "Mdhihirishaji", na ni nini asili ya dai Lake kwamba ni Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku hizi?

Mfano mwingine ni kauli "Wabahá'í hutii sheria zilizoletwa na Bahá'u'lláh." Kama ilivyo, kauli hii dhahiri ni kipengele cha taarifa, tena cha muhimu sana. Lakini kutoa habari hii tu ni sehemu ndogo sana ya kumuelezea mtu kwamba, kama Mbahá'í itambidi atii sheria fulani. Ili hilo liweze kufanyika, ni muhimu kumsaidia mtu huyo kupata angalau kiasi fulani cha uelewa juu ya dhana kadhaa zihusianazo, kwa mfano, dhana nzuri mno la "sheria" kama ilivyoelezwa na Bahá'u'lláh pale anapoziita sheria Zake "taa za majaliwa Yangu ya upendo miongoni mwa watumishi Wangu, na funguo za rehema Yangu kwa viumbe Wangu."

Pindi utakapoweza kutofautisha kati ya taarifa na dhana, hutakuwa na shida tena kutambua idadi kubwa ya dhana, ambazo uelewa wake utawasaidia watafutaji kumtambua Bahá'u'lláh na kujiunga na safu za wafuasi Wake. Jaribu kutengeneza orodha kama hiyo. Tena andika dhana zote ambazo huja akilini mwako, bila kujali kuhusu urefu wa orodha yako au mpangilio wake. Utarudi na kuipitia baadaye.

Sasa linganisha orodha yako na zile za washirki wenzako katika kozi hii.

## SEHEMU YA 6

Baada ya kuangalia tofauti kati ya dhana na taarifa, sasa hebu tukazie majadiliano yetu juu ya uwasilishaji wa mwanzoni ambao utautoa wakati unapoelezea Imani kwa mtu mwenye shauku lakini ambaye anajua kidogo juu yake. Kumbuka kwamba shabaha yako ni kufungua malango ya mji wa moyo wa mtafutaji kwa Bahá'u'lláh. Bila shaka, utampa msikilizaji taarifa fulani na kumsaidia kuelewa dhana kadhaa za kimsingi. Kwa udhahiri, dhana kuu ambayo unataka kuwasilisha ni kwamba Bahá'u'lláh ni Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku ya leo. Kwa kuwa ni kutokana na uelewa huu kwamba yeye ataamua kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í. Ukiwa na dhana hili kuu akilini, basi, itakubidi useme mambo kadhaa, ambapo yote yatasaidia kuifanya dhana hiyo ieleweke na kumuongoza mtafutaji kulitambua Daraja la Bahá'u'lláh.

Katika kuchagua dhana na taarifa utakazowasilisha, na mpangilio utakaoufuata, utahitaji kuweka umakini wa karibu kwenye kifungu kilichoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu:

> **"Wale ambao hujitangaza wenyewe kama Wabahá'í sharti wawe wamependezwa mno na uzuri wa Mafundisho, na kuguswa na upendo wa Bahá'u'lláh. Waumini wapya hawahitaji kujua mathibitisho, historia, sheria na kanuni zote za Imani, lakini katika mchakato wa kujitangaza wenyewe lazima, pamoja na kupata cheche ya imani, kimsingi wawe wamefahamishwa juu ya Wakuu wa Imani, vile vile kuwepo kwa sheria ambazo lazima wazifuate na utawala ambao lazima wautii."[3]**

Sasa, rudia zile orodha za dhana na taarifa ulizotayarisha katika sehemu zilizotangulia. Kutokana na maneno ya hapo juu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, amua ungeongeza nini kwenye orodha yako ya taarifa na nini ungeondoa. Tengeneza orodha mpya, ukiviweka vipengele hivyo katika mpangilio ambao ungeviwakilisha katika utambulishaji wa Imani. Fanya hivyo hivyo kwa orodha yako ya dhana.

Taarifa: ______________________________________________

Dhana: ______________________________________________

## SEHEMU YA 7

Ili kukusaidia kufikiria zaidi juu ya dhana na taarifa utakazojumuisha wakati unapomuelezea mtu Imani kwa mara ya kwanza, tutachukua hali ya kufikirika tu na kuchambua yale yanayosemwa.

Anna ni kijana mwenye umri wa miaka kumi na saba aishiye na familia yake katika kijiji kidogo na anasoma katika shule ya mji ulio karibu. Alilelewa kama Mkatoliki na alijifunza juu ya Imani ya Kibahá'í kutoka kwa kaka yake miaka minne iliyopita. Tangu wakati huo, amekuwa akisoma kozi za taasisi na kufanya shughuli za huduma, ikiwemo kuendesha, kwa msaada wa mama mmoja kijijini, darasa la watoto la Kibahá'í mara moja kwa juma.

Emilia anasoma katika shule hiyo hiyo kama Anna. Naye alilelewa kama Mkatoliki. Amekwishasikia juu ya Imani ya Kibahá'í hapo kabla, lakini anajua kidogo sana juu yake. Kuhusu imani yake mwenyewe, ingawa hajajihusisha sana na dini, amebeba upendo wa Kristo moyoni mwake na ni mtu mwema. Anna anapomuuliza iwapo angependa kuambatana naye kwenye darasa la watoto analowafundisha, Emilia anajiunga naye kwa furaha. Anapenda kusaidia darasa na kuwasaidia vijana wadogo kujifunza kukariri sala na nukuu kutoka Maandiko ya Kibahá'í. Maneno ya Bahá'u'lláh yanaugusa moyo wake, na anamwambia Anna, "je, unaweza kuniambia zaidi kuhusu Imani ya Kibahá'í?"

Katika sehemu zifuatazo, mtasoma maneno ya utangulizi ya Anna kadiri anavyoanza kumfundisha rafiki yake. Mnapaswa myasome vyema na mfanye mazoezi yahusianayo kwa uangalifu mkubwa. Mazoezi haya yamebuniwa kukusaidia kufikia maamuzi machache juu ya jinsi utakavyoelezea Imani kwa makundi tofauti tofauti ya watu. Kabla ya kwenda kwenye sehemu hizi, pengine ungependa kuandika hapo chini usuli wa baadhi ya makundi ambayo yumkini una uwezekano mkubwa wa kuyafundisha.

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 8

Hivi ndivyo Anna anavyoanza maelezo yake ya Imani kwa Emilia:

Tayari unajua kwamba Imani ya Kibahá'í ni dini ya ulimwengu ambayo mafundisho yake yamejikita juu ya umoja wa wanadamu. Wabahá'í ni wafuasi wa Bahá'u'lláh, Ambaye wao huamini ndiye Mwahidiwa wa zama zote. Mafundisho ya takariban watu wote yanajumuisha ahadi ya siku zijazo ambapo amani na mapatano vitasimamishwa duniani na wanadamu wataishi katika usitawi. Tunaamini kwamba ile saa iliyoahidiwa imefika na kwamba Bahá'u'lláh ndiyo ile Nafsi Kuu Ambaye Mafundisho Yake yataiwezesha jamii ya wanadamu kujenga ulimwengu mpya. Katika mojawapo ya Maandiko Yake, Bahá'u'lláh husema:

**"Kile ambacho Bwana ameamuru kama tiba kuu na chombo chenye nguvu kabisa kwa ajili ya uponyaji wa ulimwengu mzima ni muungano wa watu wake wote katika Hoja moja ya ulimwengu, Imani moja kwa watu wote."**[4]

Kama unakubali, kwanza nitaongelea maneno machache kuhusu jinsi mafundisho ya Imani ya Kibahá'í yanavyomwelezea Mungu na uhusiano wetu Naye. Bahá'u'lláh

hutufundisha kwamba Mungu hajulikani katika Asili Yake. Hii humaanisha kwamba taswira yoyote tuliyo nayo kuhusu Mungu akilini mwetu—kwa mfano, kumfikiria Yeye kama mtu—ni tunda la fikra zetu tu. Kwa ujumla, kile ambacho kimeumbwa hakiwezi kumuelewa muumba wake. Mathalani, meza haiwezi kuelewa asili ya fundi seremala ambaye ameitengeneza. Kuwepo kwa fundi seremala hakufahamiki kabisa kwa vitu anavyovitengeneza.

Mungu ndiye Muumba wa vitu vyote. Mwanadamu aliumbwa, tunaambiwa na Bahá'u'lláh, kutokana na upendo wa Mungu. Yeye husema:

**"Ewe Mwana wa Mtu! Nilipendezwa na kuumbwa kwako, na ndipo nikakuumba. Kwa hiyo, nipende ili niweze kulitaja jina lako na kuijaza roho yako kwa pumzi ya uzima."[5]**

Hivyo ingawa uwepo wa Mungu upo mbali na uelewa wetu, upendo Wake huyagusa maisha yetu na nafsi zetu bila kukoma. Jinsi upendo huu unavyotiririka kwetu ni kupitia Agano Lake la Milele. Kufuatana na Agano hili la Milele, Mungu kamwe hatuachi peke yetu na bila mwongozo. Katika kila zama, kadiri jamii ya mwanadamu inavyokengeuka kutoka Kwake na kusahau mafundisho Yake, Mdhihirishaji wa Mungu hutokea na hufanya Mapenzi na Kusudi Lake vijulikane kwetu.

Neno hili "dhihirisha" humaanisha kufunua, kuonesha jambo fulani ambalo lilikuwa halijulikani hapo kabla. Wadhihirishaji wa Mungu ni zile Nafsi maalum Ambazo huifunulia jamii ya wanadamu Neno na Mapenzi ya Mungu; hivyo tunapowasikiliza Wao, tunaitika Mwito wa Mungu.

Kuna mfano kutoka ulimwengu wa kimwili ambao hutusaidia kuelewa dhana hii ya "Udhihirisho" kama ilivyofundishwa na Bahá'u'lláh. Katika ulimwengu huu, jua ndio chanzo cha joto na mwangaza, ambavyo bila hivyo uhai usingekuwepo juu ya sayari. Lakini jua lenyewe halishuki duniani, na kama tungejaribu kulikaribia, tungeteketezwa kabisa.

Lakini mathalani tukichukua kioo kilichong'arishwa vyema na kukielekeza kwenye jua. Ndani yake tutaona taswira ya jua, na kadiri kioo hicho kinavyong'arishwa kwa ukamilifu zaidi, ndipo taswira hiyo itakavyokuwa kamili zaidi. Wadhihirishaji wa Mungu ni kama Vioo kamili ambavyo huakisi Mwangaza wa Mungu katika uzuri wake wote. Na Vioo vyote hivi huakisi Mwangaza ule ule. Wakati Mungu hatuwezi kumfikia, Nafsi hizi kamili hutujia kipindi hadi kipindi, huishi miongoni mwetu, hutupa miongozo, na hutujaza nguvu tunazozihitaji ili kuendelea, kimwili na kiroho.

Wewe una bahati ya kulelewa kulingana na mafundisho yaliyotumwa na Mungu kwa jamii ya wanadamu kama miaka elfu mbili hivi iliyopita kupitia Mdhihirishaji Wake, Kristo, Ambaye Daraja Lake ni lile la Mwana wa Mungu. Sasa unaweza kupokea mafundisho ya Mdhihirishaji mpya, Bahá'u'lláh, Ambaye jina Lake humaanisha "Utukufu wa Mungu". Mafundisho ya Bahá'u'lláh, hivyo, hupatana kabisa na mafundisho ya Kristo, lakini hushughulikia hali ya jamii ya mwanadamu kwa wakati huu. Kama ukifikiri kwa kitambo kidogo juu ya hali mbaya ya jamii ya wanadamu, nina hakika utakubali kwamba wakati umewadia kwa Mdhihirishaji mwingine wa Mungu kutokea. Hebu nikutongolee kifungu kimoja kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh ambacho kinaongelea juu ya Siku ambamo sisi tunaishi:

> **"Hii ndiyo Siku ambamo fadhili bora kabisa za Mungu zimemiminiwa juu ya watu, Siku ambamo neema Yake yenye nguvu kabisa imeingizwa ndani ya viumbe vyote. Imewapasa watu wote wa ulimwengu kusuluhisha tofauti zao, na, kwa umoja kamili na amani, waishi chini ya kivuli cha Mti wa uangalizi Wake na wema Wake wa upendo."[6]**

Kabla sijaendelea, labda ningesimama hapa ili tuweze kujadili maswali yoyote uliyonayo. Unafikiria nini juu ya yale ambayo nimeshiriki nawe hadi sasa?

## SEHEMU YA 9

Sasa hebu tuyachunguze yale ambayo Anna ameyasema hadi sasa. Vipengele vitano vya uwasilishaji wake vimechambuliwa katika mazoezi ya hapo chini. Wekea alama kauli zile ambazo unakubaliana nazo. Mazoezi haya hayahitaji majadiliano marefu. Unapaswa usome kila kauli, ichunguze, na amua kama unakubaliana nayo au hapana. Jambo muhimu la kukumbuka ni kwamba ufundishaji wa Imani lazima uendewe kwa mwelekeo wa kujifunza.

1. Anna anaanza kwa kusema kwamba Imani ya Kibahá'í ni dini ya ulimwengu ambayo mafundisho yake yamejikita juu ya umoja wa jamii ya wanadamu. Halafu mara tu humtambulisha Bahá'u'lláh kama yule Mwahidiwa wa zama zote.

   _____ Mara baada ya kumtambulisha Bahá'u'lláh kama Mwahidiwa ni njia nzuri sana ya kuwasilisha Imani kwa watu wa dini zote—Wakristo, Waislamu, Wahindu, Wabuddha na wengine—kwa kuwa dhana ya Mwahidiwa imekuwepo katika kila utamaduni wa kidini kwa namna moja au nyingine.

   _____ Watu wengi leo hawana shauku ya dini, hata kama wao ni waumini wa dini fulani, kwa hiyo ni bora kutotambulisha Utu wa Bahá'u'lláh papo hapo. Inafaa zaidi kuongelea kwanza kuhusu itikadi za Kibahá'í, kueleza kwa kina kidogo baadhi ya kanuni mbalimbali kama vile usawa wa wanaume na wanawake, utokomezaji wa aina zote za chuki na amani ya ulimwengu.

   _____ Kama unamfundisha mtu ambaye anaona taabu kumwamini Mungu, bado ungeutambulisha Utu wa Bahá'u'lláh papo hapo. Kwa jinsi hivyo, hata hivyo, kwanza utamrejelea Yeye kama mmoja wa wale Waelimishaji wa ulimwengu Ambao huja kwa jamii ya wanadamu kipindi hadi kipindi. Baadaye, ungeweza kuitambulisha dhana ya "Mdhihirishaji wa Mungu".

   _____ Uwasilishaji ambao Anna huutoa ungekuwa wenye ufanisi zaidi kama, baada ya kumtambulisha Bahá'u'lláh kama Mwahidiwa wa zama zote, angeendelea kwa kutaja idadi fulani ya matabiri ambayo yangemthibitishia Emilia kwamba Yeye ni utimizo wa kila utabiri.

   _____ Katika hali nyingi mno, utumiaji wa matabiri kuwathibitishia watu juu ya uhalali wa Daraja la Bahá'u'lláh husababisha shida. Huwafanya watu wawe wabishi, badala ya kuwaweka katika hali ya kutafakari. Anna huwasilisha wazo muhimu kwamba Bahá'u'lláh ndiye yule Mwahidiwa wa zama zote, lakini yeye haendi kwa undani.

2. Baada ya kuongea na Emilia kuhusu utu wa Bahá’u’lláh, Anna anaelezea kwa kifupi dhana ya Mungu na uhusiano Wake na wanadamu. Hususan jambo la kuangalia ni jinsi anavyoyatambulisha mawazo haya. Yeye haanzi kwa kusema “Wabahá’í huamini . . .”, wala hata “mimi naamini . . .” yeye anaweka wazi kwamba anachota kutoka mafundisho ya Bahá’u’lláh ili umakini unabaki juu Yake.

_____ Katika ulimwengu wa leo, kuzungumzia juu ya Mungu na uhusiano Wake na wanadamu mapema mno katika uwasilishaji wetu wa Imani kutawakatisha watu tamaa. Watu wengi sana hupenda zaidi mambo ya kijamii kuliko yale ya kiroho. Ingekuwa bora zaidi kwa Anna kutoileta mada hiyo.

_____ Kutambulisha wazo kwamba Mungu, kama ilivyoelezwa katika mafundisho ya Kibahá’í, kama Mungu Asili isiyojulikana ni jambo lenye manufaa sana kwa watafutaji kutoka kila usuli wa kidini na hata kwa wale ambao wana shida kumuamini Mungu. Kwa haraka huitenganisha Imani kutoka aina zote za ushirikina na itikadi isiyo ya kimantiki. Wakati huo huo, hushughulikia shauku ya roho ya mtafutaji kutambua Chanzo cha kuwepo kwake.

3. Anna ni mwangalifu kutumia neno “Mdhihirishaji” kila anapomtaja Bahá’u’lláh na Kristo. Dhana ya kioo humsaidia yeye kuelezea dhana hii kwa Emilia.

_____ Neno “Mdhihirishaji” ni gumu mno. Anna angepaswa kutumia neno “Mtume” kwa kuwa ni rahaisi zaidi na jepesi kulielewa.

_____ Mtu mwenye usuli wa Kikatoliki angechukulia ni ukosefu wa heshima kumtaja Kristo kama Mtume. Kwa mantiki hiyo hiyo, kama Anna angemtaja Bahá’u’lláh kama “Mtume”, angempa Emilia dhana kwamba daraja Lake ni la chini kuliko lile la Kristo.

_____ Kama mtu anamfundisha Muislamu, neno “Mjumbe” lingefaa, kwa kuwa Waislamu humtaja Muhammad kama Mjumbe wa Mungu lakini dhana ya “Mdhihirishaji wa Mungu” pia inapaswa kuelezwa.

_____ Ni sahihi kwa Anna kuepuka kusema kwa uwazi kwamba Bahá’u’lláh ni Kurudi kwa Kristo kwa kuwa wazo la “kurudi” limevurugwa mno katika akili za watu kiasi kwamba hakuna namna ya kujua lingekuwa na maana gani kwa Emilia. Kwa kutumia mfano wa kioo, Anna huwasilisha wazo hilo bila kulikanganya jambo hilo.

_____ Anna ametumia hekima kwa kutolieleza sana wazo la “Kristo kama Mwana wa Mungu”. Yeye hulitaja tu kwa kugusua na halafu huelezea kwamba Bahá’u’lláh ni Utukufu wa Mungu. Kwa kufanya hivyo, Anna anaukubali ukweli fulani bila kutoa maongezi nje ya muktadha.

_____ Kama ungekuwa unamfundisha mtu mwenye usuli wa Kihindu, bado ungetumia mfano wa kioo kuelezea dhana ya “Mdhihirishaji”. Lakini badala ya kumtaja Kristo, ungetaja kauli ya Bwana Krishna: “Wakati wowote uadilifu unapopungua, Ewe Bharat, na kuinuka kwa utovu wa dini, hapo ndipo Mimi hutuma roho Yangu. Kwa ajili ya wokovu wa walio wema, uangamizaji wa

waovu, na kwa ajili ya kuiweka imara dini ya kweli, Mimi hujidhihirisha Mwenyewe kutoka zama hadi zama."

_____ Kwa kumtambulisha Mungu kama Asili isiyojulikana, Anna anakiri kwamba mlamgo wa ujuzi wa Mungu umefungwa kwetu. Bado Mungu, kwa rehema Yake, huwatuma kwetu Wadhihirishaji Wake Ambao, mithili ya Vioo vikamilifu, huakisi sifa Zake zote na hutufunulia Kusudi Lake. Ufafanuzi huu wa dhana ya "Wadhihirishaji wa Mungu" unamfaa kila mtu, wakiwemo wale ambao wana shida kumwamini Mungu, shida ambayo aghalabu hutokana na namna Mungu anavyoelezewa kwa kawaida.

4. Alipokuwa anaongea na Emilia, Anna alinukuu moja kwa moja kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh mara chache.

_____ Maneno yaliyomo katika nukuu hizo ni magumu mno. Ingekuwa bora zaidi kwa Anna kuepuka kunukuu moja kwa moja kutoka Maandiko, hasa mapema kiasi hicho katika uwasilishaji wake, na kutoa mawazo hayo kwa maneno yake mwenyewe. Mbali na hilo, yeye anaepukana na hatari ya kusikika kama mhubiri.

_____ Anna huzifuma nukuu hizo katika uwasilishaji wake kwa namna ya kawaida, kwa kufuatana kabisa na ushauri wa Bahá'u'lláh Mwenyewe. Hata kama rafiki yake Emilia haelewi nukuu hizo kikamilifu, maneno hayo yatakuwa na athari moyoni mwake.

5. Anna hutumia mifano miwili kujadiliana dhana ngumu na Emilia. Kama ilivyotajwa hapo juu, mfano wa jua na kioo humsaidia Anna kuelezea kifungu cha maneno "Mdhihirishaji wa Mungu". Mfano mwingine anaoutumia ni ule wa fundi seremala na meza kuelezea dhana kwamba Mungu yu mbali na uelewa wa wanadamu.

_____ Kama ukitumia mifano unapowaelezea watu Imani, wao watafikiri kwamba unawadharau kwa namna fulani. Watu hawapendi kuchukuliwa kama watoto.

_____ Kutumia mifano ni njia ifaayo kuwafundisha watu wote—vijana au wazee, wasiojua kusoma na kuandika au walioelimika rasmi. Kwa kweli, bila mifano hii, ingekuwa vigumu sana kuelewa baadhi ya kweli za ndani kabisa zlizomo katika mafundisho ya Imani.

## SEHEMU YA 10

Ingawa Anna husita kidogo ili kumpa rafiki yake nafasi kuelezea hisia zake na kuuliza maswali, kwenye hatua hii ya awali ya mazungumzo, Emilia husema kidogo. Yeye anamwambia tu Anna kwamba anapenda yale aliyoyasikia hadi sasa, amefurahishwa hasa na njia ya kimantiki ambayo ya Imani ya Kibahá'í huelezea mambo; inatoa ufumbuzi wa mambo mengi ambayo huwakanganya watu kuhusu dini leo. Anna kisha anaamua kuendelea:

> Sasa hebu nikushirikishe baadhi ya mawazo yanayohusu mafundisho ya msingi ya Imani ya Kibahá'í, kwamba wanadamu ni wamoja. Bahá'u'lláh hutuambia kwamba

sisi ni matunda ya mti mmoja na majani ya tawi moja. Ingawa tunatofautiana kimuonekano mmoja kwa mwingine, ingawa tuna vipawa na uwezo tofauti, sote tunatoka kwenye mzizi mmoja; sote ni sehemu ya familia moja ya binadamu.

Jamii ya wanadamu inaweza kulinganishwa na bustani kubwa ambamo ndani mwake maua ya kila umbo, rangi na manukato hukua sambamba. Mvuto na uzuri wa bustani hiyo vimo katika anuwai hii. Tusiruhusu tofauti zilizopo miongoni mwetu – katika tabia zetu za kimaumbile, mielekeo yetu, usuli wetu, fikra na maoni yetu– ziibue mafarakano na ugomvi. Sharti tuwaone watu wa mbari ya mwanadamu kama maua mazuri yameayo katika bustani ya jamii ya wanadamu na tufurahie kuwa sehemu ya bustani hii.

Ingawa umoja wa jamii ya wanadamu ni ukweli usiokanushika, watu wa dunia wapo mbali mno nao kiasi kwamba kuwaunguanisha si kazi rahisi. Kama ukichagua kujiunga na Imani ya Kibahá'í—na ingeniletea furaha kubwa mno kama ungefanya hivyo—utakuwa umemkubali Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa wakati huu na utajitahidi kutumia mafundisho Yake siyo tu katika maisha yako mwenyewe bali pia katika jitihada za kufanya kazi sanjari na sote katika kujenga jumuiya zenye kupuma na zilizoungana. Sote tunajaribu kupatanisha mawazo na vitendo vyetu pamoja na imani yetu katika umoja wa jamii ya wanadamu. Tunaambiwa kwamba, wazo la vita likija akilini mwetu, mara moja tunapaswa tuliondoe kwa wazo la amani. Hisia ya chuki ikianza kujijenga mioyoni mwetu, mara moja tuliondoe kwa kwa hisia ya upendo. Tunapaswa tufanye kila liwezekanalo kuzishinda chuki zetu. Chuki ya kimbari, rangi, utaifa, kiutamaduni, kidini, na jinsi, hivi ni miongoni mwa vikwazo vikubwa kabisa vya kujenga ulimwengu bora zaidi. Vifungu vingi sana katika maandiko ya Kibahá'í vinatufundisha jinsi ya kutembea katika njia ya umoja na jinsi ya kuwasaidia wengine kufuata njia hiyo hiyo. Kuna kifungu kizuri ajabu kutoka mojawapo ya mazungumzo ya 'Abdu'l-Bahá, Ambaye nitamzungumzia baadaye, ambacho nimekikariri. Yeye husema:

**"Bahá'u'lláh amechora duara la umoja, Yeye ameweka muundo kwa ajili ya kuwaunganisha watu wote, na kwa ajili ya kuwakusanya wote chini ya kivuli cha hema la umoja wa ulimwengu. Hii ni kazi ya Fadhili Takatifu, na sote lazima tujitahidi kwa moyo na roho mpaka tumepata uhalisia wa umoja miongoni mwetu, na kadiri tufanyavyo kazi, ndivyo tutakavyopewa nguvu."**[7]

## SEHEMU YA 11

Mazoezi yafuatayo yatakusaidia kuchambua sura mbili za uwasilishaji wa Anna:

1. Katika suala hili mahsusi, Anna huchagua kuzungumzia kwanza somo kuhusu Mungu na Mdhihirishaji Wake na kisha juu ya kanuni ya umoja. Angeweza kabisa pia kuanza vinginevyo, akianza na kanuni ya umoja, akifuatia majadiliano juu ya Mungu na Mdhihirishaji Wake. Kwa vyovyote, yeye anachagua utaratibu wa kwanza kwa sababu anamfahamu Emilia na huuona mtiririko huu wa mawazo unafaa zaidi kwa ajili yake. Je, unaona manufaa yoyote katika mtiririko mmoja au mwingine? Je, mpangilio wa mawazo unaouchagua kuiwasilisha Imani ungetegemea juu ya yule ambaye ulikuwa unamfundisha? Kwa jinsi gani? Je, unaweza kutoa baadhi ya mifano?

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

2. Wakati wa uwasilishaji wake, Anna huonesha tumaini kwamba Emilia atakuwa Mbahá'í na atajifunza kuchota kwenye mafundisho wakati wa kuulea ukuaji wake kama mtu binafsi na katika kufanya kazi ya kujenga jumuiya zinazopuma na zilizoungana. Zipi kati ya kauli za hapo chini unakubaliana nazo? Ziwekee alama.

_____ Ni ujinga kumualika mtu kujiunga na jamii ya Kibahá'í wakati yeye bado anafahamu kidogo juu ya Imani. Huenda Emilia anakereka kwamba rafiki yake anajaribu kumbadilisha dini.

_____ Kwa kuonesha matumaini kwamba Emilia atakuwa Mbahá'í, Anna amevuka mipaka ya kiasi na anaongoa.

_____ Kwa kuonesha matumaini kwamba rafiki yake atakuwa Mbahá'í, Anna anaweka wazi mwanzoni, kwamba Emilia anakaribishwa kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í wakati wowote ule. Lakini anafanya hivyo kwa namna ambayo kwayo Emilia hajihisi kuwa anashinikizwa visivyo.

_____ Hakuna sababu ya Anna kuonesha matumaini kwamba Emilia atajiunga na Imani. Inatosha kwa Anna kumsaidia rafiki yake kujihusisha zaidi na zaidi katika ufanyaji shughuli za kuhudumia jumuiya, kwa kuwa hilo ndilo muhimu hasa.

_____ Kama tunapenda watu wajiunge na jumuiya ya Kibahá'í, tusiseme chochote kuhusu kile watakachopaswa kufanya hadi watakapokuwa wamejisogeza karibu zaidi na Imani. Ni vyema zaidi, tungengojea hadi watakapokuwa wamejitangaza.

_____ Inahuzunisha kusema, lakini watu wengi sana wanapenda tu kile kitakacho wanufaisha wao. Hawajali kile wanachoweza kufanya ili kuusaidia ulimwengu unaowazunguka. Badala ya kumuelezea Emilia jinsi atakavyoshiriki katika jitihada ya kujenga zinazopuma na zilizounganika, Anna angemwambia kuhusu upendo na undugu mtu auhisio pale anapojiunga na Imani.

_____ Anna anaweka usawa katika kumuwasilishia rafiki yake hisia ya kile kitakachomaanisha, kivitendo, kwa yeye kuwa Mbahá'í. Yeye anaifanya ionekane kama changamoto, lakini isiyoelemea. Nukuu ambayo Anna huchagua hususan inafaa hasa, kwa Emilia kuelewa kwamba ataongezewa nguvu katika jitihada zake za kufanya kazi kwa ajili ya umoja na maendeleo ya kijiji chake. Pindi Emilia atakapokuwa mwana-jamii wa jumuiya ya Kibahá'í, yumkini, hatakuwa mtazamaji baridi, bali mfanyakazi amilifu wa Hoja.

## SEHEMU YA 12

Kama watu wengi kabisa siku hizi, Emilia amevutiwa hasa na Mafundisho ya Kibahá'í juu ya umoja. Akitiwa shauku na kile alivchosikia kuhusu jitihada za Wabahá'í katika sehemu nyingi za kujenga jumuiya zilizounganika, anaingia katika mazungumzo mafupi lakini yakusisimua na Anna juu ya madhara ambayo chuki za kila aina huleta kwa jamii ya wanadamu. Halafu Anna huendelea na uwasilishaji wake:

Bahá'u'lláh alizaliwa mnamo mwaka 1817 huko Tehrán, mji mkuu wa Iran. Tangu utoto Wake wa mapema, Yeye alionesha ishara za ukuu. Ingawa Yeye alipata mafunzo kidogo nyumbani, Yeye hakuhitaji kuhudhuria shule, kwa kuwa alijaliwa na Mungu ujuzi wa kiasili. Bahá'u'lláh alitokana na familia bora na alipokuwa kijana, alipewa wadhifa wa juu katika baraza la Mfalme, lakini Yeye aliukataa. Yeye alipenda kutoa muda Wake kwa ajili ya kuwasaidia wadhulumiwa, wagonjwa na masikini, na kuitetea hoja ya haki.

Kuna sura mbili za maisha ya Bahá'u'lláh ambazo ningependa kuzitaja hasa. Moja ni mateso aliyovumilia. Nyingine ni athari kubwa mno aliyokuwa nayo juu ya mioyo na akili za watu. Hizi kwa kweli huainisha maisha ya Wadhihirishaji wote wa Mungu.

Mateso ya Bahá'u'lláh yalianza pale tu alipoinuka kutangaza Hoja ya Mungu. Maisha Yake yalikuwa yale ya uhamisho, kifungo na mateso. Alifungwa minyororo katika shimo lenye giza na la kusikitisha huko Tehrán. Alihamishwa mara nne kutoka nchi hadi nchi. Katika mojawapo ya Nyaraka Zake uliofunuliwa wakati wa uhamisho wake mrefu, Yeye aliandika:

**"Uzikumbuke siku Zangu maishani mwako, na taabu Zangu na uhamisho Wangu katika gereza hili la mbali. Na uwe thabiti sana katika upendo Wangu kwamba moyo wako hautatetereka, hata kama panga za maadui zitanyesha vipigo juu yako na mbingu zote na nchi vitainuka dhidi yako."**[8]

Bahá'u'lláh hatimaye alipelekwa kwenye Mji—Gereza wa 'Akká katika Milki ya Ottoman. Mateso Yake yalikuwa makali mno hapo kiasi kwamba ameutaja mji wa 'Akká kama "Gereza Kuu Kabisa". Mimi wakati wote nabeba daftari dogo kwenye mkoba wangu ambamo naandika vifungu kutoka maandiko ya Kibahá'í ambavyo hasa vimeugusa moyo wangu. Hebu nikusomee kile ambacho Bahá'u'lláh amesema kuhusu mateso Yake:

**"Uzuri wa Kale amekubali kufungwa kwa minyororo ili jamii ya wanadamu iweze kuachiliwa kutoka kwenye utumwa wake, na amekubali kufanywa mfungwa ndani ya Ngome hii kuu kabisa ili ulimwengu mzima uweze kufikia kwenye uhuru wa kweli. Amekunywa mashinda ya kikombe cha huzuni, ili watu wote wa dunia waweze kufikia kwenye shangwe ya kudumu, na kujazwa na furaha. Hii ni kwa huruma ya Bwana wenu, Mwenye huruma, Mwenye rehema Kabisa. Tumekubali kutwezwa, Enyi waumini katika Umoja wa Mungu, ili muweze kutukuzwa, na tumepata mateso mengi, ili muweze kusitawi na kushamiri. Yeye Ambaye amekuja kuujenga upya ulimwengu mzima, tazama, jinsi wale ambao wamefanya washiriki wa Mungu walivyomlazimisha kukaa ndani ya miji yenye ukiwa kabisa!"**[9]

Kila jitihada ilifanywa na falme mbili zenye nguvu—zile za Mfalme wa Iran na Milki ya Ottoman—kumpinga Bahá'u'lláh na kuzuia kuenea kwa mafundisho Yake. Lakini Mwangaza wa Ukweli hauzimwi kwa urahisi. Maji yenyewe ambayo humiminwa juu ya moto huu ili kuuzima mwale wake hugeuka kuwa mafuta, na moto huo huwaka kwa nguvu zaidi. Hakuna kilichoweza kufanywa kuzuia ushawishi wa Bahá'u'lláh uliokuwa ukiongezeka. Kadiri mamlaka yalivyomhamishia mbali zaidi, ndivyo idadi kubwa zaidi ya watu ilivyovutiwa na mafundisho Yake na kutambua nguvu na ukuu Wake. Licha ya mateso yasiyokoma, Bahá'u'lláh aliendelea kufunua Neno la Mungu kwa zaidi ya miaka arobaini na kuachilia nguvu kubwa mno za kiroho ambazo hatimaye zingeuhuisha ulimwengu mzima.

Bahá'u'lláh alifariki mnamo mwaka 1892. Kaburi Lake Takatifu, ambalo tunalichukulia kama Mahali Patakatifu kabisa duniani, lipo karibu na mji wa 'Akká. Hapa kuna baadhi ya picha za sehemu ya kuingia kwenye Kaburi Takatifu hilo na bustani zinazolizunguka. Hujui jinsi gani ningependa kwenda kuhiji katika Nchi Takatifu. Natumaini, siku moja, utaweza kufanya hivyo pia.

## SEHEMU YA 13

Mazoezi yafuatayo yanachunguza sura mbali mbali za masimulizi ya Anna juu ya maisha ya Bahá'u'lláh:

1. Katika kusimulia hadithi ya maisha ya Bahá'u'lláh, Anna anachagua mawazo makuu mawili ambayo angependa kuyawasilisha. Katika kufanya hivyo, anatoa mada ya kweli kadhaa juu ya maisha Yake, lakini ni dhahiri siyo nia yake kuwasilisha taarifa nyingi sana. Anafahamu kwamba, kama atumainivyo, kama Emilia atakuwa Mbahá'í, atajifunza hadithi ya maisha ya Bahá'u'lláh kwa utondoti zaidi. Ni dhana zipi mbili ambazo yeye anajaribu kuziwasilisha?

   a. ____________________

   b. ____________________

   ____________________

2. Kwa nini unafikiri yeye huchagua dhana hizi mbili? ______________________________

3. Je, unakubaliana naye kwamba dhana hizi ndizo zile mbili muhimu kabisa kwa Emilia kuzielewa katika hatua hii? Kama sivyo, je, una mapendekezo mengine?

4. Tengeneza orodha ya vipengele vya taarifa ambayo Anna huvitoa katika maelezo yake ya maisha ya Bahá'u'lláh.

5. Je, kuna taarifa nyingine yoyote ambayo unafikiria ingekuwa ya lazima iwasilishwe katika hatua hii?

6. Licha ya kujaribu kuwasilisha dhana mbili kuu na habari fulani za lazima, Anna anatumaini kabisa kumwasilishia hisia fulani Emilia. Ni zipi? Je, anafanikiwa?

7. Sasa kwa kuwa umefikiria juu ya uwasilishaji wa Anna juu ya maisha ya Bahá'u'lláh, Je, unafikiri inabidi urekebishwe kama ungekuwa unazungumza na mtu wa usuli tofauti wa kidini au usirekebishwe kabisa? Kama ndivyo, je, unaweza kutoa mifano michache ya mabadiliko ambayo ungeyafanya?

## SEHEMU YA 14

Kusikiliza maneno ya Bahá'u'lláh Mwenyewe juu ya mateso Yake kwa uwazi umemgusa Emilia. Yeye anakumbuka bila shaka, kwamba, Kristo alitoa maisha Yake kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Hivyo marafiki hawa wawili wanazungumza kwa muda fulani juu ya maana ya mateso ya Wadhihirihsaji wa Mungu Ambao, ingawa ni Wenye Uwezo-Kabisa, kwa hiari hukubali mateso ili tuweze kupata uhuru wa kweli. Anna kisha anauliza kama ni sawa kuendelea na anasema kwamba angependa kumtambulisha Mkuu mwingine wa Imani ya Kibahá'í, yaani, Báb. Anaendelea hivi:

> Miaka kadhaa kabla Bahá'u'lláh hajatangaza Dhima Yake, Mungu alimtuma Mjumbe maalum kutangaza ujio Wake. Nafsi hii kuu, Mwenyewe alikuwa Mdhihirishaji wa Mungu na alichukua jina la "Báb" ambalo humaanisha Lango. Yeye kwa kweli alikuwa Lango kwa ujuzi wa Mungu na kwa kipindi kipya katika maisha ya mwanadamu. Kwa miaka sita alifundisha bila kukoma kwamba kujitokeza kwa Yule aliye mkuu kuliko Yeye kulikuwa kumekaribia na aliandaa njia kwa ajili ya ujio Wake. Yeye aliwaambia watu kwamba walikuwa wakishuhudia mapambazuko ya zama mpya, mapambazuko ya Siku Iliyoahidiwa ya Mungu. Aliwasihi watakase mioyo yao kutokana na uchafu wa kidunia ili waweze kumtambua "Yule Ambaye Mungu Angemdhihirisha".
>
> Maelfu kwa maelfu ya watu waliukubali Ujumbe wa Báb na wakuanza kufuata mafundisho Yake. Lakini serikali ya Iran na makasisi wenye nguvu ambao waliutawala umma waliinuka dhidi Yake. Wafuasi Wake waliteswa na idadi yao kubwa waliuawa. Báb Mwenyewe alipokuwa na umri wa miaka 31 aliuawa kishahidi na kikosi cha askari ambao, kwa amri ya serikali, walimning'iniza katika uwanja wa hadhara na kumpiga risasi.
>
> Ili uweze kuona jinsi Maneno ya Báb yalivyo na uwezo wa kupenyeza, ningependa kukutongolea sala Zake mbili:
>
> **"Kuna Muondoa shida yeyote isipokuwa Mungu? Sema: Mungu asifiwe! Yeye ni Mungu! Wote ni watumishi Wake, na wote hutii amri Yake!"**[10]
>
> **"Sema: Mungu hutosheleza vitu vyote juu ya vitu vyote, na hakuna chochote mbinguni au duniani bali Mungu hutosheleza. Kwa kweli, Yeye Mwenyewe Nafsini Mwake ni Mjuzi, Mruzuku, Mwenye Nguvu—Zote."**[11]
>
> Wabahá'í wengi wanaijua hasa sala hiyo ya kwanza kichwani na huitongoa katika nyakati za shida. Kama unataka, tunaweza kusita kidogo hapa na unaweza kuikariri. Kwa kweli ni rahisi kufanya hivyo.

Baada ya kukariri, Anna anaendelea:

> Punde baada ya kuuawa Kwake kishahidi, mabaki ya Báb yaliokolewa na wafuasi Wake na kuhamishwa kutoka mahali hadi mahali, daima yakifichwa kutoka maadui wa Imani. Hatimaye yalihamishwa hadi Mlima Carmel katika Nchi Takatifu. Hapa kuna baadhi ya picha za Kaburi Lake Takatifu huko Haifa ambazo ningependa kukuonesha pamoja na Sehemu zingine chache Takatifu chache katika mji huo na katika mji wa 'Akká, ambao upo upande wa pili wa ghuba. Leo miji hii miwili pacha ndio makao makuu ya kiroho na ya kiutawala ya Imani ya Kibahá'í—makao ya kiroho kwa sababu

ni hapa ndipo Makaburi Matakatifu ya Báb na Bahá'u'lláh, vile vile Sehemu zingine Takatifu yalipo, na makao ya kiutawala kwa sababu juu ya Mlima Carmel ndipo Makao Makuu ya chombo kikuu kabisa cha kiutawala cha Imani, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, yalipo.

## SEHEMU YA 15

Mazoezi ya hapo chini yatakusaidia kufikiria kuhusu sehemu hii ya uwasilishaji wa Anna.

1. Tengeneza orodha ya dhana muhimu na vipengele vya taarifa ambavyo Anna huviwasilisha katika maelezo yake kuhusu maisha ya Báb.

   Dhana: ______________________________

   Taarifa: ______________________________

2. Kwa nini ni muhimu kuutambulisha Utu wa Báb katika hatua ya mwanzoni katika uwasilishaji wa Imani kama ule anaoufanya Anna?

## SEHEMU YA 16

Baada ya kutoa kuelezea kwa ufupi maisha ya Wadhihirishaji Pacha, Anna anaendelea kuongelea juu ya ‘Abdu’l-Bahá na Agano la Bahá’u’lláh:

> Wazo kuu kabisa kwa maisha yetu kama Wabahá’í ni kwamba tumeingia katika Agano na Bahá’u’lláh. Kama ujuavyo, katika dini zingine zote, baada ya kufariki kwa Mdhihirishaji, wafuasi Wake walikuwa na mabishano yasiyokoma miongoni mwao wenyewe na, matokeo yake, waliigawa dini hiyo katika madhehebu mengi. Chanzo cha utengano wakati mwingine kilikuwa ni tamaa ya uongozi kwa baadhi ya watu wenye tamaa. Lakini, pale tofauti za maoni zilipoibuka hata kati ya waumini wanyoofu juu ya maana ya maneno ya Mdhihirishaji, hakuna aliyekuwa ameidhinishwa na Mdhihirishaji Mwenyewe kutuliza mitafaruku hii, na hii ilichangia kwenye ugomvi na marafakano. Kila seti ya ufafanuzi ilisababisha uibukaji wa madhehebu tofauti tofauti.
>
> Bahá’u’lláh ameilinda Imani Yake dhidi ya migawanyiko kama hiyo kwa kuijalia nguvu ya kipekee, Nguvu ya Agano. Kabla ya kufariki Kwake, alisema kwa maneno yaliyo wazi kabisa, kwa maandishi, kwamba baada Yake, Wabahá’í wote sharti wamgeukie ‘Abdu’l-Bahá. ‘Abdu’l-Bahá, Mwanaye mkubwa kabisa wa kiume, hivyo alitajwa kuwa Mfafanuzi pekee wa Neno Lake na Kitovu cha Agano Lake. Yeye alilelewa na Bahá’u’lláh Mwenyewe, alipata kulitambua Daraja Lake angali mtoto mdogo na alishiriki katika mateso ya Baba Yake. Yeye alikuwa zawadi yenye thamani kabisa iliyotolewa kwa wanadamu, Mfano wa kuigwa wa Mafundisho yote ya Kibahá’í.
>
> ‘Abdu’l-Bahá aliishi katika duniani kwa miaka 77. Alizaliwa usiku ule ule Báb alipotangaza Dhima Yake mnamo mwaka 1844 na alifariki mnamo Novemba 1921. Maisha Yake yalijawa na mateso, lakini kila mmoja aliyefika machoni Pake Yeye alimletea shangwe na furaha kuu kabisa. Baada ya kufariki kwa Baba Yake, wajibu kwa jumuiya ya Kibahá’í uliangukia mabega Mwake, na alijishughulisha mchana na usiku kueneza Imani kote Mashariki na Magharibi. Aliandika maelfu ya Nyaraka kwa mtu mmoja mmoja na vikundi kila mahali akifafanua Mafundisho ya Baba Yake. fasiri Zake hivi sasa ni sehemu muhimu ya Maandiko ya Imani ya Bahá’í.

Kwa kumkubali ‘Abdu’l-Bahá kama Kitovu cha Agano, Wabahá’í wa ulimwengu wanabaki wameunganika katika jitihada zao za kuishi maisha ya Kibahá’í na kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii. Tunakumbuka kwamba kama sehemu ya ahadi yetu kwa Bahá’u’lláh, tunaaswa kupendana, na ndani ya ‘Abdu’l-Bahá, tunaona udhihirisho kamili wa upendo. Tunakumbuka kwamba lazima tuitetee haki, kwamba sharti tuwe wakarimu, kwamba sharti tusiangalie makosa ya wengine, na kutoka mfano wa ‘Abdu’l-Bahá tunajifunza haki, ukarimu na usamehevu. Zaidi ya kingine chochote kile, kwa kudumisha umakinifu wetu juu ya ‘Abdu’l-Bahá, daima tunatambua agano letu na Bahá’u’lláh kwamba hatutaruhusu umoja wa wafuasi Wake kuvunjika na kwamba, tukiwa tumeunganika kama jumuiya ya ulimwengu, tutajitoa hadi umoja wa jamii ya wanadamu utakapokuwa umesimamishwa imara.

Katika Wasia na Agano Lake, ‘Abdu’l-Bahá alimtaja mjukuu Wake Shoghi Effendi, Mlinzi wa Imani ambaye baada ya kufariki Kwake, angekuwa mfafanuzi mwenye mamlaka ya maneno ya Bahá’u’lláh. Kwa miaka thelathini na sita, yeye aliendeleza kazi ya Babu Yake, akifafanua mafundisho ya Mdhihirishaji na akiiweka imara Imani Yake katika sehemu zote za sayari. Miaka mitano na nusu baada ya kufariki kwake, Wabahá’í wa ulimwengu walichagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kama ilivyoonwa na Bahá’u’lláh na kuelezewa kwa ufasaha na ‘Abdu’l-Bahá na Mlinzi. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ni asasi kuu kabisa ya Imani ambayo kwayo Wabahá’í wote wa ulimwengu hivi sasa hugeukia.

## SEHEMU YA 17

Yumkini umetambua kwamba sehemu hii ya uwasilishaji wa Anna ni nzito, kwa sababu yeye anamuelezea Emilia kwa maneno machache baadhi ya dhana za ndani kabisa. Zoezi la hapo chini litakusaidia kuchunguza maoni yake kwa utondoti zaidi.

1. Hadi wakati huu, Anna, kufuatana na tamko la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, lililonukuliwa katika Sehemu ya 6, amemzungumzia Emilia juu ya Daraja la Mtangulizi wa Imani, Báb, na Mtunzi wake, Bahá’u’lláh. Sasa anataka kumsaidia Emilia kulitambua Daraja la ‘Abdu’l-Bahá. Ili kufanya hivi, Anna pia hutambulisha dhana ya Agano la Bahá’u’lláh. Anawasilisha kweli kadhaa ili kumsaidia Emilia kupata uelewa kiasi wa dhana hizi mbili zinazohusiana.

   Hapo chini kuna orodha ya baadhi ya kweli hizi. Kila kauli imekusudiwa kuchangia kwenye uelewa wa Emilia wa mojawapo au nyingine ya dhana hizi mbili, au zote. Weka “1” mbele ya zile ambazo unaona kwa kiasi kikubwa zinaimarisha dhana ya Daraja la ‘Abdu’l-Bahá na “2” mbele ya zile ambazo zinaelekea zaidi kwenye dhana ya Agano la Bahá’u’lláh. Kama unaona kauli hiyo inachangia sawia kwenye uelewa wa dhana zote mbili, weka “1” na “2” kando yake.

   ______ Dini zingine zote zimegawanyika katika madhehebu mengi kwa sababu ya kukosekana kwa mfafanuzi dhahiri mwenye mamlaka.

   ______ ‘Abdu’l-Bahá ni Kitovu cha Agano la Bahá’u’lláh.

   ______ ‘Abdu’l-Bahá ni Mfasiri wa Maneno ya Bahá’u’lláh.

______ Uanzishwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ulionwa na Bahá'u'lláh.

______ 'Abdu'l-Bahá alimtaja mjukuu Wake kuwa Mlinzi wa Imani katika Agano na Wasia Wake.

______ 'Abdu'l-Bahá aliandika maelfu ya Nyaraka akifafanua mafundisho ya Imani.

______ Bahá'u'lláh aliilinda Imani Yake kutoka kugawanyika kwa kuijalia Nguvu ya Agano.

______ 'Abdu'l-Bahá ni Mfano wa kuigwa wa mafundisho ya Bahá'u'lláh.

______ 'Abdu'l-Bahá alileta shangwe na furaha kwa kila aliyefika mbele Yake.

______ Bahá'u'lláh alieleza kwa maneno ya wazi kabisa, kwa maandishi, kwamba, baada ya kufariki Kwake, Wabahá'í wote wamgeukie 'Abdu'l-Bahá.

______ Tamaa ya uongozi inaweza kuwa chanzo cha utengano katika dini.

______ 'Abdu'l-Bahá alijishughulisha mchana na usiku kueneza Imani kote Mashariki na Magharibi.

______ Wabahá'í wa ulimwengu walichagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu mapema baada ya kufariki kwa Mlinzi.

______ Kutokuwepo kwa mfasiri mwenye mamlaka katika dini hufungulia mlango kwa ugomvi na mafarakano.

## SEHEMU YA 18

Wakati wa maelezo yake juu ya Agano la Bahá'u'lláh na Daraja la 'Abdu'l-Bahá, Anna alitambua kwamba Emilia alikuwa ameelemewa kidogo. Mara moja alitathmini akilini mwake chaguo la mawazo mawili yaliyo mbele yake: anaweza kujipa muda na kuijadili mada hiyo kwa kina zaidi, au aendelee na uwasilishaji wake na kuhakikisha kwamba, katika mazungumzo mengine baada ya muda mfupi wangeongelea tena mada ya Agano. Yeye huamua juu ya njia ya pili ya utendaji na huendelea hivi:

> Mawazo mengi niliyoyaelezea juu ya mada hii ya mwisho yanahitaji fikra za kutosha. Kama unakubali, wakati mwingine tunaweza kulijadili jambo hili kwa kina zaidi. Kwa majadiliano hayo, nitaleta vifungu vichache kutoka Kitabu cha Agano la Bahá'u'lláh, vile vile Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá ili tuweze kuvisoma pamoja. Lakini acha niendelee kukuwasilishia mawazo mengine machache ambayo ni muhimu kuyajua kuhusu Imani ya Kibahá'í tangu mwanzoni kabisa.

Emilia anakubali na kwa madaha husema kwamba aliyapenda hasa yale maelezo, kwamba amepata kianga kidogo juu ya umuhimu wa Agano la Bahá'u'lláh, na kwamba anasubiri kwa hamu kujifunza zaidi mada hiyo hivi karibuni. Anna, akiwa mwenye furaha na mtulivu, anaendelea:

Muhimu kwa kila dini, ni sheria ambazo Mdhihirishaji huzileta kwa jamii ya wanadamu kwa minajili ya kuiongoza katika njia iliyonyooka. Baadhi ya sheria na amri hizi ni za milele, zingine hubadilika kadiri wanadamu wanavyoendelea na kukua. Katika Imani tunafundishwa kwamba tusifikirie sheria za Kibahá'í kama seti ya kanuni, orodha ya yale yanayopaswa kufanywa na yasiyopaswa kufanywa. Bahá'u'lláh hutuambia kwamba sheria Zake ni "taa za majaliwa Yangu ya upendo miongoni mwa watumishi Wangu, na funguo za rehema Yangu kwa viumbe Vyangu." Wala tusitii sheria hizi kutokana na woga wa adhabu, kwa kuwa Yeye amesema dhahiri katika Kitabu Chake Kitakatifu Kabisa: "Tiini amri Zangu, kwa ajili ya upendo wa uzuri Wangu."

Mawazo haya yatakuwa wazi zaidi ikiwa nitakupa mifano michache ya sheria za Kibahá'í. Katika ulimwengu wa kimwili, wanadamu lazima wale kila siku. Haya ni mahitaji ya mwili wa mwanadamu; tusipokula, tutaumwa na kufa haraka. Hivyo, tunaweza kusema, kwamba kula kila siku ni sheria ya uhai wa kimwili ambayo lazima itiiwe. Vivyo hivyo, mojawapo ya amri za Bahá'u'lláh ni kwamba lazima tusali kila siku. Kama vile mwili wetu, roho yetu inahitaji chakula daima, na sala hutoa chakula kwa ajili ya ukuaji wetu wa kiroho. Kuna sala nyingi nzuri zilizofunuliwa na Báb, na Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá ambazo tunaweza kuzisema tunapokuwa peke yetu au kuzitongoa katika mikutano. Baadhi ya sala ni za faradhi, na pamoja na sala zingine chache maalum, zina nguvu maalum. Mojawapo ya sala za kila siku za faradhi husema:

**"Nashuhudia, Ee Mungu wangu, kwamba Wewe umeniumba mimi kukujua Wewe na kukuabudu Wewe. Nashuhudia, katika wakati huu, juu ya unyonge wangu na uwezo Wako, juu ya umasikini wangu na utajiri Wako.**

**"Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, Msaada hatarini, Ajitoshelezaye Mwenyew."**[12]

Ni sala fupi na nzuri na baada ya kuona jinsi ilivyo rahisi kwako kuzikariri aya hizi, nina hakika utaikariri baada ya kuirudia rudia mara chache.

Katika amri nyingine, Bahá'u'lláh hukataza usengenyaji na uzushi. Hii ni muhimu kwa sababu, kama ukiifikiria, adui mmojawapo mkubwa kabisa wa umoja ni usengenyaji. Na kwa bahati mbaya, imekuwa desturi iliyokithiri miongoni mwa wanadamu wengi sana kuzungumzia makosa ya watu wengine wasipokuwepo. Kila mtu huonekana akijishughulisha na mapungufu ya mtu mwingine, ambayo hufanywa kuwa makubwa zaidi na zaidi kila wakati yanapotajwa. 'Abdu'l-Bahá anatuambia tufanye kinyume kabisa. Tunapaswa kupuuzia kasoro za wengine na kuziona kwa jicho la usamehevu. Tunapaswa tuwapende watu kwa ajili ya Mungu. Kuna mapungufu katika kila mwanadamu, 'Abdu'l-Bahá hutuambia, na daima hatutakuwa wenye furaha kama tukiwatazama watu wenyewe. Lakini tukiwatazama kumuelekea Mungu, tutawapenda na kuwa wema kwao.

Emilia, ambaye anasikiliza kwa umakini maalum maoni ya mwisho ya Anna, anakumbuka matukio ya hivi karibuni shuleni ambapo usengenyaji ulisababisha watu wengi kuumizwa. Marafiki hawa wawili waliongea kwa muda kidogo kuhusu usengenyaji unavyoweza kuharibu urafiki, na halafu Anna anatafuta katika daftari lake na kusoma yafuatayo:

**“Ewe Mwenzi wa Kiti Changu cha Ufalme! Usisikie uovu, na usione uovu, usijishushe, wala kuhema kwa shaka na kulia. Usiseme uovu, ili usiweze kuusikia ukisemwa kwako, na usiyakuze makosa ya wengine ili makosa yako mwenyewe yasije yakaonekana makubwa; na usimtakie fedheha yeyote, ili fedheha yako mwenyewe isije kufichuliwa. Ishi basi katika siku za uhai wako, ambazo ni chache kuliko muda mfupi upitao, ukiwa mwenye akili isiyo na mawaa, moyo wako usio na najisi, mawazo yako safi, na asili yako iliyotakasika ili, ukiwa huru na aliyeridhika, uweze kuliwekea mbali umbo hili la umauti na kwenda kwenye paradiso isiyoelezeka na kuishi katika ufalme wa milele hata milele.”[13]**

Halafu anaendelea:

Bahá’u’lláh pia hukataza unywaji wa pombe na, bila shaka, matumizi ya mihadarati. Unywaji wa pombe kwa kweli ni mojawapo ya maradhi makubwa kabisa ya kijamii yaliyopo ulimwenguni siku hizi. Ni mojawapo ya vyanzo vya kawaida kabisa vya vurugu na uangamizaji wa maisha mazuri ya familia. Kusema ukweli, sielewi kamwe kwa nini watu wangetumia kitu ambacho kinaingilia akili zao na kuwafanya wapoteze uwezo wao kufikiri kwa ufasaha. Unywaji huwafanya watu waweze kutenda mambo ya aibu, wakati kwa kweli tumeumbwa bora. Naijua nukuu nzuri kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh juu ya ubora:

**“Ewe Mwana wa Roho! Nilikuumba tajiri; kwa nini unajishusha kwenye ufukara? Nilikuumba bora, kwa nini unajishusha mwenyewe? Kutoka katika kiini cha maarifa nilikupa uhai, kwa nini unatafuta elimu kutoka kwa mwingine kando Yangu? Kutoka katika udongo wa upendo nilikufinyanga, kwa jinsi gani unajishughulisha na mwingine? Geuzia macho yako kwako mwenyewe, ili uweze kuniona nikisimama ndani mwako mwenye nguvu, mwenye uwezo na ajitoshelezaye.”[14]**

Amri nyingine ya Bahá’u’lláh, ambayo ni mojawapo ya zile ambazo hasa huugusa moyo wangu, ni kuhusu wajibu wa wazazi na jamii kuelimisha watoto. Hapa, katika daftari langu nina kifungu kifupi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá kinachoelezea jambo hili vyema:

**“Kwahiyo, wapendwa wa Mungu na wajakazi wa Mwenye rehema kwa moyo na roho lazima wawaelimishe watoto na kuwafundisha katika shule ya sifa njema na ukamilifu. Lazima wasikubali uzembe wowote katika jambo hili au mapungufu. . . .**

**“ Wajibu wa kwanza wa wapendwa wa Mungu na wajakazi wa Mwenye rehema ni kujitahidi kwa njia zozote zile ziwezekanazo kuelemisha watoto wote, wa kike na wa kiume kadhalika. Kwa kuwa hawa wa mwisho ni sawa na wale wa mwanzo; hakuna tofauti yoyote ile kati yao. Ujinga wa mmojawapo unastahili lawama; na kutotambua kwa mmojawapo kunapaswa kulaumiwa. ‘Je, wale wanaojua na wale wasiojua ni sawa?’”[15]**

Amri hii ni ya muhimu sana kiasi kwamba jumuiya ya Kibahá’í huendesha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto vijijini, kila mahali katika eneo lote. Mimi nasoma kozi inayotolewa na taasisi ya mafunzo ya Kibahá’í ili kunisaidia kujenga uwezo wa kufundisha mojawapo ya madarasa haya, lile ulilonisaidia mara kadhaa sasa.

Kozi za taasisi humfungulia kila anayezisoma njia ya huduma kwa jumuiya yetu, na kama unapenda, naweza kukueleza juu yake wakati mwingine.

## SEHEMU YA 19

Ili kukusaidia kufikiria juu ya mawazo ambayo Anna ameyawasilisha, kamilisha mazoezi hapo chini.

1. Katika sehemu hii ya uwasilishaji wake, Anna anajaribu kufuata mwongozo wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wa kumuarifu mtafutaji juu ya kuwepo wa sheria katika Imani ambazo lazima zifuatwe. Je, unakubaliana na kauli zipi kati ya zifuatazo hapo chini?

______ Kwenye hatua hii, ingekuwa bora zaidi kwa Anna kutolileta suala la sheria kabisa. Katika jamii ya siku hizi, watu huthamini uhuru wao wenyewe binafsi na wazo la "sheria za kidini" huwaondolea shauku.

______ Anna angetaja nyingi mno, kama siyo zote, kati ya sheria za Bahá'u'lláh kwa Emilia, kwa mfano, sheria za mirathi, ndoa, mazishi, na Huqúqu'lláh. Vinginevyo Emilia hatafahamu kikamilifu juu ya kile kinachomaanisha kuwa Mbahá'í.

______ Kile kilicho muhimu kabisa kwa Emilia ni kuelewa ukweli kwamba sheria zipo katika Imani ya Kibahá'í, kuwa na mwanga kidogo juu ya asili ya sheria hizi, na kutambua kwamba, kama Mbahá'í, itambidi azitii. Kwenye hatua hii, hahitaji kujua sheria zote.

______ Kwa makusudi ya Anna, ingetosheleza kutoa mfano wa sheria moja, yaani, sheria ya sala. Amezidisha kiasi kwa kuwasilisha nne.

______ Maelezo ya Anna juu ya sheria ya sala ni yenye ufanisi sana. Kwa kuwasilisha kwanza mojawapo ya sheria inayotawala maisha yetu ya kimwili, Anna anaweza kumuelezea Emilia maana ya sheria zinazotawala maisha yetu ya kiroho. Kwa njia hii hapunguzi sheria za Mungu, kama ilivyozoeleka, kwa seti ya kanuni.

______ Kumzungumzia na mtafutaji juu ya katazo la Bahá'u'lláh juu ya utumiaji wa pombe siyo wazo zuri, hasa kwa kijana ambaye anajitahidi sana kuimarisha uhuru wake na kuonesha kuwa yeye sasa ni mtu mzima. Kijana yeyote kwa kawaida atapenda kujaribu kunywa pombe, na mtajo wowote wa sheria dhidi yake utamsukumia mbali kutoka Imani.

______ Namna Anna anavyowasilisha katazo la Bahá'u'lláh juu ya matumizi ya pombe inafaa. Kwa kuzungumzia juu ya athari ya pombe kwenye akili timamu ya mtu, anaonesha hekima ya sheria hiyo. Aidha, kwa kutambulisha mada ya ubora, yeye huiweka sheria katika muktadha wa juu zaidi wa kiroho.

______ Anna hufanya kosa kwa kutozungumzia kwa uthabiti zaidi juu ya utii kwa sheria za Bahá'u'lláh. Kwa kweli, angelileta suala la vikwazo vya kiutawala ili Emilia aweze kujua matokeo ya kutotii.

______ Wakati hatilii mkazo suala kuhusu utii kwa sheria za Bahá'u'lláh, Anna kwa uwazi anamfikishia Emilia wazo kwamba utii hutiririka kutokana na upendo wa Mungu na siyo kutokana na kuoga adhabu. Wakati Emilia atakapokuwa Mbahá'í, kutii sheria kutakuwa ni matokeo ya kawaida ya upendo wake kwa Bahá'u'lláh.

______ Kama ulikuwa unamfundisha mtu ambaye ana tatizo la unywaji wa pombe, ingekuwa muhimu kabisa kwako kumuelezea sheria inayokataza utumiaji wa pombe. Katika suala hili, bila shaka, ingekubidi umuambie kwamba kama akiwa Mbahá'í, ingempasa aache kunywa mara moja.

______ Kama ulikuwa unamfundisha mtu ambaye ana tatizo la unywaji wa pombe, ingekuwa muhimu kabisa kwako kumuelezea sheria inayokataza utumiaji wa pombe. Walakini, ukitambua tatizo lake, ungeweza kumuelezea kwamba ingekuwa sawa kwake kuendelea kunywa baada ya kuwa Mbahá'í, maadam hakuna mtu anayemuona.

______ Kama ulikuwa unamfundisha mtu ambaye ana tatizo la unywaji wa pombe, ingekuwa muhimu kwako kumuelezea katazo la Bahá'u'lláh juu ya utumiaji wa pombe, sambamba na sheria zingine. Pia ungemwambia kwamba siyo rahisi wakati wote kufuata kila sheria; sisi si wakamilifu na mara nyingine tunafanya makosa. Lakini tunapomkubali Bahá'u'lláh, na kadiri tunavyomuomba, Yeye Mwenyewe hutusaidia kushinda udhaifu wetu na hutupa nguvu kutii sheria Zake.

2. Mathalani unamfundisha mtu ambaye ana shida ya kumuamini Mungu. Je, bado ungemuwasilishia sheria ya sala? Kama ndivyo, jinsi gani ungefanya hivyo?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 20

Mazungumzo ya mwanzoni ya Anna na Emilia juu ya Imani yanakaribia mwisho. Emilia ameonesha kuvutiwa mno katika uwasilishaji wa Anna, na hili limemtia moyo kuelezea mawazo fulani kwa utondoti kiasi. Sasa lazima ahitimishe maoni yake:

> Nina hakika unatambua kwamba ninakualika kujiunga na dini na siyo tu kukubali makusanyo ya mawazo mazuri. Kwa kweli, Imani ya Kibahá'í ni dini yenye utaratibu mzuri sana ambayo waumini wake wanafanya kazi kiutaratibu kutumia mafundisho ya Bahá'u'lláh katika maisha yao wenyewe na katika maisha ya jamii. Itakusaidia kufikiria juu ya kazi hii kama ujengaji wa ustaarabu wa ulimwengu. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutuambia kwamba kuna washiriki watatu katika jitihada hii, kila mmoja akiwa na kazi muhimu sana.
>
> Mshiriki wa kwanza ni muumini binafsi. Ni wajibu wa mtu huyu binafsi kubakia thabiti katika Agano, kujitahidi kila siku kupatanisha maisha yake na mafundisho ya Kibahá'i, na kuitumikia jamii ya wanadamu, daima akitambua ukweli kwamba maisha hayaishii na kifo na kwamba uhusiano wa mtu na Mungu ni wa milele. Baada ya kifo, roho zetu huendelea kwenda mbele kumuelekea Mungu milele na milele. Maisha yetu hapa ni sawa kabisa na maisha ya mtoto mchanga katika tumbo la uzazi la mama. Kwa miezi ipatayo tisa mtoto hukuza viungo—macho, masikio, mikono na kadhalika—ambavyo vingetumika baadaye katika ulimwengu huu. Vivyo hivyo, hapa tunapaswa kukuza viungo vya kiroho ambavyo tutavihitaji kwa ajili ya kuendelea katika malimwengu mengine ya Mungu. Bila shaka, hatutimizi kusudi letu kwa kulifikiria tu. Bali, ni katika uga wa huduma, kadiri tunavyofanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa jamii, ndivyo tukuavyo kiroho na kiakili.
>
> Mshiriki wa pili ni jumuiya. Mwanadamu hakuumbwa kuishi peke yake. Tunaishi katika jumuiya na lazima tufanye kazi pamoja kuujenga ule ustaarabu mpya. Jumuiya iliyo karibu kabisa nasi ni ile ya mahali ambayo hujumuisha Wabahá'í wa kijiji au mji wetu. Walakini haidhuru wapi tunaishi, kila mmoja anaalikwa kujiunga na jitihada zetu za kujenga uwezo kwa ajili ya huduma na kuchangia katika maendeleo ya ujirani na vijiji vyetu. Ni katika jumuiya ya mahali kwamba, kwa pamoja na marafiki na majirani ambao hufanya kazi sambamba nasi, tunajifunza kushirikiana mmoja kwa mwingine, kuendelea kwa pamoja na kuwa kitu kimoja. Zaidi ya kuwa wana-jumuiya wa jumuiya ya mahali, sisi pia ni wana-jumuiya wa jumuiya ya kitaifa na kisha wana-jumuiya wa jumuiya ya Kibahá'í ya ulimwengu, ambayo inaendelea kupanuka na kuwavutia watu kutoka usuli wa kila dini, taifa, tamaduni, mbari na kabila.
>
> Asasi za Imani, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutuambia, huwakilisha yule mshiriki wa tatu katika ujenzi huo wa ustaarabu mpya. Hii ni mada ambayo tutaizungumzia zaidi kidogo zaidi tutakapokuwa tunajadili kuhusu Agano. Kwa sasa, hebu nitaje tu zile zilizomo katika amri za Bahá'u'lláh ambazo nyingi zinahusiana na jinsi jamii

inavyopaswa kusimamiwa. Katika nyakati zilizopita, Wadhihirishaji wa Mungu hawakusema mengi juu ya jinsi wafuasi wao wanavyotakiwa kujisimamia wenyewe, na watu iliwabidi wagundue jinsi ya kufanya hili wao wenyewe. Lakini, katika Imani ya Kibahá'í, tuna baraka ya Utaratibu wa Kiutawala uliowekwa kiutakatifu, maana yake ni kwamba Bahá'u'lláh Mwenyewe ametuambia ni asasi zipi inatubidi kuziunda, jinsi gani zinavyopaswa zifanye kazi, na jinsi gani jamii ya wanadamu inavyopaswa kujitawala.

Tayari tumezungumzia kuhusu asasi kuu kabisa, ambayo ni Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Katika kila nchi, Wabahá'í huchagua mara moja kwa mwaka Baraza la Kiroho la Kitaifa, na katika kila eneo, Baraza la Kiroho la Mahali. Hii ni asasi ambayo utaifahamu hivi punde. Hakuna wachungaji wala makasisi katika Imani ya Kibahá'í, na ni Baraza la Kiroho la Mahali ambalo huongoza shughuli za jumuiya na kulinda usitawi wa waumini wake mmoja mmoja. Baraza la Kiroho la Mahali lina wajumbe tisa wanaochaguliwa katika hali ya ibada kwa kura za siri na waumini wote watu wazima katika jumuiya. Mabaraza ya Kiroho ni muhimu sana kwa Wabahá'í. Kupitia kwayo tunajifunza jinsi shughuli za wanadamu zinavyopaswa kusimamiwa na jinsi utaratibu mpya unavyoweza kusimamishwa katika jamii.

Tunaweza kufikiria kwamba mazungumzo kati ya Anna na Emilia yanafikia mwisho hapa. Emilia kwa udhahiri ana shauku kuendelea na majadiliano siku nyingine. Anna anachukua kitabu kidogo cha sala kutoka kwenye mkoba wake na kumpa Emilia kama zawadi, akipendekeza wasome sala pamoja kabla ya kuachana. Emilia anafungua kitabu na kusoma:

**"Umba ndani mwangu moyo msafi, Ee Mungu wangu, na fanya upya dhamiri tulivu ndani mwangu, Ee tumaini langu! Kupitia roho yenye nguvu Unithibitishe katika Hoja Yako, Ee Mpendwa wangu kabisa, na kwa nuru ya utukufu Wako unifunulie njia Yako, Ewe Lengo la haja yangu! Kwa kupitia nguvu ya uwezo Wako mkuu kupita kiasi uniinue hadi kwenye mbingu ya utakatifu Wako, Ee Chanzo cha uhai kwangu, na kwa pepo nyanana za umilele Wako unifurahishe, Ewe Ambaye ni Mungu wangu! Acha lahani Zako za milele zipulizie utulivu juu yangu, Ee Mwenzi wangu, na acha utajiri wa Wajihi Wako wa kale uniokoe kutoka vyote isipokuwa Wewe, Ee Bwana wangu, na acha habari za ufunuo wa Asili Yako isiyoharibika, ziniletee shangwe, Ewe Ambaye u mwenye kudhahiri kabisa kati ya waliodhahiri na aliyefichika kabisa kati ya waliofichika!"[16]**

Ingawa maelezo tuliyotoa kuhusu Anna na Emilia siyo halisi, imejikita juu ya tajiriba ya maelfu ya Wabahá'í kote ulimwenguni. Kama mwisho wa hadithi, hivyo, tunaweza kusema kwa imani kwamba, katika siku chache na baada ya maongezi mengine mara moja au mbili, Emilia atajiunga na jumuiya ya Kibahá'í, na kuanza, kwa msaada wa Anna, kutembea katika njia ya huduma kwa Hoja.

## SEHEMU YA 21

Hebu tutathmini uwasilishaji wa Anna kwa jumla kupitia mazoezi mawili yafuatayo:

1. Mawazo ambayo Anna anashiriki na rafiki yake, hasa katika maoni yake ya kuhitimisha, yatakuwa na athari kubwa juu ya jinsi Emilia anavyoyaona majukumu

yake kama muumini binafsi wa jumuiya, ushiriki wake katika shughuli zake, na uhusiano wake wa baadaye na asasi za Imani.

Ni taswira gani ya muumini binafsi Anna anajaribu kuiwasilisha? Ni zipi baadhi ya sifa bainifu za mtuhuyu?

Ni taswira gani ya jumuiya ya Kibahá'í Anna anajaribu kuiwasilisha? Ni zipi baadhi ya sifa zake bainifu?

Ni taswira gani ya asasi za Kibahá'í Anna anajaribu kuiwasilisha? Ni zipi baadhi ya sifa zake bainifu?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

2. Kwa wakati wote, Anna kwa udhahiri anajaribu kufungua mlango kwa Emilia kujiunga na jumuiya ya Kibahá'í. Ni yapi kati ya yafuatayo ungefikiria ndio msukumo hasa wa ombi lake?

______ Kwamba Wabahá'í ni watu wazuri na jumuiya ya Kibahá'í imeunganika, kwa hiyo natumaini utajiunga nasi.

______ Kwamba Imani ya Kibahá'í ina kanuni endelevu kabisa za kiroho na kijamii na maadamu unazikubali, wewe ni Mbahá'í.

______ Kwamba kwa utangulizi mfupi ambao nimekupa, sasa unahitaji kufanya uchunguzi wa kina wa Imani ya Kibahá'í na halafu uamue kama utakuwa Mbahá'í au la.

______ Kwamba kutokana na niliyokwishasema, na baadhi ya ufafanuzi zaidi nitakaokupa, kuhusiana na maswali yoyote unayoweza kuwa nayo, natumaini utatambua kwamba Bahá'u'lláh ni Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku hizi na kuona haja ya kuwa mmoja wa wafuasi Wake waaminifu.

## SEHEMU YA 22

Uwasilishaji tuliouchunguza katika kurasa hizi, ambao unafuata kwa mapana tamko la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika Sehemu ya 6, unaeleza seti yenye nguvu ya mawazo kuelezea vipengele muhimu vya Imani ya Kibahá'í kwa mtu anayejua kidogo kuhusiana nayo, lakini ambaye ana shauku ya kujifunza zaidi. Tumefanya uchunguzi huu katika muktadha wa jitihada za ufundishaji binafsi, katika mazungumzo kati ya marafiki wawili. Kwa kawaida, hali ambamo tunajikuta wenyewe hutofautiana, na utapaswa kuwa umejiandaa katika juhudi zako zote za ufundishaji ziendane na uwasilishaji wako kwa hali maalum—kwa kiwango cha upokevu wa wale ambao unakutana nao, kwa kiwango cha ujuzi wao wa Imani na ushirikiano wao na jumuiya ya Kibahá'í, na kwa usuli wao mahususi. Hivyo, ingawa unahamasishwa kujifunza vyema uwasilishaji wa mawazo ambayo Anna anashiriki na Emilia, bado muhimu zaidi ni kwa wewe kutathamini mantiki iliyomo. Ni kwa jinsi hii tu kwamba utaweza kuchota kutoka humo kwa urahisi, jizuie msukumo wa kuugeuza kuwa fomyula, na kuirekebisha kufuatana na hali.

Itakusaidia kusita kidogo hapa na kutafakari juu ya kile kinachohitajika. Tangu ulipoingia katika njia ya huduma iliyofunguliwa na kozi hizi, umejenga kwa uthabiti uwezo uhitajikao kwa ajili ya kuongea na wengine kuhusu mafundisho ya Kibahá'í na kuhusu Mtunzi wake. Sasa unaombwa kusonga mbele zaidi na kujenga uwezo wa kufanya uwasilishaji wenye mantiki wa Imani ambao unajibu upokevu na shauku za wale ambao unawajua au unaokutana nao katika mazingira anuwai. Mazoezi yaliyotolewa sanjari na uwasilishaji katika kitabu hiki yalikusudiwa kukusaidia kufikiria kuhusu asili ya uwezo huu na kile kitakachohitajika kutoka kwako. Pengine ungependa kuandika mawazo yako machache ya awali hapo chini.

## SEHEMU YA 23

Kama ulivyoona kwa hakika hapo juu, uwezo unaoongelewa unakuzwa ugani kwa utendaji na huongezeka wakati hadi wakati kadiri mtu anavyofundisha Imani kwa watu wengi zaidi na zaidi. Sawa na Anna katika hadithi yetu, sisi sote tuna marafiki na ndugu, wafanyakazi-wenza na wana-rika-wenza, ambao, kila mmoja kwa namna yake mwenyewe, hutafuta ukweli, na baadhi watapenda kuchunguza ujumbe wa Bahá'u'lláh katika mazungumzo yanayowasilisha mafundisho Yake kwa njia yenye mantiki na ya moja kwa moja. Tunaweza kufanya mazungumzo kama hayo na wale watu ambao tumekutana nao hivui punde kama sehemu ya kampeni ya pamoja ndani ya kundi pokevu katika kijiji au ujirani wetu. Kuhusu hili la pili, tunapaswa tukumbuke mwongozo ufuatao kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu:

> **" Kama kukutana kwetu kwa mara ya kwanza na wale marafiki waliopatikana hivi karibuni kutahitaji mwaliko kwa wao kujiandikisha katika jumuiya ya Kibahá'í au kushiriki katika mojawapo ya shughuli siyo jambo la kuhofia sana. Muhimu zaidi ni kwamba kila roho ijihisi kukaribishwa kujiunga na jumuiya katika kuchangia kwenye uboreshaji wa jamii, kwa kuanza njia ya huduma kwa jamii ya wanadamu ambao juu yao, tangu mwanzoni au baadaye zaidi, uandikishaji rasmi unaweza kutokea."**[17]

Kile tunachopaswa kukumbuka, basi, ni kwamba miongoni mwa wale wanaofanya kazi sanjari nasi katika jitihada zetu za kujenga jumuiya, au kuwasasaidia kwa njia tofauti, ni wale ambao, kwanza wanasukumwa na shauku ya kuitumikia jamii ya wanadamu, na sasa wapo tayari kunywa kwa kina zaidi kutoka Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Kuhusiana na hili, Nyumba ya Haki huandika:

**"Bila shaka, jumuiya hukaribisha kiwango chochote cha ujihusishaji ambacho mtu angependa kukidumisha, kiwe kikubwa au kidogo. Bado kumtambua Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu na kupata manufaa na majukumu ambayo kipekee yanahusiana na ufuasi katika jumuiya ya Kibahá'i ni tukio moja katika maendeleo ya kiroho ya mtu, tofauti kabisa na ushiriki wa mara kwa mara katika shughuli za Kibahá'i au kuunga mkono kanuni za Kibahá'i. Tajiriba imeonesha kwamba mazingira yaliyotengenezwa na jitihada za ujengaji wa jumuiya katika eneo humwezesha yeyote anayependa kupiga hatua hii kufanya hivyo kwa urahisi zaidi. Popote ambapo jitihada hizi zinaendelea, ni muhimu kwa marafiki kuwa makini kwamba milango ya Imani ipo wazi kabisa na kuwatia moyo wale ambao husimama kizingitini. "[18]**

Hivyo, iwe katika jitihada ya ufundishaji wetu binafsi au katika shughuli za pamoja, tunapaswa kuwa tayari kufanya aina ya mazungumzo ya wazi yaliyoonwa hapo juu, yale ambayo yatatumika kuwahamasisha wale waliosimama kwenye kizingiti chake kuingia katika ngome ya Hoja na kuchota nguvu kutoka nguvu iunganishao ya Agano.

## SEHEMU YA 24

Tumesema kwamba kwa jumla kuna miktadha miwili ambamo tunajihusisha katika kitendo cha kufundisha: katika jitihada zetu binafsi na katika kampeni za pamoja. Tutaichunguza miktadha hii miwili, kwa zamu, katika sehemu kadhaa zitakazofuata. Hebu tuanze kwa kufikiria kuhusu jitihada zetu binafsi za ufundishaji. Tayari unaifahamu nukuu hiyo hapo chini kutoka masomo yako ya kozi za awali lakini sasa unaombwa kutafakari juu ya maana yake kwa karibu zaidi, kwa kuwa kutoka humo tunaweza kubuga kanuni za kiroho ambazo zinaunda msingi wa kila mpango binafsi wa ufundishaji.

**"Ewe msafiri katika njia ya Mungu! Twaa sehemu yako ya bahari ya neema Yake, na usijinyime mwenyewe vile vitu ambavyo vimefichwa katika vina vyake. Uwe miongoni mwa wale ambao wameshiriki katika hazina zake. Tone la umande kutoka bahari hii, kama lingemwagwa juu ya vile vyote viliyomo mbinguni na duniani, lingetosheleza kuwatajirisha kwa fadhili za Mungu, Mweza, Mjua—Vyote, Mwenye Hekima—Kabisa. Kwa mikono ya kujikana teka kutoka maji yake yatiayo uhai, na unyunyizie kwayo viumbe vyote, ili viweze kutakaswa kutoka vizuizi vyote vya kibinadamu na viweze kukaribia kiti chenye nguvu cha Mungu, Mahali hapa pang'aapo na kutukuzwa.**

**"Usihuzunike ikiwa utaifanya wewe pekee yako. Acha Mungu awe atoshelezaye vyote kwako. Zungumza na Roho Yake kwa ukaribu kabisa, na uwe miongoni mwa wale wenye shukurani. Tangaza Hoja ya Bwana wako kwa wote walioko mbinguni na duniani. Kama mtu yeyote akiitika mwito wako, muwekee wazi mbele yake lulu za hekima za Bwana, Mungu wako, ambazo Roho Yake imekushushia, na uwe miongoni mwa wale ambao kwa kweli huamini. Na ikiwa yeyote ataikataa zawadi yako, geukia mbali kutoka kwake, na weka tumaini na imani yako kwa Bwana, Mungu wako, Bwana wa malimwengu yote."[19]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Lazima tutwae ______________ yetu ya bahari ya ___________________ .

   b. Kwa mikono ya _________________ , lazima tuteke kutoka _________________ yake __________________ .

   c. Tunapaswa tunyunyizie ____________________________________ kwa maji yatiayo uzima ya neema ya Mungu.

   d. Hatupaswi _______________ ikiwa tutaifanya kazi hii ____________ .

   e. Tunapaswa _____________________________________ na Roho Yake.

   f. Tunapaswa kuwa miongoni mwa wale __________________ .

   g. Tunapaswa _________________ Hoja ya Bwana wetu kwa wote walioko mbinguni na duniani.

   h. Ikiwa mtu yeyote angeitika mwito wetu, tunapaswa _____________________ mbele yake ______________________________________ za Bwana.

   i. Ikiwa yeyote ataikataa zawadi yetu ________________ kutoka kwake, na kuweka _______________________________________ yetu kwa Mungu.

2. Inamanisha nini kutwaa sehemu yetu ya bahari ya neema ya Mungu? _____________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

3. Ni vipi baadhi ya vitu ambavyo vimo ndani ya vina vya bahari hii na ambavyo, vikigunduliwa, vingetuwezesha kufundisha Hoja kwa ufanisi uongezekao daima? ___
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

4. Je, tone moja la bahari ya neema ya Mungu linaweza kufanya nini? ______________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

5. Je, kwanini lazima tutumie “mikono ya kujikana” kuteka kutoka maji yatiayo uzima ya bahari hii? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

6. Je, tufanye nini na maji tunayoyateka kutoka bahari ya neema ya Mungu? __________

______________________________

______________________________

7. Je, unyunyiziaji huu utakuwa na athari gani? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

8. Je, wakati wote lazima tufundishe Imani kwa msaada wa Wa-Bahá’í wengine? ______

9. Je, tunamhitaji yeyote isipokuwa Mungu tunapotangaza na kufundisha Hoja? ________

10. Je, tuzungumze na nani tunapotangaza na kufundisha Hoja? ____________________

11. Je, kwa kipi inatubidi tuwe wenye shukurani tunapotangaza na kufundisha Hoja? _____

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

12. Je, tumtangazie nani Hoja? ______________________________

______________________________

______________________________

13. Je, tunatakiwa kumfundisha nani? ______________________________

14. Je, tufanye nini kama ujumbe tunaoutoa unakataliwa? __________________________

______________________________

______________________________

15. Je, tunapoambiwa kwamba tugeukie mbali kutoka wale wanaoukataa ujumbe humaanisha tusiwe na urafiki nao tena? Au humaanisha tu kwamba tusisisitize kuwafundisha Imani?

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

16. Hapo chini kuna virai vichache kuhusu ufundishaji. Amua vipi vinapatana zaidi na kifungu cha hapo juu kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh. Viwekee alama.

_____ Niliamua kwamba mtu ambaye ningemfundisha ni rafiki yangu wa karibu sana, Miguel. Hivyo kwa miaka mitano iliyopita, nimekuwa nikikazia juhudi zangu juu yake tu. Hashawishiki vyema, lakini siku fulani atashawishika. Kimsingi, huo ndio mpango wangu binafsi wa ufundishaji.

_____ Nafikiria kwamba ni wajibu wetu kuitangaza Imani kwa watu. Halafu ni shauri yao kama wanapenda kuichunguza zaidi. Kama kweli wanataka, wanaweza kuomba kitabu cha kusoma ili waweze kuamua wao wenyewe.

_____ Jana, nilikuwa naelezea ujumbe wa Bahá'u'lláh kwa mmoja wa majirani zangu wakati tulipokuwa tunakunywa kahawa pamoja. Baada ya muda alisema kwamba, ingawa aliheshimu shauku yangu, alikuwa ameridhika na dini yake. Lakini alisema hivyo kwa namna ambayo ilikuwa dhahiri kwamba alikuwa hafungi mlango kwa mazungumzo ya siku zijazo juu ya Imani. Hivyo tutakapokutana tena baadaye, nitajaribu kubaini baadhi ya vipemgele vya mafundisho vitakavyomvutia na kumfanya amsogelee kwa karibu zaidi Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii.

_____ Kwa sababu tu mtu mmoja ananiambia kwamba hana shauku ya kusikia kuhusu Imani, haimaanishi kwamba ni lazima iwe hivyo. Mimi nasisitiza tu.

_____ Kama mtu anajua kwamba mimi ni Mbahá'í lakini haniulizi maswali yoyote juu ya Imani, ina maana kwamba yeye hana shauku.

_____ Ikiwa mtu anayefanya kazi sambamba nami katika shughuli za kujenga jumuiya hajawahi kuniuliza kuhusu jinsi gani mtu anavyoweza kujiandikisha katika Imani, humaanisha kwamba yeye hataki kufanya ahadi ya kiroho ya kumkubali Bahá'u'lláh.

_____ Najaribu kukutana na watu wengi kadiri iwezekananvyo na, fursa inapotokea, nashiriki nao baadhi ya mafundisho ya Imani. Kama nikiwaona wapokevu, naendelea kuwafundisha hadi hatimaye niweze kuwaalika kujiunga na Imani.

## SEHEMU YA 25

Katika *Majilio ya Haki Takatifu*, Mlinzi ameandika kifungu ambamo kwa ufasaha anaelezea vipengele vya kimsingi vya mpango wa ufundishaji wenye utaratibu wa mtu binafsi. Kifungu hicho kimegawanywa katika sehemu fupi fupi hapo chini. Soma kila kimoja na kisha jaza sehemu zilizo wazi katika sentensi zinazofuata.

**"Kwa ari yake mwenyewe, na bila kutishwa na vipingamizi ambavyo kwavyo rafiki au adui wanaweza, pasipo kujua au kwa makusudi, kuzuia njia yake, ameazimia kuinuka na kuitika mwito wa ufundishaji, mwache afikirie kwa uangalifu kila njia ya uendeaji ambayo yeye angeweza kuitumia katika jitihada zake za binafsi za kuteka hisia, kudumisha shauku, na kuimarisha imani, ya wale ambao yeye anataka kuwaingiza katika zizi la Imani yake. Mwache achunguze fursa ambazo mazingira maalum ambamo yeye huishi humpa, atathmini manufaa yake, na aendelee kiakili na kiutaratibu kuyatumia kwa ajili ya utimizaji wa lengo alilonalo akilini."[20]**

1. Mlinzi hutuambia kwamba lazima, kwa ___________________ yetu wenyewe, tunuie ___________ na ______________ mwito wa ________________ .

2. Katika kufanya hivyo, hatupaswi kuruhusu vipingamizi ambavyo _________________ au _________ huweza, _______________________ , au _____________________ kuviweka katika njia yetu kutuondoa kutoka kusudi letu.

3. Thabiti katika azma yetu, lazima tufikirie kwa uangalifu ________________________ ya ________________ ambayo tungeweza kuitumia katika jitihada zetu binafsi za kuteka __________________ , kudumisha ________________ , na kuimarisha ____________ ya wale ambao tunataka kuwafundisha Imani.

4. Thabiti katika azma yetu, lazima kwa uangalifu _________________ kila njia ya uendeaji ambayo tungeweza __________________ katika jitihada zetu binafsi ____________ hisia, _________________ shauku, na _______________ imani ya wale ambao tunataka kuwafundisha Imani.

5. Tunaambiwa ______________________ fursa ambazo ___________________ maalum ambamo tunauishi hutoa.

6. Tunapaswa __________________ manufaa ya fursa zilizo mbele yetu.

7. Baada ya kuweza kufanya hivyo, sharti tuendelee _______________ na ___________ _____________________________________________________________________ .

**"Mwache pia ajaribu kubuni njia kama vile ushirikiano na vilabu, maonesho, na vyama, mihadhara juu ya mada zinazoebdana na na mafundisho na kanuni bora za Hoja yake kama vile ukadirifu, uadilifu, ustawi wa jamii, stahamala ya kidini na ya kimbari, ushirikiano wa kiuchumi, Uislamu, na dini linganishi, au ushiriki katika mashirika ya kijamii, kiutamaduni, kibinadamu, kihisani, na kielimu na shughuli ambazo, wakati zinalinda uadilifu wa Imani yake, zitamfungulia njia na nyenzo nyingi ambapo anaweza kujipatia kwa mfuatano huruma, msaada na hatimaye uaminifu wa wale ambao yeye hukutana nao."[21]**

8. Tunapaswa pia tujaribu kufikiria njia kama vile ushirikiano na ________________ , ________________________ , na ____________________ , ________________ juu ya mada zinazopatana na ___________________ na ______________ ya Hoja.

9. Aidha, tunapaswa tujaribu kutafuta njia za kushiriki katika mashirika ya ___________ , __________________ , _________________________ , ____________________ , na __________________________________________ na _________________ , ambapo siku zote _______________________ uadilifu wa Hoja.

10. Tunapaswa kufanya hivi ili wingi wa _______________________ zitafunguliwa kwetu ambapo tunaweza kuwaandikisha kwa mfuatano ______________________ , _____________ , na hatimaye __________________ wa wale ambao tunakutana nao.

**"Mwache, wakati mawasiliano kama hayo yakifanywa, akumbuke madai ambayo Imani yake daima hufanya juu yake kuhifadhi heshima yake, na daraja, kulinda uadilifu wa sheria na kanuni zake, kudhihirisha ukamilifu wake na ujumuishaji wa wote, na kutetea bila woga raghba zake nyingi na muhimu. Mwache afikirie kiwango cha upokevu cha msikilizaji wake, na ajiamulie yeye mwenyewe ufaaji wa ama njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja ya ufundishaji, ambayo kwayo anaweza kumvutia mtafutaji kwenye umuhimu mkuu wa Ujumbe Mtakatifu, na kumshawishi kujiunga na wale ambao tayari wameukubali."**[22]

11. Tunapokuwa tunafanya mawasiliano kama hayo, kamwe tusisahu wajibu wetu wa _______________ heshima ya Imani , _________ uadilifu wa _________________ na ________________ , ________________ ukamilifu wake na _______________ , na _______________ bila woga ____________ zake nyingi na ____________________ .

12. Mlinzi hutuambia kwamba lazima tufikirie kiwango cha ___________________ cha msikilizaji wetu, na tujiamulie wenyewe __________________ wa njia ya ___________________ au isiyo ya ______________________ ya ufundishaji.

13. Katika kuchagua njia mojawapo, lazima tukumbuke kwamba kusudi letu ni _________ _______________ mtafutaji ________________________________ wa Ujumbe Mtakatifu na ______________________ na wale ambao tayari wameukubali.

**"Mwache akumbuke mfano uliowekwa na 'Abdu'l-Bahá, na onyo Lake la mara kwa mara kummiminia wema mwingi mno mtafutaji, na kuonesha mfano wa kiwango cha juu kabisa cha ile roho ya mafundisho ambayo yeye hutumaini kuingiza ndani mwake, kiasi kwamba mpokeaji huyo kwa hiari yake mwenyewe atasukumwa kujitamulisha mwenyewe na Hoja yenye mafundisho kama hayo. Mwache ajizuie, tangu mwanzoni, kusisitizia sheria na kanuni kama zile ambazo zinaweza kutwisha mkazo mkali mno juu ya imani ya mtafutaji iliyoamshwa hivi karibuni, na kujitahidi kumlea, kwa subira, kwa busara, na lakini kwa**

**kudhamiria, kwenye ukomavu kamili, na kumsaidia kutangaza kukubali kwake kikamilifu chochote kile kilichoamriwa na Bahá'u'lláh."[23]**

14. Katika jitihada zetu za ufundishaji, lazima tukumbuke _________________ uliowekwa na 'Abdu'l-Bahá na onyo Lake la mara kwa mara la _________________ mtafutaji ____________________ na kujitahidi _________________ cha ______________ ya mafundisho ambayo tunatumaini kuingiza ndani mwake.

15. Tunapaswa kuwa wenye hadhari mno katika kufuata mfano wa 'Abdu'l-Bahá kwamba mtafutaji ________________________________________ kujitambulisha na Hoja.

16. Baada ya kumleta mtafutaji kwenye Imani, tunapaswa kuwa waangalifu mwanzoni _____________________ kama zile zinazoweza _____________________ juu ya imani yake iliyoamshwa hivi karibuni.

17. Tujitahidi ________________ , kwa subira, kwa busara, na lakini kwa kudhamiria, kwenye _____________________ , na __________ kutangaza _________________ ____________________ kwake kikamilifu wa chochote kile ___________________ na Bahá'u'lláh.

18. Sharti tumlee, ______________________ , _____________________ na lakini ________________________ , kwenye ukomavu kamili, na kumsaidia ____________________ kukubali kwake kikamilifu chochote kile kilicho amriwa na Bahá'u'lláh.

**"Mwache, mara tu hatua hiyo imefikiwa, amtambulishe kwa waumini wenzake, na kutafuta, kupitia undugu endelevu na ushiriki amilifu katika shughuli za eneo za jumuiya yake, kumwezesha kuchangia sehemu yake kwenye usitawishaji wa maisha yake, uendelezaji wa kazi zake, uimarishaji wa raghba zake, na uratibu wa shughuli zake pamoja na zile za jumuiya mwenza."[24]**

19. Mara tu mtafutaji amefikia hatua hii, sharti ___________________ kwa wana-jumuiya wengine wa jumuiya.

20. Kuanzia hapo na kuendelea sharti tutafute, kupitia ________________________ ______________________ na _______________________________________ katika _________________________ za jumuiya, kumwezesha ________________________ sehemu yake kwenye _______________ wa maisha yake, ____________________ wa kazi zake __________________ wa raghba zake, na ____________________________ wa shughuli zake za na jumuiya mwenza.

**"Mwache asiridhike mpaka yeye ameingiza ndani mwa mtoto wake wa kiroho shauku ya ndani kabisa kiasi cha kumsukuma kuinuka kwa kujitegemea, na kwa**

**zamu yake, kujitoa nguvu zake kwa ajili ya uhuishaji wa roho zingine, na utetezi wa sheria na kanuni zilizowekwa na Imani yake aliyoikubali hivi karibuni."[25]**

21. Mlinzi hutuambia kwamba tusiridhike mpaka _______________ ndani mwa wale tunaowafundisha _____________ ya ndani kabisa kiasi cha _____________ kuinuka _________________________ na _________________ , __________________ zao kwa ajili ya ufundishaji wa roho zingine na kutetea sheria na kanuni za Imani.

## SEHEMU YA 26

Ukiwa na vifungu kutoka sehemu mbili zilizotangulia akilini, sasa unaombwa kuelekeza fikra zako katika kutengeneza mpango wako binafsi wa ufundishaji wenye mpangilio. Kama hatua ya kwanza, utahitaji kufikiria kuhusu jinsi vipengele vilivyoainishwa na Shoghi Effendi vitakavyotumika katika mpango wako. Mazoezi hapa chini yatakusaidia kufanya hivi.

1. Ni wazi kwamba, kipengele muhimu cha mpango wako binafsi wa ufundishaji ni azma yako isiyoyumba ya kufanya jitihada madhubuti kuzipata roho pokevu na kuzifundisha. Wakati wowote tunapoamua kuweka ahadi thabiti ya kufanya jambo fulani, azma yetu inajaribiwa. Vikwazo bila kuepukika huibuka. Katika suala la ufundishaji, baadhi ya vikwazo viwekwavyo njiani mwetu hutokana na upinzani kwa Imani au hali ya ulimwengu unaotuzunguka. Kwa mfano, uyakinifu katika jamii unaweza kufanya jitihada zetu za kufundisha ziwe ngumu zaidi, kama vile utepetevu wa jumla wa watu kwenye masuala ya kiroho. Ni vipi baadhi ya vikwazo vinavyoibuka kutokana na hali ya ulimwengu ambavyo unaweza kukumbana navyo unapokwenda kufundisha?

   a. ____________________________________________
   b. ____________________________________________
   c. ____________________________________________
   d. ____________________________________________
   e. ____________________________________________
   f. ____________________________________________

2. Baada ya kudhamiria kuinuka na fundisha Imani, utahitaji kufikiria kuhusu hali yako na hali ya maisha yako mwenyewe. Bila shaka, kuu miongoni mwa haya yote ni ushiriki wako katika shughuli za kujenga jumuiya katika kijiji au ujirani wako, na tayari tumeshaonesha kwamba hili litakufungulia fursa za ufundishaji. Lakini, mbali na hili, fikiria sura zingine za maisha yako. Andika aya fupi inayoeleza haya. Mathalani, je, wewe ni mwanafunzi, mzazi, babu au bibi? Kazi yako ni ipi, au unajipatiaje riziki? Unashirikiana na vikundi na mashirika gani, ni aina gani ya watu unaokutana nao kila suiku?

   ____________________________________________
   ____________________________________________

Ukiwa na hayo hapo juu akilini, andika fursa mbalimbali zilizopo katika maisha yako kwa ajili ya ufundishaji wenye mpangilio:

3. Mbali na fursa ambazo umezibaini hapo juu, kama kipengele kimoja cha mpango wako binafsi wa ufundishaji, utahitaji kubuni njia mbalimbali ambazo utaweza, wakati ukilinda uadilifu wa Imani, mara kwa mara ukikutana na watu wapya, ambapo baadhi yao watathibitisha kuwa wapokevu kwa ujumbe wa Bahá'u'lláh. Kwa mfano, ungeweza kujiunga na shirika ambalo shabaha zake zinapatana na mafundisho. Ikiwa unaishi karibu na kituo cha kielimu, unaweza kuhudhuria mihadhara juu ya mada zinazohusiana na mafundisho na kanuni za Hoja. Kipengele hiki cha mpango wako ni muhimu sana kwa sababu, kama hauendelei kukutana na watu wapya, utaishia kuelekeza nguvu zako zako kwa watu wale wale wachache mwaka hadi mwaka ambapo wengi wao inawezekana hata wasiwe wapokevu. Andika baadhi ya njia ambazo unaweza kutumia kukutana na watu wengi zaidi na zaidi.

4. Kama ulivyoona, kupitia fursa zote ulizoziona katika Mazoezi ya 2 na ya 3, ili uweze kukutana na idadi iongezekayo ya watu, utahitaji kufikiria kuhusu jinsi utakavyofanya shabaha za Ufunuo wa Bahá'u'lláh zijulikane kwao, kwa namna ya busara na staha. Ambapo kwa hakika watapata vianga vidogo vya uzuri wa mafundisho Yake kupitia vitendo vyako, utapenda kutafuta fursa zinazofaa kujadili vipengele mbalimbali vya Imani pamoja nao. Kutoka ujifunzaji wako wa kitengo cha pili cha Kitabu cha 2, "Mazungumzo Yainuayo", na tajiriba inayofuata, unajua jinsi ya kuendesha mazungumzo kama hayo. Wakati unatafakari juu ya kipengele hiki cha mpango wako, ingekusaidia kuzingatia vikundi tofauti vya watu ambao utakutana nao. Jinsi gani unaweza kufikisha shabaha na maadili bora ya Hoja kwenye fikra za wale waliopo katika kila kikundi kwa ufanisi zaidi? Ni wazi kwamba, utaweza tu kuandika mawazo yako ya awali hapa, kwa kuwa utajua tu kwa uhakika kile unachopaswa kuwaambia watu pale unapokuwa katika hali halisi. Aidha, mawazo yako yataendelea kukua kadiri unavyopata tajiriba.

5. Wakati unaendelea kufanya shabaha na maadili bora ya Hoja kujulikana kwa watu wengi zaidi na zaidi, utaanza kuwafundisha wale ambao unaona kuwa wapokevu. Jinsi unavyoamua kuendelea itategemea na mazingira yenyewe. Pamoja na baadhi, kama alivyofanya Anna na rafiki yake Emilia, unaweza kuamua kama ingefaa kuwasiilisha mambo muhimu ya Imani kinagaubaga na kwa uwazi. Pamoja na wengine, unaweza kuendelea kujihusisha na mazungumzo, kwa mfano, katika mazingira ya fayasaidi ya mara kwa mara. Bado wengine unaweza kuwaalika kwenye mkutano wa ibada katika kijiji au ujirani wako. Halafu watakuwepo wale ambao tayari wameshajidhatiti kwa muono wa Bahá'u'lláh wa utaratibu mpya wa ulimwengu, na wanahitaji tu uhamasaji wako wa upendo. Katika hali zote hizi, bila shaka, utaendelea kugeukia kwa Mungu, ukimuomba kuzileta roho unazozifundisha katika hifadhi ya Hoja Yake. Shabaha yako itamsaidia kila mmoja wao kupata uelewa wa kina zaidi wa mafundisho ya Bahá'u'lláh. Na pale wanapomtambua Yeye kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii na kujiunga na safu za wafuasi Wake, utahitaji kuwasaidia katika jitihada zao za kuongeza ujuzi wao na kuitumikia Hoja Yake—hili, kama imani yao waliyoipatikana hivi karibuni itazihimili nguvu za mmomonyoko wa kimaadili unaoendelea kufanya kazi katika jamii. Orodhesha mambo ambayo ungeweza kufanya ili kusaidia kuwalea kwa namna hii.

## SEHEMU YA 27

Baada ya kubaini vipengele vya mpango binafsi wa ufundishaji, pengine sasa ungependa kufanya mpango wa kwanza wa utendaji wa kipindi maalum, ama majuma kadhaa au miezi michache. Mpango wako utakuwa wenye msaada mkubwa zaidi kama ni mahsusi, ukitaja majina ya watu unaowafahamu na kuonesha hatua thabiti unazotaka kuchukua. Kadiri unavyofuatilia mpango wako, ndipo, fursa mpya zitakapoibuka na uhusiano utakuwa, na utaweza kubuni hatua mpya ipasavyo.

## SEHEMU YA 28

Bila shaka kama ulivyoona wakati wa kufikiria kuhusu vipengele vya mpango wako binafsi wa ufundishaji na kutengeneza mpango wa awali wa kiutendaji, aghalabu jitihada zetu

binafsi za ufundishaji hufumwa katika ruwaza ya shughuli inayoendelea kukunjuka katika vijiji na ujirani wetu. Vile vile uliona, jinsi jitihada binafsi kama hizi huchangia na kuimarisha ruwaza hii. Lakini ili ruwaza ya ukuaji katika jumuiya iweze kuchapuzwa—la, kupanuka kwa mapana—kampeni za pamoja zinahitajika. Ili kushiriki ipasavyo katika kampeni kama hizo tunahitaji kukuza uelewa dhahiri wa maana ya utendaji wa pamoja. Hebu tufikirie, kwa mfano, kisa kifuatacho:

Mathalani unashiriki katika mkusanyiko ambamo marafiki kutoka vijiji na ujirani kadhaa vya karibu wamekuja pamoja kupanga kampeni ya ufundishaji ulioitishwa na Kamati ya Ufundisha ya Eneo. Mkutano huo unafanyika katika mazingira ya kiroho, mazungumzo machache yenye mguso juu ya umuhimu wa ufundishaji na wajibu wa mtu binafsi hutolewa, na msisimko mkubwa hufanyizwa. Mazungumzo yanapotamatika wale kutoka kila kijiji au ujirani hushauriana kama kikundi juu ya mipango ya kampeni ya ufundishaji. Baada ya muda, vikundi vyote huja pamoja kushiriki mipango yao. Mwakilishi kutoka kikundi kimojawapo hutoa muhtasari wa matunda ya ushauriano huo kwa maneno haya: “Mpango tulioubuni kuchangia katika kampeni hii ni wa wazi kabisa. Unahitaji kwamba kila mtu kusali kila siku ili wafanikiwe angalu mara moja katika ufundishaji, kwamba angalau kila mtu aitaje Imani kwa angalau mtu moja kila siku, na kwamba kila familia iwe na fayasaidi angalau moja kila baada ya siku kumi na tisa.”

Hebu tudhani kwamba marafiki kutoka kikundi hiki huupeleka mpango huo hadi kwenye kijiji au ujirani wao. Bila shaka kama kila mmoja akiinuka kufuata mapendekezo ya kikundi kwa dhati na shauku, tunaweza kutarajia kwamba jumuiya itashuhudia ukuaji wa yote mawili kiidadi na kiuwezo, ikijiandaa kuanza hata shughuli kubwa zaidi. Hata hivyo, ili kuongeza uelewa wetu wa mada hii, ingefaa kutafakari kama mpango kama huo unaendana na mawazo yetu yote juu ya utendaji wa pamoja wenye mpangilio. Je, mpango huu unahusisha zaidi ya kuwahamasisha watu binafsi kufuata jitihada zao wenyewe za ufundishaji binafsi, yumkini kwa shauku iongezekayo inayotokana na ufahamu kwamba watu wengine pia wanahusika katika aina hiyo hiyo ya shughuli? Je, utendaji wao wa pamoja haupaswi kubuniwa kwa namna ambayo vipaji na uwezo wa watu binafsi huimarishana, na hivyo kuzidisha uwezo wao? Je, utendaji wao wa pamoja kama kikundi cha watu usingeleta matokeo mengi zaidi kuliko jitihada zao zote zilizotawanyika za mtu mmoja mmoja? Tafakari juu ya maswali haya pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako.

## SEHEMU YA 29

Majadiliano ya maswali ya hapo hapo juu kwa hakika yamethibitisha kile ambacho tayari ulikuwa umeshaanza kukielewa kutokana na tajiriba yako mwenyewe. Bila shaka umeona, kama sehemu ya kiini kipanukacho cha watu binafsi wanaofanya kazi pamoja katika kijiji au ujirani, jinsi, kwa nguvu za utendaji wa pamoja, uwezo wetu unavyoongezeka. Shabaha yetu katika sehemu iliyobaki ya kitengo hiki itakuwa kujaribu kupata baadhi ya umaizi wa utekelezaji huu katika muktadha wa upanuzi na uimarishaji wa Imani.

Kwanza, hebu tupitie kwa haraka kile ambacho huenda unakijua hadi sasa kuhusu uendeaji wetu kwenye ukuaji wa Imani kote ulimwenguni. Katika wakati huu, jitihada za kuchapuza mchakato wa ukuaji kwa kiasi kikubwa zinafanyika katika ujirani au vijiji maalum ndani ya klasta. "Klasta" humaanisha eneo dogo la kijografia lenye ukubwa unaoweza kusimamiwa kwa urahisi kwa makusudi ya kupanga mipango. Kamati ya Ufundishaji ya Eneo hufanya kazi kwenye ngazi hii. Ndani ya mazingira ya klasta, tunahamasishwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kushughulika katika "maduru ya miezi mitatu mitatu ya shughuli ambazo kupitia humo jumuiya hukua—mlipuko wa upanuzi unaoonekana kama matokeo ya utendaji shadidi; kipindi muhimu cha uimarishaji wakati ambapo ongezeko la safu huimarishwa kadiri wao, kwa mfano, wanavyoshiriki katika mikusanyiko ya ibada na Karamu ya Siku Kumi na Tisa na kupokea wageni katika kaya zao; na fursa zilizokusudiwa kwa ajili ya wote kutafakari na kupanga."

Maduru, hivyo, yanaweza kuainishwa kwa awamu zinazofuatana za upanuzi, uimarishaji, na tafakari na upangaji mipango. Kila duru hujenga juu ya mafanikio ya lile lililotangulia. Kadiri watu wengi zaidi na zaidi wanavyoingia katika mchakato wa taasisi baada ya kila wimbi la upanuzi, uwezo wa pamoja huongezeka kadiri wanavyoanza kuweka katika vitendo kile wanachojifunza. Seti ya shughuli zinazoshabihiana, za msingi kwa ajili ya mchakato wa ukuaji—mikusanyiko ya ibada, madarasa ya watoto, vikundi vya vijana chipukizi, na vikundi vya mafunzo—matokeo yake hupanuka, na kiini kikuacho cha wasaidizi amilifu wa Imani kinaweza kuongeza mwendo wa jumlla wa shughuli. Mchakato wa ukuaji huchapuzwa zaidi kwa namna hii.

Awamu ya upanuzi hudai kiwango cha juu kabisa cha ushadidi, aghalabu kinachopatikana kupitia utekelezaji wa kampeni za pamoja. Malengo yake yatatofautiana kutegemea na hali ndani ya klasta, kama ilivyotajwa hapo juu. Wakati mwingine, kampeni inaweza kulenga kuongeza idadi ya washiriki katika shughuli moja au zingine za msingi. Wakati mwingine, shabaha inaweza kuwa ufundishaji wa moja kwa moja. Aghalabu jitihada hizi za pili, zikifanyika katika eneo ambako shughuli zinaanza kubumba maisha ya jumuiya, huhusisha kuwaita watu katika kaya zao. Kuhusana na kampeni za aina hii, Nyumba ya Haki ya ulimwengu hutoa mwongozo ufuatao:

> **"Kwenye kiini cha suala hili, hivyo, ni jinsi kampeni ya ufundishaji Imani kwa kuzitembelea kaya inavyohusiana na shughuli zingine zinazofanyika katika ujirani—jinsi inavyoshabihiana na jitihada za kuendesha mikutano inayoimarisha tabia ya kiibada ya jumuiya pana zaidi, kuendesha madarasa yanayokuza maendeleo ya kiroho ya watoto, kuunda vikundi vinavyoelekeza nguvu za vijana chipukizi, kuanzisha vikundi vya mafunzo, wazi kwa wote, ambavyo huwawezesha watu wa usuli tofauti tofauti kupiga hatua sawa na kuchunguza utumiaji wa mafundisho katika maisha yao binafsi na ya pamoja."**[26]

## SEHEMU YA 30

Kama ilivyopendekezwa katika nukuu hapo juu, tusifikirie kwamba kampeni za kufundisha zinafanyika katika ombwe. Zinaunda kipengele kimoja tu cha mbinu yetu ya ukuaji. Juhudi zaidi katika upanuzi na uimarishaji wa Imani wa kiwango kikubwa huwa na mafanikio zaidi pale zinapofanyika kiutaratibu na kwa kipindi kirefu miongoni mwa kundi maalum.

Katika kitengo hiki, tumetaja istilahi "kundi pokevu" kama mara mbili hivi. Tajiriba imeonesha kwamba, kama vile watu binafsi, baadhi ya makundi yanaweza kuwa tayari zaidi kuliko mengine kuchunguza athari za Imani kwa maisha yao ya pamoja. Upokevu kama huo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutuambia kuwa, aghalabu "hujidhirisha wenyewe katika ridhaa ya kushiriki katika mchakato wa ujenzi wa jumuiya ulioanzishwa na shughuli za msingi." Katika kila klasta, kazi iliyopo mbele ya marafiki ni:

> **"Kufundisha ndani ya idadi moja au zaidi ya makundi pokevu, kwa kutumia njia ya moja kwa moja katika uelezaji wao kinaganaga wa kanuni za kimsingi za Imani yao, na kuzipata zile roho zenye shauku ya kujivua utepetevu uliotwishwa juu yao na jamii na kufanya kazi sambamba mmoja kwa mwingine katika ujirani na vijiji vyao kuanzisha mchatao wa mabadiliko ya pamoja."[27]**

Kinachoongelewa hapa ni mjongeo wa watu kuelekea muono wa Bahá'u'lláh wa utaratibu mpya wa ulimwengu na ustaarabu wenye usitawi na upatano. Ili kutafakari zaidi juu ya umuhimu wa mchakato huu unaofanyika katika klasta kote duniani, soma dondoo zifuatazo kutoka ujumbe ulioandikwa na Nyumba ya Haki:

> **"Pale umma wa jamii ya wanadamu unapoamshwa na kuingia katika Imani ya Mungu, mchakato mpya huanzishwa na ukuaji wa ustaarabu mpya huanza. Shuhudia uibukaji wa Ukristo na wa Uislamu. Umma huu ni watu wa kawaida, waliozama katika mila zao, lakini ambao ni wapokevu kwa Neno jipya la Mungu, ambalo kwalo, wanapolipokea ipasavyo, wanakuwa wenye kuathiriwa mno kiasi cha kuwabadilisha wale wanaokutana nao.**
>
> **"Viwango vya Mungu ni tofauti na vile vya wanadamu. Kulingana na viwango vya wanadamu, kukubaliwa kwa hoja yoyote na watu wenye vyeo, wenye umaarufu na hadhi inayotambulika, huamua thamani na ukuu wa hoja hiyo. Lakini, katika maneno ya Bahá'u'lláh: 'Miito na Ujumbe Tulioutoa kamwe haukukusudiwa kuifikia au kuinufaisha nchi moja au watu wa aina moja tu. Jamii ya wanadamu kwa ujumla wake sharti itii kwa uthabiti chochote kile ambacho kimefunuliwa na kukabidhiwa kwake.'"[28]**

Kuhusu asili ya mchakato wa mabadiliko ambayo yanayokunjuka katika klasta kila mahali, tunasoma yafuatayo katika ujumbe mwingine ulioandikwa na Nyumba ya Haki:

> **"Wakisukumwa na nguvu zinazofanyizwa kote ndani na nje ya jumuiya ya Kibaha'i, watu wa dunia wanaweza kuonekana wakijongea kutoka sehemu tofauti tofauti kuja karibu zaidi na zaidi mmoja kwa mwingine, kuelekea kile kitakachokuwa ustaarabu wa ulimwengu wenye tabia ya kustaajabisha sana kiasi kwamba ingekuwa ni kazi bure kwetu kujaribu kuufikiria kwa wakati huu. Kadiri kani hii ya mjongeo wa watu inavyochapuzwa kote ulimwenguni, baadhi ya vipengele katika kila utamaduni, ambavyo haviendani na mafundisho ya Imani, pole pole vitaachwa kando ambapo**

**vingine vitaimarishwa. Vile vile, vipengele vipya vya utamaduni vitaendelea kukua kipindi hadi kipindi kadiri watu kutoka kila kundi la wanadamu wanavyovuviwa na Ufunuo wa Baha'u'llah, kudhihirisha ruwaza za fikra na vitendo vinavyoletwa na mafundisho Yake . . . "**[29]

1. Kulingana na nukuu ya pili hapo juu, jibu maswali hapo chini.

   a. Nini hutokea pale umma wa jamii ya wanadamu unapoamshwa na kuingia katika Imani ya Mungu? ______________________________________________

   ______________________________________________

   b. Ni badiliko gani hutokea katika umma pale wanapolipokea ipasavyo Neno jipya la Mungu? ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   c. Kifungu hiki kinaelezaje tofauti kati ya viwango vya Mungu na viwango vya wanadamu? ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

2. Kulingana na nukuu ya tatu hapo juu, amua ipi kati ya kauli zifuatazo ni kweli:

   _____ Ili kujongea karibu zaidi kwenye ustaarabu wa ulimwengu uliotazamiwa katika maandiko, kila kila kundi la watu linahitaji kuchukua vipengele vya utamaduni mmoja unaotawala.

   _____ Kila utamaduni ulimwenguni hujumuisha vipengele ambavyo hustahili sifa, na vipengele ambavyo ingekuwa bora zaidi kuviondoa.

   _____ Kiwango cha kile ambacho ni sahihi na kile kisichohitajika katika utamaduni wowote ni Ufunuo wa Bahá'u'lláh.

   _____ Haikubaliki kwa kikundi cha watu, kwa jina la utamaduni, kuwachukulia wanawake kama duni kuliko wanaume.

   _____ Vipengele vya utamaduni wowote ule ambao husisitiza juu ya ushirikiano vinapaswa kuthaminiwa na kupendwa.

   _____ Vile vipengele vya utamaduni ambavyo hustahili sifa huchangia kuongeza anuwai na uzuri wa familia nzima ya mwanadamu.

_____ Vipengele visivyokubalika vya utamaduni vinatakiwa kubadilika kadiri vinavyo angazwa na mwangaza wa mafundisho ya Imani.

_____ Hakuna chochote kinachochekesha kuhusu mzaha na maneno ambayo kwa namna moja au nyingine hubeza kikundi chochote cha watu; hayo hasa ni mabaki ya kuanzia utoto wa jamii ya wanadamu ambayo hayana budi kutupiliwa mbali.

_____ Kundi fulani la watu linapojiiunga na Imani, pole pole litaacha vile vipengele vya utamaduni wake ambavyo haviendani na mafundisho.

_____ Kundi fulani la watu linapojiiunga na Imani, vile vipengele vya utamadunii vinavyoendana na mafundisho, vitakaziwa na kuimarishwa.

_____ Kila kundi la watu, kwa wakati muafaka, litajitwalia vipengele vipya vya utamaduni vinavyovuviwa na Ufunuo wa Bahá'u'lláh—mathalani, vile ambavyo huakisi umuhimu unaowekwa juu ya kuelimisha vizazi vichanga.

_____ Kadiri watu wanavyokaribia zaidi na zaidi kwenye bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh, bila kuepukika watakaribiana mmoja kwa mwingine.

_____ Makundi anuwai ya watu hatimaye yatakaribiana zaidi mmoja kwa mwingine kadiri kila moja linavyofuatilia njia zake za ukuaji, iwe yanafuata mafundisho ya Bahá'u'lláh ama la.

_____ Ushiriki wa idadi kubwa zaidi na zaidi katika shughuli za msingi ndani ya kundi pokevu unaanzisha mchakato wa mabadiliko ambao utawaleta karibu zaidi na zaidi na muono wa utaratibu mpya wa Bahá'u'lláh.

Kulingana na hapo juu, fikiria juu ya tajiriba yako mwenyewe katika klasta ambamo unaishi. Tangu umeanza kutembea njia ya huduma, umechangia kwenye kuimarisha na kupanua seti moja ya shughuli zinazoshabihiana—hili, iwe miongoni mwa wakazi wa kijiji chako au miongoni mwa kundi maalum katika eneo fulani la ujirani wako au waliosambaa kila mahali katika klasta. Fikiria shughuli hizi katika ujumla wake na mchakato wa mabadiliko waliouanzisha. Elezea jinsi mjongeo wa watu unavyoanza kufanyizwa kadiri kiini kikuacho ambacho wewe ni sehemu yake kinavyojifunza kufanya yafuatayo kwa namna ya iliyounganika; kukuza tabia ya kiibada ya jumuiya; kusaidia kuwawezesha vijana chipukizi wengi zaidi na zaidi kiroho na kiakili; kuwaalika vijana wengi zaidi na zaidi kutembea njia ya huduma, kuwapa msaada katika safari yao, kuwapa elimu ya kiroho watoto wengi zaidi na zaidi; kuwezesha familia nyingi zaidi na zaidi za watoto na vijana kujifunza kuhusu mafundisho na jinsi ya kuyatumia maishani mwao.

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 31

Sasa kwa kuwa umetafakari juu ya jinsi jitihada za kiini kinachoendelea kupanuka cha marafiki katika kijiji au ujirani wako kinavyofanyiza mjongeo wa watu kuelekea muono wa Bahá'u'lláh wa utaratibu mpya wa ulimwengu, hebu tuchunguze hali ambazo zinafanikisha utendaji kama huo wa pamoja. Utakubali kwamba sharti la kwanza linalotakiwa kufikiwa ni umoja. 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Ikiwa kweli ninyi mmeunganika, ikiwa ninyi mnakubali kuendeleza kile ambacho ni kusudi muhimu, na kudhihirisha upendo uunganishao vyote, naapa kwa Yule Ambaye husababisha mbegu kupasuka na upepo mwanana kuvuma, ni mkubwa mno mwangaza utakaong'aa kutoka nyuso zenu hata kufika kwenye mbingu za juu kabisa, umaarufu wa utukufu wenu utatangazwa kila pahali, shuhuda za ukuu wenu zitaenezwa kila mahali katika maeneo yote, nguvu yenu itapenyeza katika uhalisia wa vitu vyote, shabaha na makusudi yenu yatakuwa na ushawishi juu ya mataifa makubwa na yenye nguvu, roho zenu zitauzingira ulimwengu mzima wa kuwa, na ninyi mtajigundua wenyewe kuwa wafalme katika milki za ufalme, na kuvikwa mataji matukufu ya Milki isiyoonekana, na kuwa majemadari wa jeshi la amani, na wana-mfalme wa majeshi ya mwangaza, na nyota zing'aazo kutoka upeo wa ukamilifu, na taa angavu zikitawanya nuru juu ya wanadamu."[30]**

Kuwa tuliounganika mno kiasi kwamba nguvu zetu huzidishwa, kama ilivyoelezwa hapo juu na 'Abdu'l-Bahá, siyo hali tunayoipata kwa mkupuo. Inahitaji jitihada ya kila siku. Haidhuru tunajifunza vyema namna gani kupanga na haidhuru tunakuwa mahiri jinsi gani katika kutekeleza mipango yetu, itazaa matunda machache sana ikiwa tutaruhusu mafarakano hata kidogo au shida kunyemelea ndani.

Vyanzo vya mafarakano kwa kawaida ni vya kipuuzi na mara chache daima husababishwa na kijicho. Mara nyingi, migogoro huibuka kwa sababu mtu mmoja ya kukosa subira na mapungufu ya mwingine au kusisitizia juu ya kufanya kile anachotaka yeye. Tiba ni ukarimu na uwezo wa kuvishinda vitu vidogo-vidogo vya maisha. 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Sasa ni wakati, Enyi wapendwa wa Bwana, kwa ajili ya jitihada yenye shauku. Jitahidini, na jibidiisheni. Na maadam Uzuri wa Kale alikabiliana mchana na usiku kwenye uwanja wa kifo cha kishahidi, hebu kwa wakati wetu tufanye kazi kwa kujikalifu, na kusikia na kutafakari mawaidha ya Mungu; hebu tutupilie mbali maisha yetu, na tuzikane siku zetu fupi na chache. Hebu tugeuzie macho yetu mbali kutoka njozi tupu za sura tofauti tofauti za ulimwengu huu, na tulitumikie badala yake kusudi hili adhimu kabisa, mpango huu mkuu. Hebu, kwa sababu ya mawazo yetu wenyewe, tusiukate mti huu ambao mkono wa neema ya mbinguni umeupanda; hebu tusifutilie mbali, kwa mawingu ya giza ya mauzauza yetu, maslahi yetu ya kibinafsi, utukufu ambao humiminika kutoka**

**Milki ya Abhá. Hebu tusiwe kama vizuizi ambavyo huizuilia nje bahari isukasukayo ya Mwenyezi Mungu. Hebu tusiyazuie manukato safi na mazuri kutoka bustani ya Uzuri Mtukufu Kabisa kuvuma kwa marefu na mapana. hebu, tusizuie, katika siku hii ya kuunganika tena, mmiminiko wa baraka za msimu wa machipuko kutoka juu. Hebu tusiridhie kwamba wangavu wa Jua la Ukweli daima utafifia na kutoweka. Haya ndiyo maonyo ya Mungu, kama yalivyoandikwa katika Vitabu Vyake Vitakatifu, Maandiko Yake Matakatifu, Nyaraka Zake, ambavyo huzungumzia mawaidha Yake kwa wanyofu.**

**"Utukufu uwe kwenu, na rehema ya Mungu, na baraka za Mungu."[31]**

Mlinzi husema:

**"Kazia macho yako juu ya fursa zenye nguvu, baraka zisizopimika, moyo usioshindika wa Imani hii ikuayo na inayokakamka ya Mungu, na usiruhusu ugomvi mdogo mdogo na tofauti zisizoepukika za wakati huu kutia giza uoni wako wa utukufu mwangavu ambao wakati ujao wa Hoja umehifadhi kwa ajili ya wasaidizi wake thabiti na shujaa."[32]**

Kukariri na kuzingatia vifungu kama cha hapo chini kutatusaidia kuchangia katika umoja wa jitihada zetu za pamoja.

**"Kama tofauti zozote huibuka miongoni mwenu, nitazameni Mimi nikiwa nimesimama mbele yenu, na msameheane makosa ya mmoja kwa mwingine kwa ajili ya jina Langu na kama dalili ya upendo wenu kwa Hoja Yangu iliyo dhahiri na angavu. Sisi tunapenda nyakati zote kuwaona mkipatana kwa urafiki na maelewano ndani ya Paradiso ya ridhaa Yangu njema, na kuvuta kutoka matendo yenu manukato ya urafiki na umoja, ya wema wa upendo na undugu. Hivyo ndivyo awashaurivyo yule Ajuaye—Yote, Mwaminifu. Wakati wote tutakuwa nanyi; kama tukivuta marashi ya undugu wenu, moyo Wetu kwa hakika utafurahia, kwani hakuna kingine kinachoweza kuturidhisha Sisi. Kwa hili kila mtu mwenye uelewa wa kweli hushuhudia."[33]**

Umoja ni rahisi zaidi kuudumisha pale kila mmoja anapotambua maana ya kazi inayohitaji kufanyika na ukuu wa malengo yanayotakiwa kufikiwa. Pale uelewa kama huo unapokuwepo, watu hawatapata shida sana kuweka kando tofauti zao na bila ubinafsi kujitoa kikamilifu kwa kazi iliyo mbele yao. Sita kidogo na ufikiri: Je, ungekubali kuudhuru mchakato ambao hatma yake ni kuzileta karibu korija za roho zinazongojea kuukaribia Ufunuo wa Bahá'u'lláh kwa alili ya mojawapo ya sababu zifuatazo:

_____ Kwa sababu haupo tayari kusamehe vitendo vya mwingine?

_____ Kwa sababu unajidhughulisha na kasoro zako mwenyewe?

_____ Kwa sababu hutaki kufuata njia ya kiutendaji ambayo kila mmoja ameikubali?

_____ Kwa sababu unaamini wewe mwenyewe kuwa upo sahihi na kila mmoja mkosefu?

_____ Kwa sababu unapenda kuongea mizaha kila fursa inapojitokeza, hata kama haifai na huwafanya wengine wajisikie vibaya?

______ Kwa sababu unang'ang'ania kukosoa kila mapungufu unayoyaona, bila kujali jinsi kitendo hicho kinavyoathiri shauku ya kikundi?

______ Kwa sababu hauthamini hitaji la ushadidi katika jitihada ya pamoja?

______ Kwa sababu mtu mmoja alikusemesha kwa namna ambayo hukuipenda?

______ Kwa sababu hujisikii vizuri kuwatembelea watu katika kaya zao?

______ Kwa sababu hujafurahi kwamba vipaji vyako maalum havijatumika?

## SEHEMU YA 32

Umoja uliopo miongoni mwa wajumbe wa kiini cha marafiki waliojitoa kufanya kazi katika kijiji au ujirani haufungiwi ndani ya undugu wa upendo unaowaunganisha. Unajidhihirisha wenyewe katika ufasaha wanaoshiriki kuhusu kusudi lao la pamoja. Umoja wa kusudi ni sharti lingine la lazima kwa ajili ya utendaji wa pamoja; hutoa mwelekeo kwa jitihada zetu, siyo tu tunapokuwa tunafanya kazi pamoja bali pia tunapokuwa tunafanya vitendo binafsi vya huduma, kama vile uendeshaji wa darasa la watoto au kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi. Unaenea katika kila kitu tunachokifanya na kuvipa vitendo vyetu maana. Tunaona jinsi jitihada zetu binafsi zinavyofumwa pamoja na shughuli za pamoja kuunda ruwaza changamfu ya shughuli ambazo huwasukuma watu kwenda mbele. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu husema:

> **"Jumuiya inatumikia zaidi na zaidi kadiri yale mazingira ambamo jitihada binafsi na utendaji wa pamoja, vikisimamiwa na taasisi, vinaweza kukamilishana baina yao ili kupata maendeleo. Upumaji huu unaodhihirishwa nao na umoja huu wa kusudi unaohuisha jitihada zake unawachota katika safu zake zinazoendelea kutuna kutoka kila nyanja ya maisha wale wenye shauku ya kutoa muda na nguvu zao kwa ajili ya usitawi wa jamii ya wanadamu."**[34]

Hisia hii ya kusudi moja, kwa hiyo, huenda mbali zaidi ya ngazi ya mahali. Tunatambua jinsi jitihada zetu kama sehemu ya kiini kinachoendelea kupanuka katika kijiji au ujirani wetu kuchangia kwenye kusudi kubwa zaidi la kuendeleza kazi ndani ya klasta ambamo tunaishi. Tunaona, kwa upande wake, jinsi hili linavyoongeza maendeleo ya jumuiya yetu ya kitaifa na ukunjukaji wa Mipango ya kiulimwengu ya Imani, ambayo hatimaye itasababisha uibukaji wa utaratibu wa ulimwengu wa Bahá'u'lláh.

1. Kwa nini ni muhimu kutambua kwamba kazi yetu katika ujirani au kijiji huchangia katika kusudi kubwa zaidi? ______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

2. Tutahakikishaje kuwa shabaha na kusudi binafsi huenda sambamba na malengo ya Imani? ______________________________
______________________________

3. Jinsi gani jitihada zetu binafsi na shughuli za pamoja, zinazosimamiwa na taasisi, zinavyokamilishana? Kwa nini uelewa wa ukamilishanaji wake ni wa lazima kwa utendaji wa pamoja?

4. Jinsi gani umoja wa kusudi unavyoimarisha mafundo ya upendo miongoni mwa marafiki wanaohudumu pamoja?

## SEHEMU YA 33

Tumeona kwamba umoja wa kusudi ni wa lazima kwa ajili ya utendaji wa pamoja; hutupa mwamko wa kufanya kazi kwa bidii katika uga wa huduma. Ili kutambua kusudi la pamoja huhitaji uwekezaji wa muda na nguvu—saa za kazi ngumu lakini yenye furaha. Kuna dhana potofu ulimwenguni kuhusu nini hufanyiza furaha. Mara kwa mara, tunapewa ujumbe kwamba kusudi hasa la maisha ni kufurahi, kitu ambacho kinaelezwa kama burudani za kawaida. Lakini tunawezaje kulinganisha "furaha" kama hiyo na shangwe halisi ya kushiriki ujumbe wa Bahá'u'lláh na watu wengine, ya kuwaona wakiinuliwa na roho ya imani, ya kujishughulisha katika mazungumzo ya maana pamoja na familia za washiriki wa madarasa ya watoto na vikundi vya vijana chipukizi, ya kushuhudia wale wanaosoma mlolongo mkuu wa kozi za taasisi wakipiga hatua katika uelewa wao na uwezo kwa ajili ya huduma? Ikiwa daima katika shughuli za pamoja tamaa ya starehe na kujiachia hukithiri, inaweza kuondolewa kwa kumkumbuka 'Abdu'l-Bahá, Mfano wa kuigwa na jitihada Zake zisizochoka za kueneza Hoja. Hapa kuna baadhi ya Maneno Yake:

> **"Fuateni nyayo za 'Abdu'l-Bahá, na katika njia ya Uzuri wa Abhá, mtamani sana kila wakati kutoa maisha yenu. Ng'aeni kama nyota ya mchana, muwe wasiopumzika kama bahari; mithili ya mawingu ya mbinguni, tawanyeni uhai juu ya konde na kilima, na kama pepo za mwezi Aprili, pulizieni ubichi kupitia miti hiyo ya kibinadamu, na kuifanya ichanue."**[35]

> **". . . mtu anapaswa ayakabidhi kabisa mapenzi yake kwa Mungu, na kuwa msahaulifu kabisa wa masuala yake mwenyewe, ili aweze kulifikia daraja la dhabihu hai: Hivyo, ikiwa atalala, isiwe kwa ajili ya mapumziko ya kimwili, bali kujirudishia nguvu zake ili kwamba maongezi yake yaweze kuwa fasaha zaidi,**

**kauli yake yenye kupendeza zaidi, na kwamba aweze kuwatumikia viumbe wa Mungu na kutangaza mathibitisho Yake; na aamkapo, anapaswa abakie makini, ajishughulishe katika huduma kwa Hoja ya Mungu, na azizamishe kabisa tamaa na mielekeo yake katika mapenzi ya Mungu. Afikiapo kwenye daraja hili, mathibitisho ya Roho Mtakatifu yatamzunguka, na, akiwa amejihami kwa silaha yenye nguvu kama hiyo, atakuwa na uwezo wa kuwakabili watu wote wa dunia."[36]**

**"Natumaini kwamba, kupitia fadhili za Yule Ahuishaye roho, hutaweza kumpumzika hata kitambo kidogo, wala kuzuiwa kupuma kama vile mshipa mkubwa wa damu katika mwili wa ulimwengu, ili daima uweze kupulizia roho ya uzima katika mioyo na kuziwezesha roho kupaa katika milki za juu."[37]**

**"Hawa watafanya kazi bila kukoma, mchana na usiku, hawatajali majaribu wala majonzi, hawataruhusu uahirishaji katika jitihada zao, hawatatafuta kupumzika, watapuuzia raha na starehe zote, na, wakijitenga na bila mawaa, wataweka wakfu kila muda upitao upesi wa maisha yao kwa ajili ya utawanyaji wa manukato matakatifu na utukuzaji wa Neno takatifu la Mungu. Nyuso zao zitatoa mwangaza wa furaha ya mbinguni, na mioyo yao kujawa na shangwe. Roho zao zitavuviwa, na msingi wao kusimama salama. Watatawanyika ulimwenguni, na kusafiri katika maeneo yote. Watapaza sauti zao katika kila mkutano, na kuumba na kuuhuisha kila mkusanyiko. Watazungumza kila lugha, na kufasiri kila maana iliyofichwa. Watafunua siri za Ufalme, na kudhihirisha kwa kila mmoja ishara za Mungu. Watawaka kwa wangavu mithili ya mshumaa katikati ya kila mkutano, na kung'aa kama nyota juu ya kila upeo. Pepo nyanana zivumazo kutoka bustani ya mioyo yao zitatia marashi na kufufua roho za watu, na funuo za akili zao, mithili ya manyunyu, zitawatia tena nguvu watu na mataifa ya ulimwengu."[38]**

## SEHEMU YA 34

Chombo kimoja muhimu tulichopewa kutusaidia kujenga na kuimarisha umoja wetu na kudumisha mantiki ya kusudi ni ushauriano. Ni kupitia vitendo, tafakari juu ya vitendo na ushauriano kwamba tunaweza kupata umoja wa fikra. Umoja wa fikra—kuhusu asili ya shughuli zetu na kuhusu njia tunazotumia na malengo tunayoweka—ni hitaji lingine la utendaji uliounganika wenye ufanisi.

Kadiri kiini kipanukacho cha marafiki kinavyotenda kwa mfululizo na kwa umoja wa fikra, kinapaswa kiendelee kuimarisha uwezo wake na nidhamu ya kutafakari mara kwa mara juu ya ufaaji wa vitendo vyake. Katika kutafakari, kushauriana, na kusoma, kiini huchota kutoka tajiriba na kutoka vifungu husika kutoka maandiko, hususan mwongozo kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Wakati ruwaza hii ya vitendo, tafakari, ushauriano na usomaji inapokuja kueleza jinsi kikundi cha marafiki kinavyofanya kazi kwa pamoja, ujifunzaji unakuwa mtindo wao wa utendaji. Ukuaji endelevu unawezekana, kadiri wao wanavyojenga juu ya nguvu ambazo wamezipata duru hadi duru. Ili kudumisha nguvu za shughuli zetu, kuwahusisha watu wa asili zote, kusimamia shughuli za idadi kubwa—kwa ufupi, kuendelea kukua—hili ndio lengo la kujifunza katika klasta kila mahali:

**". . . hebu marafiki wasijizuie katika juhudi zao kuongeza kiwango cha ushiriki. Hebu wakaza kila neva kuhakikisha kwamba mfumo ambao ambao wameuinua**

**kwa jitihada kubwa haujikunji wenyewe bali huendelea kupanuka kwa kuwakumbatia watu wengi zaidi na zaidi. Hebu wasipoteze mwelekeo wa upokevu wa ajabu walioupata—la, hisia ya matarajio yenye shauku yaliyowasubiri—kadiri walivyoendelea kujenga imani katika uwezo wao wa kuchangamana na watu wa hali za maisha na kuongea nao kuhusu Utu wa Baha'u'llah na Ufunuo Wake."**[39]

1. Tusijizuie kufanya jitihada zozote kuongeza nini? ______________________________

   ____________________________________________________________________________

2. Tukaze kila neva kuhakikisha nini? ____________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

3. Tusipoteze mwelekeo wa nini? _______________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

4. Kiini kipanukacho ambapo wewe ni mjumbe wake bila shaka kimepata umaizi mwingi katika mchakato wa ukuaji katika kijiji au ujirani wako kadiri unavyoendelea kutenda, ukitafakari juu ya vitendo, na kushauriana pamoja. Katika hili, utakuwa umeona kwamba kuna uhusiano wa kutendeana kati ya shughuli mbili: ujenzi wa uwezo katika watu binafsi kwenye njia ya huduma iliyochorwa na kozi za taasisi na ongezeko katika ukubwa wa shughuli na idadi ya wale wanaozishiriki. Jadili juu ya baadhi ya umaizi ambao umeupata kuhusu uhusiano huu na umuhimu wake kwenye mchakato wa ukuaji.

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

Ili kutafakari zaidi juu ya matokeo ya ujifunzaji kama njia ya utendaji na juu ya ruwaza ya vitendo, tafakari, ushauriano na usomaji ambavyo huvielezea wazi, soma vifungu vifuatavyo kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Wakati unafanya hivyo, fikiria kuhusu kiini cha marafiki ambacho wewe ni sehemu yake na ambacho unahudumu pamoja nacho kwa dhati kabisa katika kijiji au ujirani wako.

**"Tunafurahi kuona kwamba katika idadi iongezekayo ya klasta, na katika ujirani na vijiji vilivyomo ndani mwake, kiini cha marafiki kimeibuka ambao kwa kupitia utendaji na tafakari wanagundua kile kinachohitajika, kwa wakati maalum, ili mchakato wa ukuaji usonge mbele katika mazingira yao. Wanachota**

**kwenye chombo chenye nguvu cha taasisi, ambapo kupitia kwacho uwezo wa kuchangia kwenye usitawi wa kiroho na kimwili wa jumuiya huchochewa, na wakati watendapo, idadi ya wale wanaojumuika nao inaongezeka. Kwa kawaida, hali hutofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka sehemu moja hadi nyingine, kama ilivyo kwa sifa bainifu za ukuaji. Lakini kwa kupitia upambanaji wa kiutaratibu, kila mmoja anaweza kutoa mchango unaofaa zaidi na zaidi kwa kazi iliyopo mbele yetu. Katika kila hali, kuna shangwe takatifu katika kuzishirikisha roho zingine katika mazungumzo ya maana na yainuayo moyo ambayo husababisha, ama kwa haraka au taratibu, msisimko wa athari za kiroho. Kadiri mwale uliowashwa katika moyo wa muumini ulivyo mwangavu zaidi, ndivyo itakavyokuwa kubwa zaidi nguvu ya mvuto ihisiwayo na wale wanaopata joto lake. Na kwa moyo ulioteketezwa kwa upendo wa Bahá'u'lláh, ni kazi gani ifaayo zaidi inayoweza kufikiriwa kuliko kutafuta moyo wa undugu, kuwatia moyo kadiri waingiavyo katika njia ya huduma, kuambatana nao kadiri wapatavyo tajiriba na—pengine shangwe kuu kabisa ya zote—kuona roho zikithibitishwa katika imani yao, zikiinuka kwa kujitegemea, na kuwasaidia wengine kwenye safari hiyo hiyo. Haya ni miongoni mwa mambo yahusudiwayo kabisa kushinda yote ya nyakati zote ambapo maisha haya ya mpito hudiriki."[40]**

**"Ujifunzaji kama njia ya utendaji huhitaji kwamba wote wajitwalie mwelekeo wa unyenyekevu, hali ambamo mtu huwa msahaulifu wa nafsi, akiweka imani kamili kwa Mungu, akitegemea uwezo Wake udumishao vyote na akiamini katika msaada Wake usioshindwa, akijua kwamba Yeye, na Yeye pekee, huweza kumgeuza kisubi kuwa tai, tone kuwa bahari isiyo mipaka. Na katika hali kama hiyo roho hufanya kazi pamoja bila kukoma, zikifurahia si zaidi sana katika mafanikio yake zenyewe bali katika maendeleo na huduma za wengine. Hivyo ni kwamba fikra zao hukaziwa wakati wote kwenye kusaidiana mmoja kwa mwingine kukwea vilele vya huduma kwa Hoja Yake na kupaa katika mbingu ya elimu Yake."[41]**

## SEHEMU YA 35

Bila shaka tunajua vyema kwamba mafanikio ya jitihada zetu, duru baada ya duru yanategemea kabisa juu ya msaada mtakatifu. Ni kwaida kwa hiyo kwamba, katika maongezi yetu ya faragha na Mungu, tunamsihi Yeye kwamba jitihada zetu, hata zikiwa ndogo jinsi gani, ziweze kukubaliwa kwenye Kizingiti Chake Kitakatifu. Ni thamani jinsi gani kuvikumbuka vifungu kama hivi:

**"Ee Bwana! Mimi ni ndege aliyevunjika mabawa na anayetamani kupaa katika anga Yako isiyo na mipaka. Nitawezaje kufanya hivi isipokuwa kupitia majaliwa na neema Yako, uthibitisho na msaada Wako."[42]**

**"Nakusihi Wewe, kwa Yule Ambaye ni Chanzo cha Ufunuo Wako na Chimbuko la Ishara Zako, kuufanya moyo wangu kuwa chombo cha kupokea upendo Wako na cha kumbukumbu Yako. Uufume, basi, kwa Bahari Yako kuu kabisa, ili kutoka kwayo yaweze kutiririka maji ya uzima ya hekima Yako na vijito angavu vya utukuzo na sifa Zako na sifa."[43]**

**“Nakuomba Wewe, Ewe Mfalme wa uwepo na Mlinzi wa vionekanavyo na visivyoonekana, kumfanya yeyote ainukaye kuitumikia Hoja Yako kama bahari ijongeayo kwa mapenzi Yako, kama yule awakaye kwa moto wa Mti Wako Mtakatifu, aking’aa kutoka upeo wa mbingu ya amri Yako.”[44]**

**“Ee Mungu wangu, Msaidie mtumishi Wako kuinua Neno, na kukanusha yale ya upuuzi na uwongo, kusimamisha ukweli, kueneza mbali aya takatifu, kufunua utukufu, na kuufanya mwangaza wa asubuhi kupambazuka katika ya mioyo ya wanyofu.”[45]**

**“Ee Mungu wangu! Ee Mungu wangu! Wewe waniona katika unyenyekevu na unyonge wangu, nikishughulika na kazi kubwa mno, nikidhamiria kuinua neno Lako miongoni mwa watu wengi na kueneza mafundisho Yako miongoni mwa watu Wako. Nitawezaje kufanikiwa vinginevyo Wewe umenisadia kwa pumzi ya Roho Mtakatifu, nisadie kushinda kwa majeshi ya ufalme Wako mtukufu, na nyunyiza juu yangu mathibitisho Yako, ambayo pekee yaweza kugeuza kisubi kuwa tai, tone la maji kuwa mito na bahari, na atomu kuwa miangaza na jua?”[46]**

Pia tunakutana pamoja kumuomba Mwenyezi kwamba Yeye ajalie mathibitisho juu ya jitihada zetu za pamoja, hususan wakati wa kampeni shadidi.

**“Ee Bwana! Dhihirisha katika nchi Zako roho nyenyekevu na tiifu, nyuso zao zikiangaziwa kwa mionzi ya uongozi, zikijitenga na ulimwengu, zikitukuza Jina Lako, zikitamka sifa Zako, na zikitawanya manukato ya utukufu Wako miongoni mwa wanadamu.”[47]**

**“Ee Mungu, Mungu wangu! Wasaidie watumishi Wako waaminifu kuwa na mioyo ya upendo na miororo. Wasaidie kueneza, miongoni mwa mataifa yote ya dunia, mwanga wa uongozi ambao hutoka Kundi la juu.”[48]**

**“Kwa kweli, wapendwa Wako wana kiu, Ee Bwana wangu; uwaongoze kwenye chemchemi ya baraka na neema. Kwa kweli, wana njaa; watelemshie meza Yako ya mbinguni. Kwa kweli, watupu; wavike mavazi ya elimu na maarifa.”[49]**

**“Ewe Mungu usiye na kifani! Ewe Bwana wa Ufalme! Roho hizi ni jeshi Lako la mbinguni. Wasaidie na, kwa jeshi la Umati Mkuu, uwafanye washindi, ili kila mmoja wao aweze kuwa kama jeshi na kuzishinda nchi hizi kupitia upendo wa Mungu na mwangaza wa mafundisho matakatifu.”[50]**

## SEHEMU YA 36

Tutahitimisha hapa uchunguzi wetu wa kitendo cha kufundisha. Bila shaka, kwa kufikiria kuhusu ufundishaji siyo tu kama juhudi ya mtu binafsi bali kama jitihada ya pamoja, unatambua kwamba kanuni zile zile za kiroho zinahusika vyote viwili. Na walakini, mchakato wa kuitambulisha Imani kwa marafiki wachache na kuwasaidia kufika kwenye fuko za bahari ya Ufunuo wa Bahá’u’lláh kwa hakika ni tofauti na ule wa kuwasaidia maelfu kwa maelfu ya wakazi wa eneo moja katika kuzikaribia fuko zile zile. Mfano rahisi utafafanua suala hili: Kanuni zinazoongoza ukuaji wa mimea ni sawa sawa na zile katika kitalu kidogo cha maua na

katika shamba lenye ukubwa wa mamia ya hekta. Walakini matunzo ya mimea michache katika bustani binafsi ni tofauti sana na kilimo cha shamba kubwa.

Pale marafiki zako wachache wanapomtambua Bahá'u'lláh na kujiunga na safu za wafuasi Wake, utaendelea kumlea kila mmoja wao kama sehemu ya mpango wako binafsi wa ufundishaji, ukitumia muda pamoja nao na kuwasaidia katika jitihada zao za kukua katika ujuzi wao wa mafundisho Yake na wa kuitumikia Hoja Yake. Sasa geuzia akili yako kwa eneo zima. Pale jitihada miongoni mwa kundi pokevu zinapoonesha kwamba idadi kubwa zaidi, hususan vijana, wapo tayari—na kwa kweli wenye shauku—kutembea katika njia ya huduma kwa jumuiya zao, pale jitihada zinapodhihirisha kwamba asilimia kubwa wapo tayari kuingia katika Imani kupitia mazungumzo yanayofanana na yale yaliyokunjuka kati ya Anna na Emilia, ndipo mchakato tofauti kabisa unapohitajika, ule ambao huwezesha korija kwa korija kuinuka na kuitumikia Hoja kulingana na uwezo wao waliopewa na Mungu. Kazi yenye ukubwa kama huo haiwezi kufikiwa na jitihada za mtu binafsi peke yake.

Sehemu zilizofuata za kitengo hiki zimekupa kianga cha jinsi upanuzi na uimarishaji wa Imani kwa kiwango kikubwa unavyoweza kusonga mbele, bega kwa bega. Vipengele vya mfumo unaoweza kusaidia michakato hii miwili vimegunduliwa kwa juhudi kubwa na kuboreshwa kupitia miongo ya ujifunzaji. Baadhi yake vimetajwa hapa, na utapata umaizi katika vingine na, muhimu zaidi, katika jinsi vinavyofanya kazi kwa pamoja kujenga mfumo imara kupitia tajiriba na masomo yako yanayoendelea. Miongoni mwake ni uundaji wa "klasta", maduru ya shughuli pamoja na awamu zake za upanuzi na uimarishaji, mpango wa uratibu, na mbinu za utendaji, tafakari, ushauriano, na usomaji. Lakini msingi kwa yote hayo ni jambo moja muhimu: mbinu ifaayo ya kujenga uwezo kwa ajili ya kutoa huduma.

Ili kuyajalia makundi yaendeleayo kukua "umaizi wa kiroho, ujuzi, na stadi zihitajikazo kutekeleza kazi nyingi za upanuzi uliochapuzwa na kuimarishwa, taasisi ya mafunzo iliundwa. Kwa chombo hiki chenye "uwezo usio na kikomo", Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huandika, inawezekana, "katika hali nyingi anuwai, takriban katika klasta yoyote ile," kwa "kiini kipanukacho cha watu binafsi kuanzisha mjongeo kuelekea lengo la Utaratibu mpya wa Ulimwengu." Kifungu kifuatacho hutujumuishia jinsi ujengaji uwezo ukuzwao na taasisi huendesha kazi ya ufundishaji na kuusukuma mjongeo huu kwenda mbele:

> **"Jambo kuu kwa muundo wa utendaji unaokua katika klasta ni mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja yasababishwao kupitia nguvu ya Neno la Mungu. Kutoka mwanzoni mwa mfululizo wa kozi, mshiriki hukutana na Ufunuo wa Baha'u'llah katika kufikiria mada nzito kama vile ibada, huduma kwa binadamu, maisha ya roho, na elimu ya watoto na vijana. Kadiri mtu akuzavyo tabia ya kujifunza na tafakari ya undani sana juu ya Neno la Uumbaji, mchakato huu wa mbadiliko hujidhihirisha wenyewe katika uwezo wa kuelezea uelewa wake wa dhana za ndani sana na kuchunguza uhalisia wa kiroho katika mazungumzo ya maana. Uwezo huu huonekana sio tu katika majadiliano ya hali ya juu ambayo huzidi kuainisha muingiliano ndani ya jumuiya, bali katika mazungumzo yaendeleayo ambayo hufika mbali zaidi—si kidogo kati ya vijana wa Kibaha'i na wale wa rika lao—huendelea kujumuisha wazazi ambao binti na vijana wao wanafaidika kutokana na programu za kielimu za jumuiya. Kupitia mabadilishano ya aina hii, ufahamu wa nguvu za kiroho hukuzwa, uwili uonekanao hujiachia kwa umaizi usiotarajiwa, hisia ya umoja na wito wa pamoja huimarishwa, imani kwamba ulimwengu bora zaidi unaweza kuundwa kuimarishwa, na kujifunga kwa utendaji hudhihirika. Mazungumzo kama haya ya kipekee pole pole huvutia**

**daima idadi kubwa zaidi kushiriki katika mlolongo wa shughuli za jumuiya. Mada za imani na yakini kiasili huibuka, zikishawishiwa na upokevu na uzoefu wa wale wahusikao. Kilicho dhahiri, basi, ni kwamba kadiri mchakato wa taasisi katika klasta upatavyo mwendo, kitendo cha ufundishaji huja kujitwalia umashuhuri zaidi katika maisha ya marafiki."**[51]

Lazima kiwe chanzo kikubwa cha shangwe kwako kujua kwamba kwa kushiriki katika kozi za taasisi, unatimiza muono wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ulioelezwa hapo juu. Vile vile utafurahi kujua kwamba kitabu kitakachofuata utakachokisoma kitakusaidia kukuza uwezo wako wa kuhudumu kama mkufunzi wa kozi za Taasisi ya Ruhi. Kitendo hiki cha huduma siyo tu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya msururu thabiti unaoendelea kupanuka wa watu binafsi kupitia kozi za taasisi bali pia mchakato mzima wa ukuaji ndani ya klasta. Kazi yako ya mara moja hata hivyo, ni kuweka katika vitendo kile ulichojifunza katika kitabu hiki. Baada ya kuimarisha uelewa wako kuhusu umuhimu wa ufundishaji, ni upeo gani wa furaha unaoweza kuufikiria kuliko kuzingatita mwito wa Mlinzi kwetu sisi sote "kuufanya kuwa shauku itawalayo maisha yetu."

# MAREJEO


1. *Siku za Ukumbusho: Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh kwa ajili ya Siku kuu za Kibaha'i* (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá'i ya Ulimwengu, 2016), na. 29.13, uk. 147, Kiingereza.

2. Shoghi Effendi, *Majilio ya Haki Takatifu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í', 2002, chapisho la 2018), aya. 73, uk. 72, Kiingereza.

3. Kutoka ujumbe wa 13 Julai 1964 kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, uliochapishwa *katika jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 1963–1986: Kipindi cha Tatu cha Zama za Ujenzi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í', 1996), na. 18.4, uk. 39.

4. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í', 1983, chapisho la 2017), CXX, aya. 3, uk. 288.

5. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í', chapisho la 2003, chapisho la 2022), Kiarabu na. 4, uk. 4.

6. *Buga kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh*, IV, aya. 1, uk. 5.

7. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo 28 Oktoba 1911, iliyochapishwa katika *Mazungumzo ya Paris* (Hekima ya 'Abdu'l-Bahá)*: Mazungumzo Yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá mwaka 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í', chapisho la 2006, 2016), na. 15.12, uk. 53.

8. Bahá'u'lláh, kati *Sala za Kibahá'í: Uteuzi* wa *Sala Zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh, Báb, na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í', chapisho la 2002, 2020), uk. 303, Kiingereza.

9. *Buga kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh*, XLV, aya. 1, ku. 111–12. Kiingereza.

10. Báb, katika *Sala za Kibahá'í*, uk. 221.

11. Kama hapo juu, uk. 55.

12. Bahá'u'lláh, kama hapo juu, uk. 4.

13. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiajemi na. 44, uk. 37.

14. Kama hapo juu, Kiarabu na. 13, ku. 6–7.

15. *Nyaraka za Abdul-Baha Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, chapisho la 1916, 1930), tol. 3, ku. 579–80.

16. Bahá'u'lláh, katika *Sala za Kibahá'í*, uk. 162, Kiingereza.

17. Kutoka ujumbe wa Riḍván 2010 ulioandikwa kwa Wabahá'í wa ulimwengu, uliochapishwa katika *Miundo ya Utendaji: Jumbe Zilizoteuliwa za Nyumba ya Haki ya*

*Ulimwengu na Nyenzo za Nyongeza, 2006–2016* (West Palm Beach: Shirika la Uchapishaji Palabra, machapisho, 2017), na. 14.4, uk. 76.

18. Kutoka barua ya 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Mabara la Washauri, uliochapishwa katika *Mpango wa Miaka Tisa, 2022–2031: Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (West Palm Beach: Shirika la Uchapishaji Palabra, machapisho ya 2022), na. 6.9, uk. 47.

19. *Buga kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXIX, aya. 1–2, ku. 316–17.

20. Shoghi Effendi, *Majilio ya Haki Takatifu*, aya. 78, ku. 76–77, Kiingereza.

21. Kama hapo juu, aya. 78, uk. 77.

22. Kama hapo juu, aya. 78, ku. 77–78.

23. Kama hapo juu, aya. 78, uk. 78.

24. Kama hapo juu.

25. Kama hapo juu.

26. Kutoka barua ya 28 Desemba 2008 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa, aya. 4.

27. Kutoka ujumbe wa Riḍván 2010 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'í wa ulimwengu, uliochapishwa katika *Miundo ya Utendaji*, na. 14.6, uk. 77.

28. Kutoka barua ya 13 Julai 1964 kwa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, iliyochapishwa katika *Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 1963–1986*, na. 18.1–2, ku. 38–39.

29. Kutoka barua ya 12 Desemba 2011 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, iliyochapishwa katika *Miundo ya Utendaji*, na. 20.19, uk. 136.

30. 'Abdu'l-Bahá, iliyonukuliwa katika barua ya 5 Juni 1947 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, iliyochapishwa katika *Chimbuko la Imani: Jumbe kwa America, 1947–1957* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1965, chapisho la 2014), ku. 29–30, Kiingereza.

31. *Mateuzi kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, chapisho la 2015), na. 207.9–10, ku. 364–65.

32. Tanbihi katika hati ya mwandiko wa Shoghi Effendi, iliyoandikwa juu ya barua ya 9 Mei 1933 iliyoandikwa kwa niaba yake kwa mtu binafsi.

33. *Buga kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXLVI, aya. 1, uk. 357.

34. Kutoka ujumbe wa Riḍván 2008 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'í wa ulimwengu, uliochapishwa katika *Miundo ya Utendaji*, na. 10.2, uk. 62, Kiingereza.

35. *Mateuzi kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 200.11, ku. 339–40.

36. *Nyaraka za Abdul-Baha Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1915, chapisho la 1940), tol. 2, uk. 460.

37. *Nyaraka za Abdul-Baha Abbas*, tol. 3, uk. 727.

38. *Mateuzi kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 204.2, uk. 347–48.

39. Kutoka barua ya 28 Decemba 2010 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Kongamano la Bodi za Mabara za Washauri, uliochapishwa katika *Miundo ya Utendaji*, na. 16.15, uk. 103, Kiingereza.

40. Kutoka Ujumbe wa Riḍván 2019 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'í wa ulimwengu, aya. 3.

41. Kutoka Ujumbe wa Riḍván 2010 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'í wa ulimwengu, uliochapishwa katika *Miundo ya Utendaji*, na. 14.20, uk. 84, Kiingereza.

42. 'Abdu'l-Bahá, katika *Sala za Kibahá'í*, uk. 204.

43. Bahá'u'lláh, kama hapo juu, ku. 192–93.

44. Kama hapo juu, ku. 194–95.

45. 'Abdu'l-Bahá, katika *Sala za Kibahá'í*, uk. 197.

46. Kama hapo juu, uk. 210.

47. Kama hapo juu, uk. 207.

48. Kama hapo juu, uk. 198.

49. Kama hapo juu, uk. 199.

50. Kama hapo juu, uk. 201.

51. Kutoka ujumbe wa 29 Decemba 2015 kwa Kongamano la Bodi za Mabara la Washauri, uliochapishwa katika *Mpango wa Miaka Mitano, 2016–2021: Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (West Palm Beach: Shirika la Uchapishaji Palabra, machapisho ya 2016), na. 1.14, ku. 8–9.